ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/ Waziri wa Afya/ /Jimbo la Ziwani.
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.

23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Said Hassan Said	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni

53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
77.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	Jimbo la Jang'ombe
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Kumi na Tano - Tarehe 30 March, 2015

(Kikao kilianza Saa 3.00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, *(Pandu Ameir Kificho)* alisoma Dua

HOJA ZA KAMATI

Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Kuchunguza Upotevu wa Nyaraka:

Ripoti ya Kamati Teule ya Kuchunguza Upotevu wa Nyaraka.

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Amina Idd Maborouk: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia asubuhi ya leo kuwa wazima na afya njema, pia, nitoe shukurani zangu za dhati kabisa kwa Kamati Teule kwa kazi nzuri waliyoifanya, lakini hasa nichukue nafasi hii kwa kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati hii Mhe. Mahamoud Mohammed Mussa na wajumbe wake wote kwa kufanya kazi hii kwa uadilifu mkubwa. Lakini hata hivyo wamefanyakazi hii kwa muda mfupi lakini pia kwa mazingira magumu.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba kazi waliyoifanya ni nzuri sana kwa kushirikiana na taasisi hii husika lakini na vyombo vya Polisi, mimi nianze tu kwa kusema kwamba ripoti hii imekamilika na tunaamini kuwa sote tuliokuwemo kwenye Baraza hili tukufu tunaikubali na tunaiunga mkono mia juu ya mia.

Mhe. Naibu Spika, ni wazi kwamba yaliyokuwemo katika ripoti hii yapo wazi na yana ukweli kabisa, wala hayana ubishi na yanakubaliana na matokeo ya uchunguzi ambao umefanywa na taasisi nyingine kama Jeshi la Polisi na Uongozi wa Idara ya Nyaraka wenyewe. Ripoti kama tumeipitia vizuri kwa makini na kwa ukamilifu ikiwemo kupitia viambatisho mbali mbali vya ripoti hii, ni dhahiri nyaraka zilikuwa hazipo na zimeibiwa na muhusika mkuu anajulikana na kwa jina anaitwa Humoud.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba waliotajwa katika ripoti hii inawezekana ni hao wawili au zaidi ya wawili. Kwa hivyo, imani yangu ni kwamba wizi huu ulikuwa ni mpango wa muda mrefu na mkakati maalum na ilikuwa inatafutwa nafasi muafaka tu ili ziweze kuchukuliwa nyaraka hizi

Mhe. Naibu Spika, si jambo la kawaida kwamba Ofisa wa Mahusiano ya Habari wa nchi nyengine lakini aletwe katika nchi nyengine na aanze kushughulikia shughuli za nyaraka za nchi nyengine. Kwa kweli hili jambo linasikitisha sana na kama Serikali tuiombe ichukue hatua muafaka katika kulishughulikia suala hili.

Mhe. Naibu Spika, baada ya matokeo ya wizi wa nyaraka hakukuwa tena na zoezi ambalo la kuhifadhi hizi nyaraka na kwa habari ya ripoti hii kwamba mtuhumiwa huyo ambaye anaitwa Humoud alikuja hapa tokea mwaka 2005, alikuwa anakuja na kurudi, lakini mwisho ikaonekana kwamba kazi aliyotumwa haifanyiki ipasavyo ikaonekana bora awepo katika Ofisi ndogo ya Ubalozi wa Oman. Ninavyoamini mimi kwa dhati ya moyo wangu kwamba huyu Humoud ametumwa kwa muda wote huo tokea 2005 na alikuwa anawekewa mazingira mazuri yaliyomtuma na kumuwezesha kufanikisha wizi huo na hadi leo kuzipata hizi nyaraka.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba Zanzibar ina mahusiano mazuri sana na wenzetu wa Oman na kwamba tunatakiwa suala hili tulishughulikie kwa uangalifu, lakini vile vile mimi niseme kwamba tusisahau kwamba hii ni nchi ambayo ina mamlaka yake kamili na ina maslahi yake na miongoni mwa maslahi ya nchi ni nyaraka zake, kwa sababu ndio kielelezo kukubwa cha kuwepo kwa nchi yenyewe. Mimi nasema tusiogope kupoteza maslahi yetu kwa sababu tutaathiri mahusiano penye haki ya kutetea maslahi yetu lazima tuyatetee.

Mhe. Naibu Spika, sote tunafahamu kwamba mahusiano ya Marekani na Israil ni mashirikiano mazuri kuliko pengine nchi zote duniani, lakini Marekani walipojua kwamba Waisrail wanataka kuwafanyinya upepelezi wamarekani wali-*react*. Kwa hivyo. Mimi niombe Serikali yetu lazima tu-*react* kwa sababu hii ni nchi kamili, lakini pia ku-*react* kwa Serikali yetu ni kulinda na kutetea maslahi ya Wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa maoni yangu nafahamu kwamba Humoud aliwekwa katika Ofisi ya Ubalozi makusudi kwa sababu likitokea hili lililotokea isiwe rahisi kupelekwa katika vyombo vya sheria na ndivyo ilivyo sasa. Hata hivyo njia mbadala za kumshughulikia Humoud na naomba basi Serikali izitumie hizo njia mbadala za kuweza kumshughulikia Humoud, lakini si hivyo tu na nyaraka zote ambazo ameziiba tuhakikishe kwamba zinarejeshwa katika Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kupitia ripoti hii kwa umakini kabisa na kuangalia mahojiano mbali mbali ambayo yamefanywa kwa wafanyakazi kwamba suala hili lingeweza kudhibitika, kama wafanyakazi wangeweza kuwa na uzalendo mkubwa na kuipenda nchi yetu, lakini pia na kuwa waaminifu wakubwa wa Taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu inaonekana kwamba huyu Humoud alikuwa familia katika taasisi hii ya nyaraka, kama ukiangalia vizuri katika ripoti hii wafanyakazi walio wengi katika Ofisi hii walikuwa wanamjua Humoud, hata walipokuwa wanaulizwa walikuwa wanasema kwamba Humoud alikuwa anapiga simu kwa baadhi ya wafanyakazi na alikuwa anawaita, anawaambia waibe nyaraka na wengine walikuwa wanakataa kuiba hizo nyaraka, lakini wengine alikuwa anawapigia simu kwa kutumia namba nyengine.

Lakini walipokuwa ofisini kwao baada ya kuzungumza baina yao na wafanyakazi wengine walikuwa wanasema huyo ni Humoud na kubwa anataka ziibiwe nyaraka. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, hili jambo si la kulipuuza na kama wafanyakazi hawa wangekuwa na moyo kama nilivyosema mwanzo wana moyo wa uzalendo wangetoa ripoti na wamesema humu katika ripoti kwamba walikuwa wanatoa ripoti kwa mabosi wao. Lakini mwisho wake ilikuwa hakuna hatua yoyote inayochukuliwa.

Lakini si hivyo Mhe. Naibu Spika, kuna mfanyakazi mmoja aliitwa katika kuhojiwa na alisema kwamba na mimi ningeiba hizi nyaraka ningetajirika kama walivyotajirika mabosi wangu. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, mimi niiombe Serikali kauli hii ambayo imetolewa na huyu mfanyakazi si ya kupuuzwa, ni kauli nziri na naiomba Serikali yetu ilishughulikie suala hili.

Mhe. Naibu Spika, Waswahili wanasema; "ukimcheleya mwana kulia utalia wewe".

Kwa hivyo, mimi niiombe Serikali kwa sababu mara zote tunakuwa tunasema katika baraza hili katika chombo hiki, lakini mwisho wa habari hakuna linalokuwa na inawezekana hapa tunasema sana lakini hatimae unakuta kwamba huyu Humoud hajachukuliwa hatua yoyote lakini pia na hizo nyaraka hazijarudishwa katika Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme kwamba wengi wamezungumza vya kutosha na kama walivyosema wenzangu tunaweza kusema hapa mpaka kipovu kikatutoka lakini hatimae hakuna lilinalochukuliwa, mimi niiombe Serikali kwa kusema hivi sasa hivi upo umuhimu mkubwa wa kuzipitia nyaraka zote zilizokuwepo hapa Zanzibar na inawezekana kwamba kuna baadhi ya nyaraka hazimo lakini hatujui na zifanyiwe utafiti nyaraka zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa gharama yoyote, kwa sababu naamini kwamba si jambo rahisi sana linahitaji fedha, lakini naamini kwamba kwa jambo hili ambalo ni *sensitive* na ni muhimu sana kwa maslahi ya Taifa letu, Serikali haishindwi kupata pesa za kufanyia utafiti wa nyaraka zetu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kusema kwamba mimi nikubaliane mia kwa mia na Ripoti ya Kamati Teule kwa asilimia mia moja na naamini kwamba Serikali inatusikia na mwisho wake watatuletea taarifa kamili ya hatua zilizochukuliwa katika kulifuatilia suala hili.

Baada ya kusema hayo nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujaalia kufika hapa leo asubuhi tukiwa wazima wa afya na kuweza kuendelea na kadhiya tuliyojia hapa.

Mhe. Naibu Spika, nikushukuru wewe pia kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweza kuchangia machache yanayohusiana na upotevu wa nyaraka kama ripoti tuliyowasilishiwa hapa barazani, mimi kama wengine nimesikitishwa sana na kadhiya hiyo ambayo imetokea katika Taifa letu na ni masikitiko kwa sababu nyaraka ambazo zimepotea ni nyaraka zenye umuhimu mkubwa sana kwa ajili ya historia, lakini vile vile kwa ajili ya maendeleo yetu. Kama tunavyofahamu umuhimu wa nyaraka hasa katika masuala ya kujua tulikotoka na wapi tunataka kuelekea.

Mhe. Naibu Spika, nikiungana na wenzangu wote ambao wamezungumzia suala hili la upotevu wa nyaraka na ninakubali yale ambayo yameshauriwa na wote waliosimama hapa kwamba lazima hatua zichukuliwe, mimi nilikuwa ni mmoja katika watu ambao walihojiwa na kamati hii na nilihojiwa kutokana na mchango wangu nilioutoa nimeweza kueleza kwa nini basi ziko nyaraka ambazo haziko katika maeneo yetu.

Na Mhe. Naibu Spika, nilisema kwamba lazima kutakuwa na wizi ambao umetokea, kwa kweli niliweza kupata nafasi ya kutembelea nchi ya Ujerumani na kwa bahati kulikuwa na mtu mkubwa ambaye anashughulika na masuala ya nyaraka katika safari ile na tulipokwenda *Archive* ya Ujerumani tuliona nyaraka za Zanzibar ambazo ziko kule na tukaulizana pale na tukaambiwa kwamba hizi Zanzibar hazipo, lakini zilikuwa ni nyaraka muhimu kwa sababu zilikuwa zinaelezea historia ya Zanzibar na namna Zanzibar ilivyoanza biashara na mataifa ya nje, nakumbuka kipindi hicho tulikuwa tunatimiza miaka mia ya mahusiano wa Zanzibar na Ujerumani na Zanzibar ina historia kubwa sana ya Ujerumani, nafikiri wengine wenzangu ambao wanafahamu nini historia ya Zanzibr na kwa bahati hata kuna kisiwa ambacho kilikuwa kinaunganishwa Zanzibar na Ujerumani na kwamba kisiwa kile kina eneo maalum linalohusiana na historia ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, hili ni jambo muhimu sana na Zanzibar haikuwa na uhusiano na nchi moja tu katika dunia hii lakini tulikuwa na uhusiano na nchi nyingi, lakini huko tulikotoka tulikuwa na historia kubwa sana, lakini historia ile ndio iliyotuweka leo tuwepo hapa. Sasa historia ile sasa hivi imeshachujwa na imeshaondoshwa katika Taifa letu kwa kweli ni masikitiko makubwa, lakini mimi nataka kusema tu kwamba nidhamu imepotea katika Taifa letu, nidhamu imepotea na tunaifumbia macho na mimi naamini na najua kwamba uko utaratibu ambao tunatakiwa tuutumie kama ikiwa ni kiongozi, lakini kama ni mtendaji wa pahala popote lazima ufuate utaratibu unaotakiwa.

Hukuufuata umekwenda kinyume na utaratibu ule, wewe hufai, sasa hawa watu wamenyamaziwa kwa muda mrefu kwa sababu kadhia hii imekuwa ikionekana na ikijulikana kwa muda mrefu, hii ripoti sio jambo geni tunaonyeshwa humu kwamba tayari kulikuwa na wasi wasi kwamba haya mambo yanatendeka.

Lakini nidhamu ile inatakiwa ichukuliwe hatua, wanaochukua hatua ama wanadharau ama wanafanya uzembe, haiwezekani nyaraka muhimu kama hizi zianze kupotea kidogo kidogo na watu ambao wanahusika wapo pale hawazioni, lakini hata kuwa na utaratibu wa kuzichunga na kuziangalia zile nyaraka haupo, hilo ni kosa kubwa sana. Sasa wale watu wanawekwa kufanya nini pale. Kama ni kuweka watu kupata mshahara basi ni bora wakae majumbani wapelekewe mishahara yao. Lakini sio kwenda ofisini wakajifanya wanafanya kazi halafu nyaraka zetu wakazichukua, wakaziuza, wakazipoteza na wakafanya wao wanavyotaka.

Mhe. Naibu Spika, hii inatugharibu sana katika utendaji wetu wote, kwa kuwa hatuna nidhamu, tunawaumiza wananchi wetu. Mimi ningeiomba sana Serikali. Mimi hii kadhia sitaki kuizungumza kwa sababu nimeshaizungumza kipindi kilichopita. Lakini ripoti hii inaonyesha udhaifu wa uchukuliaji wa hatua. Ikiwa tutaendelea hivi na kila mmoja atafanya anachokitaka, tutalifikisha mbali Taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, humu katika ukurasa wa 33 katika ripoti hii inonyesha dhahiri kabisa kwamba kuna uzembe ambao umefanyika. Ripoti inasema katika ukurasa wa 33, ripoti inasema kwamba; "Watu waliopewa dhamana ya kusimamia taasisi hii walishindwa kutekeleza wajibu wao. Kutokana na kushindwa kutekeleza wajibu wao hatimaye kutoa nyaraka kwa matukio ya wizi na hujuma kufanyika". Sasa anayeiba afanywe nini? Swali, sheria zetu zipo, mwizi anahukumiwa, tusijue kuhukumu wanaoiba kuku tu au wanaoiba mazao na hawa wanastahiki vile vile sheria inawabana.

Mhe. Naibu Spika, inasikitisha kwamba wanyonge ndio unaowakuta kule gerezani, lakini sisi hatupatikani kule gerezani, kwa nini? Na hawa wanyonge wanaiba kidogo tena waibia wanyonge wenzao. Lakini wengine wanaibia Taifa ambayo ni rasilimali itakayoweza kuinufaisha *generation* kwa *generation*.

Mhe. Naibu Spika, tunaunda vitengo vya kushughulikia mambo haya, lakini vitengo vile hatuvipi nguvu ya kushughulikia mambo haya. Matokeo yake mambo haya yanaendelea mpaka lini? Inasikitisha sana. Wizi kuibia Serikali na kuibia nchi, ni uhaini mkubwa jamani. Mimi ningeomba sana Serikali ilisimamie hili.

Mhe. Naibu Spika, naomba tusipuuzwe Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao tumechaguliwa na wananchi. Tunaposimama hapa tunatetea wananchi, hizi ni rasilimali zao. Sisi wametutuma kuja hapa kuwatetea na kuisimamia Serikali. Tunapoisimamia Serikali maana yake tunataka Serikali uchukue hatua, ndio maana ya kuisimamia Serikali. Ina maana Ripoti hii Serikali tunaiomba sana ichukue, lakini ipewe kazi taasisi inayohusika, tunayo taasisi inayohusiana na masuala ya rushwa, ipewe kazi hiyo ndiyo maana yake na wende wakafanya uchunguzi. Kwa kadhia hii ikafanye uchunguzi na zaidi ya taasisi hizo zipo na nyengine.

Mhe. Naibu Spika, mimi kinachonishangaza na kwa kweli huwa kinanishangaza sana na naomba niseme. Juzi tu hapa tumepitisha Mswada wa Maadili ya Viongozi. Tumepitisha wote sisi tulikuwa tumefurahi sana, kwa sababu tunajua sasa angalau kutakuwa na mfumo maalum wa kuhakikisha kwamba viongozi wetu tunaowaweka katika ngazi mbali mbali hawatofanya jambo lolote ambalo linaweza kuathiri Taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, mimi na wewe na wengine sote tunaishi katika jamii hii, tunajuana na uzuri wa mambo Zanzibar ni ndogo sana. Leo namuona mwenzangu ametoka amwekwenda kufanya kazi sehemu fulani na mimi nimekwenda kwenye kazi ya uwalimu, ambao tunajua walimu namna ya shinda wanazozipata, kipato chao ni kidogo sana. Mtu yule anakwenda kufanya kazi katika eneo fulani ambalo anaweza kupata mambo mbali mbali yatakayomuwezesha mtu yule kwa kipindi cha miaka miwili ana ghorofa tatu. Halafu mtu yule tunamfumbia macho, tunaona hajahusika na chochote, haifai. Sisi ni viongozi tunachukua jukumu hilo, tuhakikishe kwamba watu wanawajibika kutokana na dhamana zao walizopewa.

Mhe. Naibu Spika, mimi namuogopa sana Mungu, kwa hili la kukaa na kutafuta fedha za wananchi, mtu apewe pesa kwa ajili kwamba anauza nyaraka muhimu. Mimi nataka sana mjukuu wangu na kirembwe changu aweze kujua histori ya Zanzibar. Lakini atakapokwenda kusoma atakuwa na uwezo wa kuweza kwenda kwenye *Archives* akafanya *research* kuhusiana na masuala ya historia ya Zanzibar. Tunawanyima vizazi vyetu vijavyo haki zao kama hatujui. Tunawanyima haki zao za kujijua wapi wametoka na kadhia gani imaendelea katika nchi yao. Inatia uchungu sana na watu wanakaa wanafikiria mfuko wao.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme tu kwamba naiyomba sana Serikali jengine ambalo nimeliona humu kwenye ripoti, kulikuwa na mkurugenzi muhusika lakini kwa kipindi kirefu alikuwa hayupo. Sasa hili limekuwa ni tatizo kubwa kama mkurugenzi hayupo na lile eneo lina umuhimu mkubwa, bila shaka sehemu yoyote inataka uongozi, kwa nini hakuna wa kukaimu kwa kipindi ambacho yeye hayupo?

Mhe. Naibu Spika, lakini utaona katika idara mbali mbali vile vile hakuna viongozi wanaohusika. Ndio maana mtu yeyote anatoka kwa sababu mtu yule ana uhusiano na mtu mwengine, anatoka anakwenda kufanya anavyotaka. Jamani hii taasisi haikuwa ya mtu binafsi, hii ni yetu sote. Anapopewa madaraka mtu mmoja akafanya anavyotaka tumuondoe, hafai, hafai Mheshimiwa, hafai kabisa. Zichunguzwe taasisi zinazohusika, aliyeshariki katika upotevu wa nyaraka hizi ahukumiwe kutokana na makosa yake aliyoyafanya. Basi kunyamaziana, kwa sababu tukinyamaza watakaoathirika ni watoto wetu. Basi kuoneana huruma

Mhe. Naibu Spika, kila siku tunapata sifa wenzetu wa Ruwanda wanaendelea kwa kasi mno na hata mataifa ya nje saa nyengine wanamuhukumu Rais wa Ruwanda. Lakini kwa nini wanaendelea. Wanaendelea kwa sababu Rais wa Ruwanda hataki rushwa na haipendi kabisa na mtu yeyote anaefanya jambo lolote la rushwa anajikuta hayupo katika Ofisi yake.

Mhe. Nasibu Spika, Kenye hapa juzi mawaziri watano, makatibu wakuu saba kama si wanane, mpaka wenye viti kwenye baadhi ya Halmashauri wamewekwa pembeni. Wameambiwa waiache Serikali na taasisi zinazohusika kuchunguza ili ijulikane nani aliyefanya vitendo vya ufisadi. Itafika wakati na sisi inabidi tufanye hivyo au tukimuondoa yule, tukimuweka mwengine na mwengine atakaekuja kwa sababu anajua hakuna hatua itakayochukuliwa, atafanya yale yale. Lazima tuwe *serious*.

Mhe. Naibu Spika, mimi nimesimama kutoa joto langu zaidi. Natoa joto langu kwa sababu inanisikitisha na hofu yangu kubwa ipo katika kutizama kizazi chetu kijacho. Sisi tutaondoka watakuja wengine na watakaokuja

tutawaachia nini. Hivi ndio vitu ambavyo tunatakiwa tuwaachie na wao pia wana haki. Lakini ikiwa tutawaachia watu wabinafsi wanaofikiria kubwa ni kujaza mifuko yao, tutaumia sote.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba Serikali uchukue hatua. Hatua ya kuchukuliwa ni kwamba kwa sababu taasisi inayoshughulikia masuala haya ipo, ipewe jukumu hilo. Ningeiomba sana taasisi inayoshughulikia masuala hayo kwa kweli kwa dhati kabisa waifanye kazi hiyo. Tungeomba sana wa-*prove* kwetu sisi kwamba wanaweza kuifanya kazi hiyo. Tumeona mataifa ya wenzetu wanachukua hatua katika masuala haya.

Jamani Rais Nyerere alitwambia kwamba "rushwa ni adui wa haki", tunawanyima haki watu wetu wengine. Ofisi ya Nyaraka ni haki ya kila Mzanzibari. Sasa leo ikiwa wengine wanatia mifukoni, kutokana na ripoti hii, haya hayatoki mdomoni mwangu mimi. Ripoti hii inasema kwamba wizi umetendeka sana. Kwa hiyo, ikiwa tunawanyima haki wananchi yao ya kuwa na vitu hivi ndani ya *Achieves,* tutakuwa tumefanya dhambi kubwa sana na tukivumilia kwa kweli pia itakuwa dhambi kubwa sana.

Kwa hiyo, mimi ningeiyomba sana Serikali walichukulie hatua hili na si hili tu na jengine lolote ambalo litatokea na likaonesha kwamba kuna dalili ya ubadhilifu wa mali ya umma lichuliwe hatua, tumeshachoka. Kuona wengine wanakuwa kila siku masikini, walimu kila siku kipato chao ni kidogo. Lakini wengine wanaanza kumiliki na wanataka kumiliki maeneo mpaka Zanzibar yote kwa sababu ya uwezo wao wa kifedha. Basi tuhakikishe kwamba wale wanaohusika na haya hatuwa zichukuliwe dhidi yao.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na naipongeza sana, sana, sana kamati pamoja na Mwenyekiti, wao kwa kutuletea ripoti hii ambayo imetufunua masikio na macho na kuona namna ambavyo baadhi ya watu wachache ndani ya taasisi zetu mbali mbali wanavyochukua madaraka yao wenyewe mikoni kwa kujitajirisha wao wenyewe na kujinufaisha wao wenyewe na kusababisha umasikini kwa wananchi wa Zanzibar. Nashukuru Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Nasoro Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia kidogo taarifa hii ya Kamati Teule ya Wizi wa Nyaraka. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kuniwezesha kufika hapa nikiwa na hali ya uzima wa afya na salama.

Mhe. Naibu Spika, wakati nakuja Barazani nimepatwa na majanga baada ya gari yangu kutaka kuungua moto. Lakini mimi nasema kwamba yote ambayo nafanyiwa Mwenyezi Mungu mlinzi yupo na *Inshallah* Mwenyezi Mungu ataniwezesha kufanya kazi zangu za Uwakilishi kwa kipindi hichi na *Inshallah* ataniwezesha tena 2015 mpaka 2020 na nitakuwa ndani ya jengo hili.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, wale ambao wanasema kwamba watanifanyia kila njama, kila husda, kutokana na misimamo yangu, nawambia kwamba Mwenyezi Mungu yupo na yeye ndiye mlinzi wa yote. Nina imani kwamba atatulinda zote Wawakilishi wa CCM na Serikali ya CCM na tutaendelea kutawala nchi hii mpaka milele na milele.

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo niseme kwamba tatizo hili la wizi wa nyaraka ni tatizo kubwa ambalo sote tunapaswa kulilaani na kulikemea na Serikali ichukuwe hatua kwa wale ambao wamehusika. Serikali lazima ichukue mkondo wake, kuhakikisha wale waliohusika ikiwa ni wafanyakazi au huyo Humoud anayetajwa achukuliwe hatua sio kuwabebesha lawama viongozi wetu.

Mhe. Spika, katika kadhia hii ambayo niwapongezi sana wajumbe wanzangu ambao wamechangia kwa namna moja au nyengine katika kulikemea na kulisemea kwa hisia kali kadhia hii. Niwaunge mkono wale waliosema kwamba huyu Humoud achukuliwe hatua za kisheria. Lakini niiyombe Serikali kwamba iwe na tahadhari sana kulichukuliwa kwa tahadhari suala hili ili lisije likavunja uhusiano wetu kati yetu Tanzania na Oman. Lakini Humoud lazima achukuliwe hatua za kisheria.

Mhe. Naibu Spika, kamati hii chini ya Kamanda Jemedari Mkuu Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni, wamefanya kazi nzuri na ni haki yao kupongezwa, kwa sababu wamefichua mengi. Ripoti hii imeeleza mambo mengi na ukiisoma ripoti hii yote basi unaweza ukafika masaa matatu kuieleza ripoti hii. Ukizingatia yeye mwenyewe aliisoma kwa muda wa masaa matatu kasorobo. Kwa hivyo, mambo mengi ambayo yameelezwa mule ni mambo yenye uzito mkubwa sana. Niwajibu wetu sisi kuilazimisha Serikali kwamba ichukue hatua za kisheria kwa wale waliohusika.

Mhe. Naibu Spika, baadhi ya viongozi wetu, viongozi wenzangu katika Baraza hili wamechangia na kutoa lawama baadhi ya viongozi wetu. Lakini mimi nasema mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Mheshimiwa, leo tunakuja kumlaumu Waziri husika Mhe. Haroun Ali Suleiman kama binaadamu na kama kiongozi mwenzangu, kadhia hii inatokea hata Waziri hajakuwa Waziri. Kadhia hii imetokea nimfikirie Mhe. Haroun, matatizo aliyokuwa nayo kuanzia mwezi wa Januari mpaka Mei yupo India kwenye matibabu kutokana na ugonjwa ambao Mwenyezi Mungu ndie aliyempa.

Sasa leo tunakuja hapa tunazungumza hili na lile, kiongozi si kama kiongozi unamlaumu kiongozi mwenzako, humfikirii kule ambako alivyokuwa. Kwa hivyo, mimi nasema kwamba hapa hatumtendei haki maalim Haroun. Maalim Haroun pole sana na Mwenyezi Mungu nawe atakulinda *Inshaallah.*

Mhe. Naibu Spika, ndani ya Baraza hili kumekuwa na kauli ambazo kwa kweli za kusikitisha sana kwa baadhi ya viongozi wetu. Tumekuwa tukichukua mijadala ndani ya Baraza hili kuwatukana viongozi wetu na kushangaa zaidi kuona kwamba lawama hii inaelekea tu kwa Makamu wa Pili wa Rais, lakini hakuna kiongozi mwengine anayelaumiwa. Mambo ambayo anayafanya Makamu wa Pili wa Rais katika nchi hii ni makubwa mno na mimi nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uteuzi wake wa Balozi Seif Ali Idd, amefanya chaguo sahihi, amepata mtendaji sahihi, amepata mtu ambaye mwenye mapenzi ya nchi yake. Jamani hee, tusichukue mambo ya siasa kuwalaumu viongozi wetu na kuwatukana viongozi wetu ndani ya jengo hili tukufu.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu mengi yameshazungumzwa na nina imani kwamba Maalim Haroun ameyachukua na Serikali hasa imeshasikia hata Rais mwenyewe ameshasikia, yale ambayo wajumbe mbali mbali wameyazungumzia na kuyapendekeza katika kuchukuliwa hatua wale ambao wamehusika na kadhia hii. Sasa wengine tunakazia kazia tu tunawatilia nyalio. Maalim Rama ni hodari sana wa methali za Kiswahili nyalio ninajua anazifahamu vizuri sana yeye.

Sasa Mhe. Naibu Spika, mimi niseme kwamba Serikali hii ni sikivu, Serikali hii inaona, Serikali hii inawapenda na inawatakia heri Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla. Kwa hivyo, nina imani kubwa sana kwamba itachukua hatua kwa wale ambao wamehusika na ripoti hii tutaipata ndani ya Baraza letu tukufu na Wazanzibari watapata taarifa hizi za maamuzi ya Serikali.

Baada ya kuyasema hayo Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba naunga mkono kwa asilimia 100 ripoti hii na tunangoja maamuzi ya Serikali. Ninakushukuru sana, ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwanza tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia tena na kutupa uwezo wa kukutana katika Baraza letu hili kujadili mambo yenye hatima ya nchi yetu. Aidha, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi Mhe. Naibu Spika, na pia niishukuru sana Kamati hii Teule kwa kazi nzuri waliyoifanya, yenye umakini pamoja na maoni waliyoyatoa ambayo mimi nayaunga mkono mapendekezo ambayo wameyazungumza Kamati hii katika ripoti hii. Imefanya kazi nzuri na ni wajibu wetu yale yote ya msingi yaliyomo humu kwa mujibu wa taratibu zilizopo za kisheria tuyatekeleze kwa nia ya kuondoa tatizo kama hili la upotevu wa nyaraka au wizi lisitokee tena. Wametoa maoni ambayo ya msingi sana kwa ajili ya kupata ufumbuzi wa tatizo hili.

Pili, Mhe. Naibu Spika, jambo moja nataka niseme sana suala katika maoni yetu ya kuchanganya Serikali ya Oman. Nataka niseme wazi kwamba Serikali ya Oman haihusiki na upoteaji huu wa nyaraka wala haijamtuma mtu yeyote kufanya upoteaji wa nyaraka ama wizi wa nyaraka. Kwa hivyo, ni vyema Waheshimiwa Wajumbe tukaelewa wale waliofanya makosa ni wakosa wao na watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria ili makosa kama haya yasirudie tena.

Mhe. Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara husika, Wizara ya Kazi na Utumishi wa Umma ilianza kulifanyia kazi suala hili na Mhe. Waziri alipoitwa na kamati hii alitoa maelezo ya kina na ufasaha kwa nia ya kuisaidia kamati iweze kutekeleza majukumu yake. Nataka nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa maelezo yake aliyoyatoa katika kamati.

Mhe. Naibu Spika, hapa na mimi niseme kidogo, ukisoma katika ripoti hii utaona kwa maelezo ya ripoti hii ukurasa ule wa 27 ulivyotaja jina langu kana kwamba sielewi wizi huu au upotevu huu wa nyaraka. Nilichokisema Mhe.

Naibu Spika, ilikuwa nilikuwa sina taarifa ya ripoti iliyofanywa kupitia wizara husika na vyombo vile husika vya Polisi na Kitengo chetu cha Kuzuia Rushwa. Ripoti zao zilikuwa hazijafika Ofisini kwetu, ndicho nilichokieleza. Na napenda ninukuu *Hansard* naomba niiseme ili kuweka mambo sawa ili watu waelewe vizuri kwa sababu katika maandishi inaweza kuleta tafsiri nyengine. Wakati nikiitwa na Kamati Teule nilianza kusema kama hivi naomba kunukuu Mhe. Naibu Spika.

"Bismillahi rahmani rahim, kwa sababu leo ni Ijumaa na meneno makubwa umeyasema Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe nionavyo mimi Mhe. Mwenyekiti, kama hii kazi imeshaelezwa vizuri kwa Kiswahili cha siku hizi na wadau husika wenyewe. Maana waziri anayeshughulikia Kazi na Utumishi wa Umma na jambo hili liko Ofisini kwake ameeleza kwa kina. Halkadhalika Kaimu Waziri alilieleza, lakini waziri muhusika mwenyewe ndio amelitolea ufafanuzi na kwa upana wake. Na ijapokuwa Ofisi yetu inasimamia shughuli za Serikali, lakini kwenye jambo *specific* la namna hii Wizara husika ingepaswa kutoa taarifa hizi na kwa sababu wanazo taarifa za kutosha. Na kwa kuwa wao wanapomaliza mchakato mzima ndio wanaziwasilisha Serikalini.

Sasa kwa kuwa zile hatua zilizofanyika bado kuwasilishwa rasmi katika ofisi yetu na kwa vyovyote vile ina maana pengine kuna taratibu nyengine pia walizihitaji wazipate ili waweze kuziwasilisha rasmi. Kwa msingi huo bado mimi nahisi na kwa ushauri wangu hasa na kwa sababu inaonekana kwa maelezo ya Waziri kila kitu kipo tayari. Basi niiombe Kamati iwasiliane na Waziri na kwa bahati nzuri tayari nilishamwambia waziri kwamba Kamati Teule karibuni itakuwa imeanza kazi zake.

Sasa kwa sababu hiyo analijua na kamati inajulikana imetangazwa rasmi na kazi wamezifanya vizuri, si vizuri kwamba sasa azichukue azilete kwetu tuzilete hapa. Ni vizuri moja kwa moja wizara husika ikaeleza kazi walioifanya na ushahidi walioufanya kwa sababu yapo mambo pengine wanahitaji kuwa na vidhibiti vyengine ili walete kwetu kwa *final decision* kwa sababu zikiletwa huku tena ina maana zitapelekwa kwenye *cabinet* kwa msingi izungumzwe na Serikali itoe maelekezo yake.

Kwa hivyo, mimi nafikiri kwenye hili moja kwa moja jambo zuri na sahihi tumuone waziri muhusika na tayari ame-*cooperate* vizuri, ameshaeleza kila kitu hapa ukisoma *Hansard* yapo maelezo ya kutosha ambayo naamini yatasaidia kamati sana. Kilichopo sasa ni kupata zile taarifa alizozifanyia kazi kama wizara kupitia *institutions* nyengine za kiserikali. Nina hakika kutumia vyombo vya Serikali vya ndani katika kupata maelezo ya kina.

Kwa hivyo, mimi Mhe. Mwenyekiti, ningeomba sana kwamba jambo hili apatikane waziri ili alikabidhi na vielelezo vyote visaidie katika kamati hii. Sisi Serikalini hatuna *objection* kumueleza waziri ama nyinyi wenyewe, lakini nikiambiwa mimi saa yoyote nitamwambia Mhe. Waziri. Serikali haina tatizo ya kushirikiana na kamati hii tukufu ili kupata ukweli wa mambo ili muweze kushauri vilivyo ili liweze kufanyiwa kazi kwa uwazi na kwa haki".

Mhe. Naibu Spika, haya ndio msingi wa maelezo yangu na jengine nililolieleza huko mbele limo kwenye *Hansard* hii nilisema kwamba;

|"Ni vizuri sana jambo hili tukalifanyia kazi kwa uangalifu mkubwa sana kwa sababu lina mahusiano pia ya kidiplomasia. Ninaamini kamati imefanya wajibu wake na ninaamini kwa kiasi kikubwa imepata taarifa zile kutokana pia maelezo ya Mhe. Waziri, na kama wenyewe waliona inafaa zaidi kupata taarifa zaidi basi kamati wao ndio kuwa na wajibu wa kuchukua hatua hiyo.

Kwa kuwa bado mpaka hivi sasa taarifa hizi sisi bado hazijawasilishwa rasmi katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na kwa sababu Mhe. Waziri baada ya kuona Kamati yako tukufu Teule inalishughulikia jambo hili ndio maana ninaamini aliamini ripoti aliyokuwa nayo na ripoti ya Kamati Teule itamsaidia zaidi katika kutoa mapendekezo yake ya hatua gani zichukuliwe katika utekelezaji wa kukomesha jambo hili".

Hivyo, kamati hii pamoja na Serikali inazungumza lugha moja, lugha yetu ni kuliondoa tatizo kama hili lisitokee. Jambo la msingi hapa ni kujua nani wahusika ili wachukuliwe hatua, tufanye nini upotevu kama huu au wizi kama huu usitokee tena katika Ofisi zetu muhimu za kumbukumbu, kama alivyosema ni jambo muhimu sana na hatua zipi zichukuliwe za kimsingi kabisa kwa vile vifaa vyetu ama nyaraka nyengine mbali mbali zilizopotea muda mrefu kwa kutumia sheria zetu za ndani na sheria za kimataifa ili tuweze kuzipata wenyewe.

Ninaamini kabisa hii itakuwa ni chanzo cha kuhamasisha cha kuweka mikakati mizuri ya kuhakikisha kwamba kila kilichopotea katika nyumba zetu za kumbukumbu kinarudi Zanzibar. Kwa hivyo, kupitia taratibu zetu za ndani na taratibu za kimataifa, ninaamini sana tutafanya liwezekanalo ili tuhakikishe kwamba yale yote muhimu na nyaraka zetu za kihistoria na vitu vyetu vya thamani vya kihistoria ambavyo vimepotea basi tutachukua kila hatua kuhakikisha kwamba mambo haya yanawezekana na kukamilisha ili nyaraka zetu hizi ziweze kurudi kweli.

Kuhusiana na ushauri uliotolewa kuunda kamati nyengine ya *Tripartite* Mhe. Naibu Spika, jambo hili mimi siliungi mkono hata kidogo. Kwa sababu kazi kubwa imefanywa na Serikali na Kamati Teule, yaliyopo sasa ni ya kuyafanyia kazi haya maoni na mapendekezo yaliyoletwa mbele yetu. Ninaamini kwamba upande wetu Serikalini yale yote yaliyo katika utaratibu wa kisheria yatafanyiwa kazi ili kuhakikisha kwamba mambo kama haya katika nchi yetu yasijirudie tena.

Kuhusu suala la kuondosha hifadhi ya ndugu Humoud huyu ambaye amesemwa sana, Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje haikukataa kwa maelezo yao kuwasiliana na Serikali husika ili *immunity* ya mtu huyu iondoke. Walichosema wao walihitaji ushahidi wa ziada ili waweze kuiandikia Serikali ya Oman imuondolee *immunity* mtu huyu anayeitwa Humuoud. Na kwa sasa kwa maelezo haya yaliyopatikana kupitia Tume Teule na taarifa nyengine ambazo Mhe. Waziri atakuwa nazo muhusika, ninaamini ushahidi wa kutosha wa kuwapelekea wenzetu Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje utapatikana ili waweze kujenga hoja kwa Serikali husika ili hatua zinazopasa ziweze kuchukuliwa kwa mujibu wa sheria ya nchi yetu.

Ninaamini sana kwamba ushahidi huu unatosheleza sana pamoja na kazi iliyofanywa na Jeshi letu la Polisi pamoja na kitengo chetu cha kupambana na rushwa, ripoti ikikamilika yote itafanyiwa kazi vizuri basi tutakuwa na ushahidi wa kutosha wa kupeleka katika Ofisi ya *DPP* na Ofisi ya *DPP* ikaweza kupeleka Mahkamani na wale waliohusika, basi mkono wa sheria ukachukua nafasi yake.

Ninachotaka kusema kwamba si kuchelewa kuchukua hatua, hii nchi inatawaliwa kwa mujibu wa Katiba na Sheria. Kwa hivyo, Serikali haiwezi kutumia mabavu ya kukamata kamata tu, inakamata kwa kufuata taratibu zilizowekwa na sheria pale utaratibu na uchunguzi unapokamilika ndio hatua inachukuliwa kwa mujibu wa sheria. Bado Waheshimiwa Wajumbe tuelewe kwamba nchi yetu inatawaliwa kwa misingi ya utawala bora na sheria za nchi.

Kwa hivyo, hatuwezi kukiuka hayo, lazima hayo mambo yaliyowekwa kisheria yafatwe ili haki ya kila mmoja wetu itendeke. Maana Serikali ina wajibu wa kumtetea kila mmoja na kumpa haki ya kila mmoja lakini kwa wanaofanya makosa vile vile mkondo wa sheria uchukue nafasi yake ili wenye kufanya makosa wahukumiwe kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Naibu Spika, suala niloshauriwa la kuimarisha ulinzi katika ofisi zetu hizi za kumbukumbu ya nyaraka, hili ni jambo zuri, nataka niwahakikishie Waheshimiwa kwamba jambo hili tutafanya kila jitihada kuimarisha ulinzi katika kumbukumbu zetu za nyaraka na kila linaloweza kufanyika la kuimarisha tutafanya hivyo kadiri ya hali halisi ya uwezo wa nchi utakavyoturuhusu ili nyaraka zetu ziwe katika hali nzuri.

Vile vile, lazima tuelewe mara nyingi sana ukitizama ripoti hii inasema nyaraka hii haipo, nyaraka hii haipo. Kuwa haipo hakuna maana moja kwa moja kwamba pia imeibiwa, kuna sababu nyingi. Kwa hivyo, ni vizuri pia tukapata na taarifa zaidi kwenye yale maelezo yanayoonesha haipo, imeibiwa, imepotea au imeharibika, kuna mambo mengi. Kwa hiyo, hapa kumekuwa na changamoto kubwa ya kuhakikisha kwamba tunafuatilia kwa kina zaidi kupata masuala haya yaende vizuri zaidi. Naamini kabisa kwamba polisi wanapoona kosa limefanyika na nimeona ibara yenyewe imewaandikia mara nyingi sana, suala la uhalifu unapofanyika polisi haipaswi kuleta habari yake Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Polisi inapofanya uchunguzi ikaona uchunguzi huo umekamilika wana haki kabisa ya kuchukua ushahidi ule na kuupeleka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka na kesi ikafikishwa Mahakamani.

Mhe. Naibu Spika, si kazi yao polisi kuleta uchunguzi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais inapoona wahalifu wametenda kosa na wakathibitisha ushahidi wao kutokana na uchunguzi wao, basi utaratibu uko *very clear* wa kwenda Mahakamani. Kwa hiyo, siungani mkono hata kidogo na wale waliosema kwamba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na ofisi yake ijiuzulu. Hilo jambo unasema kwa sababu ya furaha yako na ndio nikasema hapa kwamba baadhi ya wenzetu wanachangana mambo ya msingi na siasa. Tunapozungumzia mambo ya msingi ya kutafuta ufumbuzi kwamba tatizo tulilonalo si vyema tukaanza kuchanganya na siasa, ni vizuri sana kuwa makini na maneno yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu nilipigiwa simu na baada ya kupigiwa simu wakaja kuniona wananchi nyumbani wakisikitishwa na kauli hiyo na wakasema ina maana pakitokea makosa siku hizi tuwaombe viongozi wetu wajiuzulu. Wakatoa mfano kwa namna ya uharibu wa mazingira unavyotokea na yanavyochafuliwa, wakaniambia je na sisi tuombe Makamu wa Kwanza wa Rais ajiuzulu kutokana na makosa kama haya. Kwa hivyo, nasema wazi kwamba mambo mengine tunayoyasema humu ndani yanaleta sura za kutokuelewana kwa wananchi huko nje, ni vizuri tunapozungumza mambo ya msingi ya kutafuta ufumbuzi wa tatizo tulizungumze tatizo, tulitatue tatizo na tusitafute mchawi. Na taratibu za sheria ni jambo zuri kuheshimiwa ili tufanye mambo yetu kwa muafaka mzuri.

Mhe. Naibu Spika, mengi yamesemwa na wajumbe hapa, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwa upande wetu wa Serikali yale yote muhimu yaliyoelezwa katika taarifa hii na ambayo yanaendana na taratabu za kisheria, basi Serikali itachukua hatua ili kuona tatizo hili halijirejei na wale waliohusika na tatizo hili wanachukuliwa hatua. Na nyaraka zetu na vifaa vyetu vyengine hata vilivyopotea miaka mingi iliyokwisha kutafuta taratibu za kidiplomasia na Sheria za Kimataifa ili nyaraka zetu hizo kuzipata.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naunga mkono mapendekezo yaliyotolewa na kamati hii. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana na mimi kwa kunipatia nafasi hii kuzungumza machache tu kuhusu Ripoti ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi ya Kuchunguza Upotevu wa Nyaraka kama ilivyowasilisha na Mwenyekiti wa Kamati hii Mhe. Mahamoud Mohammed Mussa.

Mhe. Naibu Spika, na mimi niungane na wenzangu kumshukuru sana Mhe. Mahamoud pamoja na kamati yake, niseme kwa kazi kubwa waliyoifanya kwa kuiweka hadharani haya mambo waliyoyabaini na kwa kweli kamati ile ni nzito, ina Wanasheria Waandamizi na wamefanya kazi kwa kweli kisheria. Nikisema hivyo, namaanisha kwamba wamelitafuta tatizo, wameliona, wamelichambua, sababu zake na mwisho wakatoa mapendekezo. Kwa hiyo, nafikiri ni jambo la msingi sana, siku zote usikosowe tu halafu ukaachia njiani, usitoe na mwelekeo. Lakini nashukuru sana kamati imetowa mwelekeo nini tufanye.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba niseme moja tu kubwa, kamati kwa kweli kwa muono wangu imefanya kazi nzuri ya kuliweka suala hili hadharani. Kwa sababu suala hili ndani ya Serikali yenyewe ilikuwa inalifanyia kazi na tuliwahi kubadilisha na Mhe. Mahamoud mawazo jinsi ya wao waende vipi. Na ukitizama barua iliyo kwenye **Kiambatanisho Nam. 35** cha Mkurugenzi mwenyewe wa Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu Ndg. Hamad H. Omar ya tarehe 6 Oktoba, 2014, kamuandikia Katibu Mkuu yenye kichwa cha habari “Kupotea kwa baadhi ya nyaraka za kale, Kilimani Zanzibar”.

Mhe. Naibu Spika, mwenyewe Mkurugenzi anamripotia Katibu Mkuu na tokea barua ya tarehe 6 Oktoba, 2014 ndio suala hilo lilipofika serikalini. Na Mkurugenzi nimependa sentensi yake moja akasema kwamba; “Kwa vile suala la uhifadhi wa nyaraka linahitaji uamini wa pamoja (*collective loyalty and responsibility*)”. Anaandika Mkurugenzi "...na kwa vile hawa ni washukiwa wakuu..." amewataja watu mbali mbali wale, "...na kwa kuzingatia maadili ya kazi na maelezo waliyotupa basi akashauri mambo ya kufanya." Barua hiyo **Kiambatanisho Nam. 35.**

Mhe. Naibu Spika, kwa hiyo, hii kama nilivyosema nataka kuthibitisha tu kwamba Serikali suala hili imekuwa ikilifanyia kazi muda mrefu na mambo kama haya ya upelelezi wa mambo kama haya yanahitaji utulivu, kufuata taratibu na siri. Haya mambo matatu lazima yaende pamoja, kwa sababu ukikosea *step* moja tu basi *step* nyengine ushaiharibu, hupati ushahidi tena. Sasa kama nilivyosema naishukuru sana kamati kwa kuyaweka pamoja yote haya na leo hii ripoti inasomeka vizuri sana.

Lakini kazi kubwa Mhe. Naibu Spika, lazima tuwapongeze sana kamati ambayo iliundwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar baada ya kuripotiwa tu tatizo hili na kamati humu kwenye ripoti zao wameigusa hii kamati.

Kazi hii tulimpa mwenyewe Kamishna Mkuu wa Polisi Zanzibar, yeye akateua kamati yake iliyoongozwa na Mkuu wa Upelelezi wa *CID* Zanzibar, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Kuhujumu Uchumi pamoja na Usalama wa Taifa. Wao ndio walikaa chini wakatafakari nini wafanye na ndio wakaja na mapendekezo mengi kabisa mpaka wakamjua yule mtuhumu mkubwa ni nani. Mbali wale wa ndani wale Mhe. Haroun, Mhe. Waziri wa Kazi bahati mbaya

kipindi kile ndio kipindi alipata maradhi akaugua na Mwenyezi Mungu kamsaidia kenda kwenye matibabu akarudi. Kwa hiyo, tuliliendeleza sisi, tuliliendeleza mpaka tukafika mahala tukaripotiwa kwamba mtuhumiwa mkubwa ni Humoud, tufanye nini?

Mhe. Naibu Spika, sasa ukimuacha yeye kuwakamata wadogo wadogo hujafanya kazi bado, wale wote ukizunguka na ukiwasikiliza wanamtaja huyu, wote ukisikia wanamtaja huyu. Sasa Serikali ikasema sasa kama ni hivyo, sasa twende kwa kitaratibu na nashukuru kamati ilisema kabisa na waligundua kwamba kweli Mhe. Mahamoud, tulipokuwa tukibadilisha mawazo yeye mwanzo alikuwa na wasi wasi kwamba huyu mtu labda si mtumishi wa ubalozi. Lakini nashukuru kwamba kamati yenyewe ime-*prove beyond reasonable doubt* kwamba kumbe huyu ni mtumishi wa ubalozi.

Sasa wamesema kwenye ukurasa wa 26 kwamba wana taratibu kwa mujibu wa makubaliano ya *Vienna* ukurasa wa 26 juu ya mahusiano kidiplomasia ya mwaka 1961, *Vienna Convention on Diplomatic Relations of 1961* na Sheria ya Kinga na Fursa za Kidiplomasia na Kikonsula Nam. 5 ya 1986. *Diplomatic and Consular Immunity and Privileges Act* Nam. 5 ya 1986.

Mhe. Naibu Spika, ninachotaka kusema Serikali ipo hapa sasa, katika hizo juhudi zetu zote tumesha-*establish* na hawa wakosa wa ndani na mkosa mkubwa. Sasa huyu papa kubwa huyu, huyu muhujumu mkubwa huyu, mtuhumiwa mkubwa ni Humoud, lakini Humoud tumegundua kwamba ana tatizo hili. Sasa kama walivyosema Waheshimiwa kwamba lazima tuende kwa utaratibu, hatuwezi kumkamata Humoud kwa mujibu wa sheria hii, hatuwezi hata kumuhoji Humoud, sisi tunataka tukamuhoji tu pia imeshindikana.

Mhe. Naibu Spika, sasa Serikali nataka kuiripoti kwamba ipo hapa sasa, kama alivyoeleza Mhe. Mohammed kwamba sasa Serikali ipo kwenye hatua hii ya kufuata hizi taratibu za kimataifa, twende vipi.

Mhe. Naibu Spika, tayari Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inashirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje ya Jamhuri ya Muungano na tushasema tuko tayari hata kutuma ujumbe ikibidi twende Muscat tukaonane na wenzetu wa Ufalme wa Oman kuzungumzia suala hili. Kwa sababu kwa kweli hili suala kama walivyosema Waheshimiwa limezungumzwa kwa undani kabisa na kwa uchungu, sote limetugusa. Limetugusa na tunahisi kwa kweli kama rafiki zetu, kwa nini kweli wamtume Balozi, kwa sababu ikiwa anahusika Balozi au Afisa wa Balozi, sisi tunahesabu ndio nchi imehusika, hatuwezi kusema sio Oman aah, ingekuwa mtu wa nje, lakini kama Balozi na bendera anatembeza hapa, basi ndio tuna wasi wasi hapo.

Sasa hatu-*conclude* kwamba kafanya yeye kama katumwa, lakini kama yeye mwanadiplomasia na anajua, kwa sababu ana sheria za kidiplomasia hatujui sisi tu na yeye anajua. Kuna mambo alopaswa afanye, kuna mambo ambayo hapaswi kufanya.

Sasa mimi nimesimama niseme nichukue muda mdogo tu Mhe. Naibu Spika, kueleza hivyo kwamba hii kazi kwa kweli Serikali haikulipuuza, maana yake tumegusiwa hapa kwenye ukurasa wa 26 kwamba kipengele cha (ii) kuwa ushauri wa Jeshi la Polisi ambalo limefanya kazi kubwa ya upelelezi wa suala hili na kutaka Humoud aondolewe kinga ya kibalozi au kufanyiwa kazi inavyostahiki. Hii ni *very strong statement,* nahisi si barabara. Serikali imelifanyia kazi ipasavyo kabisa na kama nilivyosema mambo ya diplomasia lazima uya-*handle* kidiplomasia, ukikosea kwanza shauri lako litaangushwa chini lakini na mwenyewe sasa itakuwa wewe sasa ndio unavunja hiyo diplomasia.

Mhe. Naibu Spika, nilisema niseme machache kuelezea kazi kubwa iliyofanywa na vyombo vyetu na mpaka tulipofika. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Naibu Spika, sauti yangu msione kidogo mawingu ya mvua haya na mambo wenyewe ndio mnayajua.

Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu asubuhi ya leo kuniamsha salama na kuniwezesha kufika hapa kuja kuungana na wenzetu hapa, Waheshimiwa katika suala zima la kadhia hii la nyaraka.

Mhe. Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu tokea jambo hili limeanza kuzungumzwa, limezungumzwa na watu kwa hisia tofauti. Wapo waliozungumza kwa sauti za juu, wako waliozungumza kwa sauti

za kati na wapo waliozungumza kwa hekima na busara zote. Lakini hata hao waliozungumza kwa sauti za juu walizungumza kwa nia hiyo hiyo moja kwamba hili jambo ni zito na jambo hili linahitajia Serikali kulifanyia kazi, sio kulifanyia kazi kwa ule msemo wa kawaida, tunalifanyia kazi halafu tukalilaza. Mimi ni mmoja ambaye nasema kwamba ukisema kuwa nalichungua hili tunakwenda kulikalia kitako, ukilikalia kitako jambo siku zote haliji juu. Kwa hivyo, tunalisimamia na kwenda kulifanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, kwa ruhusa yako niruhusu niwataje wote ambao wamechangia taarifa hii au ripoti hii ya Mhe. Mahamoud katika Kamati Teule. Ni jumla ya Wajumbe 20 waliochangia, hii nikuonesha kwa kiasi gani jambo hili limewagusa wananchi wengi wa Zanzibar:

1. Mhe. Mahamoud Mohammed Mussa — Mwenyekiti wa Kamati
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Hamza Hassan Juma
4. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
5. Mhe. Hija Hassan Hija
6. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
7. Mhe. Mohammed Haji Khalid
8. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
9. Mhe. Omar Ali Shekhe
10. Mhe. Subeit Khamis Faki
11. Mhe. Ali Salum Haji
12. Mhe. Hamad Hassan Omar
13. Mhe. Salim Abdalla Hamad
14. Mhe. Saleh Nassor Juma
15. Mhe. Mgeni Hassan Juma
16. Mhe. Nassor Salum Ali
17. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed
18. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makeme Mwadini na
19. Mhe. Maalim Haroun Ali Suleiman.

Mhe. Naibu Spika, ilikuwa hata nisichukue muda mrefu hapa niseme tu kwamba nimekubali maelezo na mapendekezo ya kamati na kwamba nayachukua na kwenda kuyafanyia kazi. Lakini na mimi sitowatendea haki wananchi wa Zanzibar kama na mimi sitotoa ufafanuzi wa hapa na pale. Katika *principles* za kihesabu mimi ni Mwalimu wa Hesabu na bahati nzuri wengi wa Wajumbe wa Kamati hii ni wanafunzi wangu, wengi wao, naamini *I feel proud of them* kwamba wamekwenda mpaka wakafika hatua wakamwita Mwalimu wao wakaanza kumuhoji. Mimi sikusema nimehojiwa ila nimeulizwa ili kwa kusaidia vijana wangu hawa, wakati nikiwa waziri wengine walikuwa walimu, nikiwa Mwalimu wengine ni wanafunzi wangu, Mahamoud ni mmoja wapo, ndio maana yake huwa namwita kwa jina tu hata simwiti Mheshimiwa kwa sababu ndio cheo cha uwalimu, wengine nimesomesha nao pamoja, wengine nilikuwa waziri wao katika Wizara ya Elimu.

Mhe. Naibu Spika, la msingi ni nini hapa? Jambo limetendeka, tukubali ni jambo baya sana limetendeka hili, lakini niruhusuni Mhe. Naibu Spika, nieleze kadhia hii ilivyotokezea nilikuwa wapi na niliyapataje mimi.

Mhe. Naibu Spika, mawasiliano ya simu yote ya Humoud na wafanyakazi hawa mimi nasema hawa walioshiriki katika wizi yalifanyika kuanzia Februari mpaka karibu ya Novemba, 2013; wakati ule mimi nilikuwa ni Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Baadae katika mwezi wa Novemba nikapata uteuzi wa Waziri wa Kazi na Utumishi wa Umma kwa *nature* ya nyaraka inabidi Rais mwenyewe akaamua, si lazima lakini aliamua ailete kwenye utumishi.

Tarehe 4 Januari mimi nikaanza kupata mitihani kidogo kidogo, Mhe. Makamu wa Pili tulikuwa pamoja pale Kariakoo kwenye uwekaji wa jiwe la msingi atakumbuka. Siku ile mimi ndio nilianza kuhisi maumivu, nikamuomba askari wa usalama Ndugu Adam yupo hapo nje, nikamwambia kwani lazima Makamu nimuonyeshe kila mahali kwa sababu mimi nishachoka kutokana na ile hali inavyojitokeza, nahisi kwamba siwezikumaliza ile duru. Akanambia sikiliza waziri hawa watu wana shughuli yao waachie wamalize. Basi mimi nikatafuta mahali nikapumzika kidogo.

Pia, siku ile nilipangiwa kazi siku ya pili niende Pemba nikaweke jiwe la msingi kwa skuli ya Mkanyageni. Mwenyezi Mungu kanipa nguvu nikaenda Mkanyageni na nikaweka jiwe la msingi. Niliporudi tarehe 6 nikenda kwenye maonesho Maisara kwa Mhe. Mazrui na niliporudi nyumbani hali ikaanza kubadilika zaidi. Sasa nikamwita mwenye nyumba na sote ndio washauri wetu hao wala tusiwadharau ni watu muhimu sana. Pili, nikamwambia kidogo *I'm not feel well,* akanambia ngoja nizungumze na daktari, akapiga simu kwa daktari, hiyo hadithi ni refu ieleweke, hatimaye saa kumi jioni nikashitukia niko Muhimbili. Hiyo ilikuwa ni tarehe 10 Januari. Sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar hapa mimi nimelazwa niko Muhimbili.

Mhe. Naibu Spika, walikuja viongozi wengi kunitizama Makamu wa Pili wa Rais, Makamu wa Kwanza wa Rais, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na viongozi wengi *Alhamdulillah,* pamoja na Waheshimiwa Wawakilishi wengi nawashukuru wale waliopata nafasi ya kuja kunitizama walikuja, nilipokuwa Muhimbili na Afrika ya Kusini, wale waliokuwa hawakubahatika pia nimewasamehe. Mengine nitazungumza baadae.

Mhe. Naibu Spika, tarehe 24 Januari nikafanyiwa upasuaji mkubwa huko Afrika ya Kusini, hapa pana kikao cha Baraza kinaendelea na ndipo yakapika maamuzi kwamba iundwe hii tume ambayo Mhe. Mahmoud Mohammed akawa Mwenyekiti, sijui chochote, *what is happening I do not*. Basi mimi narudi mwezi wa Aprili wanakuja jamaa, tizameni natoka kwenye maradhi ya moyo, wanakuja watu wananambia unajua yaliyotokea wizarani kwako? Nikawaambia sijui, wakasema nyaraka zimeibiwa huko za thamani kubwa. Nikasema Mungu wangu wee, natoka kwenye maradhi narejeshewa maradhi, maana yake hili liliniuma sana.

Mimi nakwambieni mwana taaluma yoyote na hizi *documents* umuhimu wake lazima ajue kwamba hili jambo ni zito na lina athari kubwa, kama kuna mtu ambaye ameathirika sana na zimemuuziza sana *documents* hizi kuibiwa ni Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Tusichukulie kwamba hili jambo ni *simple,* sio *simple* kiasi hicho. Mimi nikakaa nyumbani nikaletewa *draft* ya waraka unapelekwa Baraza la Mapinduzi kwamba kuna waraka huu lakini hali yangu ndio kama hii, nikaambiwa kaimu waziri ataisoma taarifa yako. Nashukuru, ikasomwa na yakapitishwa maamuzi yaliyopitishwa, namshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora katoa maelezo marefu juu ya Serikali hatua iliyochukua juu ya jambo hili.

Miezi miwili mimi nikaanza kujizozoa kidogo na daktari wangu alinambia usikae nyumbani tu nenda nenda ofisini, jishughulishe shughulishe kwa sababu kuna mambo kwenye mikono humu nimetolewa lakini nimeshapoa msiwe na wasi wasi na wananchi wangu Jimbo la Makunduchi wasiwe na wasi wasi *Inshaallah* mambo yatakuwa mazuri tu.

Kwa hivyo, nikakaa ofisini linaniumiza sana hili pamoja na matatizo yangu, nikasema nifanye juhudi. Nilimpigia simu Naibu Balozi wa Oman anaitwa Bwana Khalid na bahati nzuri *Hansard* hii ambayo kwa bahati mbaya kwenye ripoti ya Mwenyekiti hii *statement* haikujitokeza. Mhe. Naibu Spika, naomba niisome kwa ruhusa yako inasema hivi;

"**Mwenyekiti:** Sasa hivi tukuulize mwenzetu wewe ulitumia utaratibu gani kumwita huyu na kuweza kumhoji na ukapata yale ambayo ulitwambia?

Waziri: Mimi nimemwita Balozi na nina mamlaka ya kumwita balozi wakati wowote, nilimwambia utapokuja uje na raia wako wa Oman". Nilipomwambia hivyo wakati huo wala simjui kwamba ni mfanyakazi wa wapi au anafanya kazi wapi, sijui.

"Nilivyosikia anaitwa Humoud, aliko sikujui, wewe unamjua. Akasema *"I know this guy. he is working as advisor at Beit-El-Ajaib, I shall bring today"*.

Mhe. Naibu Spika, akamleta *immediately,* tunayo haki sisi Waheshimiwa ya kufanya hivyo. *Statement* hii kwenye *Hansard* au kwenye ripoti *unless* niwe nimetizama kwa haraka haikuandikwa na nikasisitiza kwamba kauli hii sikuitoa mimi, naibu balozi ndiye aliyesema kwamba huyu si mfanyakazi. Inawezekana ameshakuja mara moja tokea mwaka 2005 akawa mfanyakazi wa pale ubalozini na bado ana heshima, yaani mabalozi wakishafanya kazi ya ubalozi wanakuwa wanabakia mabalozi tu, ataitwa jina la balozi tu. Mimi maalim hata nikiwa waziri au nani bado jina langu la ualimu litabakia tu.

Sasa huyu inawezekana alikuwa na *immunity* kwa sababu pale alikuwa anafanya kazi miaka ya nyuma na alifanya kazi si miaka miwili au mitati, ni miaka mingi amefanya kazi pale, keshakwenda na kesharudi, kama anafanya

biashara hiyo ilikuwa haijulikani. Sasa aliponambia vile nikamuuliza maswali yangu na kama nilivyosema kwenye *Hansard* alikataa katakata akasema *I'm not involved,* sikuhisika kabisa.

Mimi nikamwambia kuwa nina ushahidi kwamba wewe umehusika, simu zilizopigwa za Februari 13 mpaka karibu ya Agosti, Septemba 13 ni simu yako wewe au simu ya nani? Akasema *It is mine*, *my number*. Ulikuwa una-*communicate* kitu gani na hawa vijana wetu wafanyakazi hawa? Hana jawabu. Sasa mimi sikujua kwamba ana *immunity* au hana kwa wakati ule, kwa sababu hizo ripoti za Serikali wakati ule ilikuwa mimi sijazipata kwa vile sijaripoti kwenye Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, zaidi ya hivyo mimi nikachukua juhudi zaidi baada ya balozi huyo na huyu kijana nikamwita mkurugenzi nikamwambia hebu muandikie barua Mkuu wa Polisi tujue hatua iliyofikia, ndio ile barua ambayo Mhe. Waziri kaisoma. Ikaandikwa barua ile tukapata taarifa ili na mimi nijue wapi yamefika nilikuwa sipo jamani. Lakini kwa mujibu wa *principle* za *management* hata kama kitu hukuwepo madhali wewe ndiye dhamana, basi huwezi kutoka umo tu. Jukumu hili ni letu sote serikalini; si la Maalim Haroun, si la nani, ni letu sote, tukubali kosa limetendeka, turekebishe makosa yasitendeke. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sasa narudi pale kwenye *mathematic* kwamba wanasem;*, "to understand a question is part of your answer*, pengine kujua jawabu. Ukishafahamu lile tatizo, to *understand the problem* basi ni sehemu ya jawabu yako. Tatizo tumeliona, Wazungu wanasema; *no objection, no doubt*.

Hata kule Afrika ya Kusini nilipofika daktari wangu namsikia anamwambia mtu "*No doubt he has a heart attack"*, daktari anaiambia familia yangu pale alikuwepo mmoja kati ya watu wa familia yangu kwamba; "*there is no doubt he has a heart attack"*. Mimi nilikuwa nasikia tu mambo ya maradhi ya moyo haya, basi baadae wakanichana walivyotaka, halafu akanirejeshea mambo yangu mengine humu ndani kama yamo yote sijui, *Alhamdulillah* Mwenyezi Mungu anajua.

Mhe. Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa hatua niliyofikia leo kwamba nimesimama hapa mbele yenu. Sasa nitajitahidi kwa ufupi kabisa kutoa jawabu ya mambo fulani fulani. Shukurani maalum kwa kamati, wametusaidia sana, tunakiri kamati imetusaidia sana; imeisaidia Serikali na wameisaidia wizara, hili halina mushkeli wowote. Nawashukuru Waheshimiwa wote waliochangia kwa njia mbali mbali hata wale waliosema tujiuzulu, Waheshimiwa watatu walijitokeza wazi wazi wao wakasema kwamba tujiuzulu nao pia nawashukuru walisema hivyo sio kwamba wanatuchukia, ni kwa kuona hili jambo ni zito kwa sababu "anayekamatwa na ngozi huyo huyo ndio mwinzi" hata kama hukuhusika.

Mhe. Naibu Spika, nataka nihakikishe kwamba baada ya tukio hili kutokea kwa kipindi hiki mpaka sasa hivi tulipofika tumechukua hatua kwa mambo kadhaa. Hizo *CCTV camera* tayari zimeshawekwa, wafanyakazi pale hawawezi kupelekwa tu kama hawajafanyiwa *vetting* na wengine wamefanyiwa *vetting* wakionekana wanafaa wanachukuliwa wengine waliokuwa hawafai hawachukuliwi, nyaraka zile kongwe zilikuwa zimewekwa zinatengenezwa vizuri sasa hivi, yote hayo kutokana na kazi ya kamati.

Kuna *label* maalum imewekwa kwa ajili ya kufanya shughuli hizi za kukarabati au kuzitengeneza hizi *documents*. Motisha kwa wafanyakazi wetu ili waweze kufanya kazi kwa moyo mzuri tumeanza kuwapa *Alhamdulillah* na kuanzia mwaka mpya wa fedha tutaendelea. Kazi ya *digitalization* inaendelea vizuri, tumenunua vifaa karibu shilingi 55 milioni pale, sera inakamilishwa sasa hivi, ukaguzi maofisini unaendelea kukagua *documents* zile.

Suala moja kuhusu bodi, nilisema kwamba bodi haikuwahi kunishauri. Mimi tokea nimechaguliwa kuwa waziri, kwanza bodi hii haikuwa kwenye mamlaka yangu, nilipokuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali mimi ndipo nilipoteuwa bodi hii. Kwa bahati mbaya ilikuwa mwisho wa mwaka wa 2010 baadae yakatokea mabadiliko na hii nyaraka ikawa haikuendelea kuwa katika Wizara yetu ya Elimu na mimi nikapelekwa Wizara ya Uwezeshaji.

Bodi hii Mwenyekiti wake ni Mhe. Ali Mzee Ali na *Alhamdulillah* yupo pale, lakini hata siku moja suala hili, nasema tena hata siku moja kwa sababu bodi yenyewe ilikuwa haikutani kutokana na matatizo fulani na watanishauri nini na mimi siko, sio waziri wao tena. Baadae bodi hii iliporejeshwa utumishi na ilikuwa muda wake ushamalizika mimi ndio nikachagua bodi nyengine au Rais akateuwa Mwenyekiti na baadae tukachagua wajumbe, sasa hivi bodi mpya ishachaguliwa.

Inawezekana kwamba bodi hii ilikuwa na matatizo fulani huko idarani kwao na mkurugenzi, *I don't know,* siwezi kusema hayo. Lakini ninachosema kwamba bodi ilikuwa katika miezi sita inakutana mara moja, sasa hivi bodi iko tayari na inaendelea na shughuli zake tumeizindua. Mimi nimeshaizindua na *Alhamdulillah I hope* kwamba itaendelea kufanya kazi vizuri kama bodi iliyopita.

Mhe. Naibu Spika, lakini la msingi ni nini hapa? Kwanza kuna suala la kontena, kontena lile sio letu la nyaraka limehifadhiwa tu pale, mule muna ma-*files* ya ma-*documents* mengi ya Mahakama Kuu, wamekuja kuhifadhi pale kwa sababu hawana nafasi. Kwa sababu kuna watu wamesema kwamba lile kontena lipo limetiwa *documents* za miaka mingi zinaharibika pale, sio kontena letu lile.

Mhe. Omar Ali Shehe, alisema suala moja hili naomba niliseme, kwa nini kila anapokwenda Maalim Haroun hii nyaraka inakwenda kwake yeye? Jamani mteuzi ni Rais, imetokezea imesadifu hivyo ni kweli. Mimi nilipokuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali mwaka 2000/2010 nyaraka ilikuwa chini ya Wizara ya Elimu, baadae mwaka 2010 Novemba ikapelekwa Wizara ya Utawala Bora na Utumishi wa Umma.

Mimi sikuwepo pale na kabla ya hapo nyaraka hizi zilikuwa chini ya Ofisi ya Rais Ikulu tokea mwaka 1988-2000, mimi sikuwepo pale hata kabla kuwa waziri na masuala ya nyaraka haya ni mambo ya historia na mambo ya taaluma. Kwa hivyo, Rais aliyekuwepo wakati ule 2000-2010 akaamua kuniweka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, sio kwamba nimekwenda kuiomba na wala sina *interest* yoyote kwenye nyaraka mimi, *interest* yangu ni ya kitaaluma tu. Watu wanakwenda wakichukua *PhD* pale pale, maana yake zile *documents* zilipochukuliwa zikaniuma sana. *I have nothing to do,* nina *interest* ya nyaraka pale zaidi ya kitaaluma tu basi.

Waheshimiwa Wajumbe, haya nitayoyazungumza yote yanaweza yakasaidia au yasisaidie, la msingi ni nini? La msingi ni kwamba kosa limetendeka tuelewe kwamba hilo kosa limetendeka kweli na bado juhudi za Serikali zinaendelea, kinachotakiwa sasa hivi na Serikali ikafanye juhudi maalum na tutafanya hivyo.

Kwanza Waheshimiwa wamependekeza kuwa popote pale alipo Humoud zifanywe taratibu za kumleta ili asaidie kutupatia ushahidi zaidi, kwa sababu tunajua kwamba Humoud ni mkosa mkubwa wa suala hili, halina *objection* hilo. Lakini na hawa wafanyakazi wetu wawili Mwanahawa na Mwanakombo wamepewa *implicated* katika kosa hili, nao wameshachukuliwa hatua wamesimamishwa kazi na wala hatutofanya kosa la kuwarejesha kwa mujibu wa utaratibu wa Sheria za Utumishi wa Umma tukawapangia kazi nyengine. Wale wote waliohusika waliotajwa kwenye ripoti hii kwa njia moja au nyengine lazima tutachukua hatua. Mimi sitokubali kabisa.

Mhe. Naibu Spika, naahidi kabisa kwamba wale wote ambao wameingizwa katika sakata hili hatutowaacha kabisa. Sitokubali kwamba makosa haya yanatendeka kama mimi ni dhamana wa hiyo *archive* kwa sasa hivi na nipo na niache mambo haya yaende yanavyokwenda tu, sitokubali kabisa Mheshimiwa hili nalisisitiza, nitaishauri Serikali ipasavyo na vyombo vinavyohusika ili tuchukue hatua za kufaa.

Nadhani nisizungumze mengi inatosha, zaidi ya kuwashukuru sana Wajumbe jambo hili limetuuma sote na hasa wale wanaosema kwamba pesa za wavuja jasho na uchungu wa nchi hii. Mimi nasema kwa uchungu wa nchi hii tunao na kama kuna mtu ambaye ana uchungu wa nchi hii wa mwanzo kabisa atakuwa Rais wetu, Makamu wa Kwanza, Makamu wa Pili, Mawaziri na viongozi wote pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa humu ndani. Sote tuna uchungu wa nchi hii, tumezaliwa hapa, tumesoma hapa, tumeendelezwa hapa kimaendeleo.

Mhe. Naibu Spika, sasa tushirikiane katika jambo hili. Nasema tena Mheshimiwa jambo hili ni zito sana, limetuuma sote tujitahidini.

Mhe. Naibu Spika, naomba nikushukuru tena, niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe, waniruhusu kwa kuniachia sasa hivi, sio nikakae kitako, kwani kukaa kitako ndio hayendi haya, tukishamaliza shughuli hii, tuendeleze kufanya kazi, kazi imeshaanza, tutachukuwa hatua moja baada ya nyengine ili kuhakikisha kwamba mabaya ya pale yote tunayaweka sawa. *Inshaallah*.

Baada ya hayo machache nashukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Waziri tunakushukuru, mawaziri tayari wamekwisha kutoa hoja zao kujibu baadhi ya sehemu, sasa tumwite Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Kuchunguza Upotevu wa Nyaraka, Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa ili aweze kufanya majumuisho.

Mhe. Mwenyekiti wa Ripoti ya Kamati Teule ya Kuchunguza Upotevu wa Nyaraka: Mhe. Naibu Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba Mbingu na ardhi kwa kutuwezesha sisi waja wake leo kwa mara nyengine tena tukaweza kukutana hapa katika taratibu zetu ambazo tumejiwekea na kukamilisha yale ambayo huwa tunajipangia kama vile ambavyo kila dua zetu asubuhi huwa tunazisoma hapa na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atuwezeshe tumalize kazi zetu hizi kwa vizuri kwa salama na amani.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nichukuwe fursa hii kuwashukuru wote ambao wamechangia kwa namna moja au nyengine na hatimae tukaweza kufikia hapa kufanya majumuisho ya michango mbali mbali pamoja na maoni na masuala na hoja ambazo zimekuwa ziwewashilishwa hapa na Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, niwashukuru Mawaziri kwa niaba ya Serikali kwa namna ambavyo wamejaribu kwa namna moja au nyengine kujibu baadhi ya mambo ambayo yana lengo la kuweza kuweka sawa hawa mambo ambayo yaliyokuwa yamejitokeza katika ripoti hii ambayo iliwasilishwa toka siku ile ambayo tulianza nayo.

Mhe. Naibu Spika, lakini mwisho na kwa aina yake nikushukuru wewe sasa Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa ya kuweza kusimama hapa kwa mara nyengine ili niweze kuzungumza machahe na hatimae kuwaomba Wajumbe wakubali kuipokea ripoti hii na baadae Serikali iweze kuendelea kuifanyia kazi pale ambapo ilikuwa imefiki, kamati ikaongoezea sasa tunairejesha tena kwenye Serikali kwa ajili ya kumalizia.

Mhe. Naibu Spika, mimi hapa nimekuja na mambo mengi sana kwanza nimekuja na ripoti yenywe, halafu nimekuja na baadhi ya *Hansard* ambazo zinahusu mahojiano na baadhi ya Wajumbe. Sina lengo la kuweza kurudi tena kuzisoka nyaraka hizi kwa mara nyengine tena.

Isipokuwa nishukuru sana Serikali kwa kukubali juu ya kazi ambayo imefanywa na kamati hii na kwamba tayari Serikali inakuwa kuweza kuifanyia kazi yale ambayo yameonekana ndani ya kamati hii, hiyo mashukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, akimaliza Mwenyekiti tunataka tuipitishe hii, sasa naona mnatoka kwa makundi. Naomba Waheshimiwa wanaotoka warudi ili tuweze kumaliza kazi yetu.

Mhe. Mwenyekiti wa Ripoti ya Kamati Teule ya Kuchunguza Upotevu wa Nyaraka: Niwashukuru sana Wajumbe wa Baraza letu hili tukufu la Wawakilishi wa Zazibar kwa michango yao mbali mbali ambayo wameitoka na hatimae ikaweza kuisababisha ripoti hii iwe nzuri zaidi.

Ninachoweza kuwaambiwa Wajumbe hawa ambao wamechangia kwa namna mmoja au nyengine kwamba pamoja na maelezo ya kamati ambayo tumeiwasilisha hapa vile vile kama Mwenyekiti wa kamati, nakubaliana na maoni pamoja na michango ya Wajumbe ambayo imewasilishwa hapa isipokuwa mmoja tu, huu nina mashaka nao.

Mhe. Spika, sikubaliani na suala zima la kumtaka Makamu wa Pili wa Rais ajiuzulu kuhusiana na suala hili. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nikimalizia hapo naomba sasa niwatambue Wajumbe ambao walikuwa wamechangia katika ripoti hii, wa kwanza kabisa kama ilivyo kawaida Mwanasheria mkubwa nae ni:-

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
Mhe. Hamza Hassan Juma
Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
Mhe. Hija Hassan Hija
Mhe. Mohammed Haji Khalid

Mhe. Wanu hafidh Ameir
Mhe. Abdalla Juma Abdallah
Mhe. Omar Ali Shehe
Mhe. Abdallah Mohammed Ali - ambaye ni mtaalamu wetu huyu
Mhe. Rufai Said Rufai
Mhe. Ali Salum Haji
Mhe. Hassan Hamad Omar
Mhe. Salim Abdallah Hamad
Mhe. Saleh Nassoro Juma
Mhe. Amina Idd Mabourk
Mhe. Mgeni Hassan Juma
Mhe. Nassor Salim Ali
Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais
Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Ikulu na Utwawa Bora
Mhe. Maalim wangu Maalim Haroun Ali Suleiman

Mhe. Naibu Spika, nakiri kwamba Mwalimu Haroun ni Mwalimu wangu katika Skuli ya Haile Selassie na vile vile ni mtu muhimu sana katika maisha yangu kwa sababu nilipopata mitihani wakati ule wa mitihani wa darasa la kumi na mbili Maalim Haroun ni miongoni watu ambao walisimama kidete kuhakikisha kwamba naendelea tena na masomo yangu akishirikiana na ndugu yake Marehemu Maalim Haji Ali Suleiman Mungu amrehemu na Maalim Abdallah Mzee Mpangile kwa sababu nilitokea Skuli ya Utaani Pemba.

Baada ya maelezo hayo sasa Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa ufafanuzi kwa ambayo yaliyozungumzwa.

Kwanza kabisa napenda kuchukuwa fursa hii kumshukuru *Allah Subhanahu wa ta'ala* kwa ukarimu wake na kutujaalia afya na uzima tukaweza kuendelea na shughuli zetu hapa. Lakini pia nakushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa kwa mara nyengine tena kusimama mbele ya Baraza hili ili kufanya majumuisho ya michango mbali mbali iliyotolewa na Wajumbe walichangia hoja ya Kamati Teule na kuchunguza upotevu wa nyaraka za Serikali.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijaaza kutoa ufafanuzi wa hoja mbali mbali kwanza naomba niwashukuru Wajumbe wote waliochangia katika hoja na kwa ruhusa yako vile vile naomba Wajumbe hawa wajisikie kwamba waliyoyafanya ni mambo ambayo kamati imeyazingatia.(*Makofi*)

Baada ya hapo Mhe. Naibu Spika, naomba nianze na suala zima la ulinzi wa jumba la nyaraka. Hoja hii imeoneka kuchangiwa na Wajumbe walio wengi na kwa sababu ya umuhimu wake, mimi naomba niungane na Wajumbe wa Baraza hili tukufu kwa kuwa ni hoja muhimu sana na lile eneo linahitaji ulinzi wa uhakika ili nyaraka ziliopo ziendelee kuhifadhika ili zisije kuendelea kupotea kama ambavyo nyengine zimekwisha kupotea na baadhi yetu ya vitu mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, nielekee katika suala zima la kuundwa kwa Kamati ya Uchunguzi. Baadhi ya Wajumbe waunga mkono mapendekezo yaliyotolewa na kamati kwamba kuna haja ya msingi ya kuundwa kwa kamati itakayokuwa na muda wa kutosha kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa nyaraka zote zilizokuwepo katika jumba la nyaraka. Suala hili lina umuhimu wa pekee kwa kuwa taarifa iliyotolewa na kamati hii ni robo tu ya uhalisia uliopo katika jumba la nyaraka.

Ni imani yangu kwamba kamati hii ambayo itaundwa baadae au Serikali itakapochukuwa jukumu la kuendeleza zaidi itafanyakazi na kuweza kupata taarifa nyingi zaidi za kuweza kuwezeshwa na kupanga upya kwa nyaraka hizo katika jumba lile kwa sababu itajukulikana ni nyaraka ipo ipo na ipi haipo.

Mhe. Naibu Spika, Wajumbe wengi vile vile walichangia hoja ya Kamati Teule na kuonesha hisia zao kuwa bila ya shaka kuwahusisha viongozi waliopewa dhamana ya kusimamia taasisi hii ilikuwa ina faraja zake. Katika kamati hii

haitaweza kukataa au kukubali moja kwa moja hoja hii kwa sababu kwa mujibu wa sheria za nchi hii huwezi kumtia mtu katika makosa ya aina yoyote basi na kufata taratibu tulizojiwekea za kisheria.

Hivyo, basi naiomba Serikali ili kukudhi matakwa ya sheria, kamati inataka Serikali kuhakikisha kwamba bwana Humoud anakamatwa na vyombo vya sheria ili aweze kuhojiwa kwa kufanya hivyo, kutakuwa na uwezekano wa kuleta ushahidi wa kutosha na kuweza kuwapata wahusika wa kadhia hii waweze kuchukuliwa hatua zinazofaa.

Hata hivyo, kamati inakubaliana na Wajumbe waliochangia kwamba viongozi wa taasisi hii wahusika katika kupelekea kutendeka kwa tukio hili, kutokana na ukweli kwamba wameshindwa kusimamia dhamana waliyopewa na Serikali hivyo hatua zinazostahiki kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma zichukuwe hatua zake.

Vile vile, naomba kwenda katika eneo la nne kuhusu uwepo wa baadhi ya nyaraka katika jumba la nyaraka Kilimani. Katika michango ya baadhi ya Wajumbe waliotaka kujua uwepo wa nyaraka kwa mfano Nyaraka za Tiptip na nyaraka nyenginezo zinazohusiana na masuala ya eka tatu, tatu na kadhalika.

Mhe. Naibu Spika, naomba niseme kwamba kamati baada ya kupewa kazi ya uchunguzi wa nyaraka ilikusudia kufanya ukaguzi wa nyaraka zote zilizokuwepo katika jumba hilo ili kuweza kujua kila nyaraka iliyokuwepo na ipi iliyokuwa haipo. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa muda haikuweza kufanya kazi kwa mujibu wa kwamba kama kamati ilivyotaka.

Kwa hivyo, lakini kwa kumbukumbu zangu mwenyewe binafi kama Mwenyekiti wa Kamati hii nakumbuka kwamba kuna *files* ambazo zinahusu masuala la Tiptip katika Idara ya Nyaraka ambazo niliziona. Nyaraka hizo Wajumbe wameulizia zinaingika katika *group* la *Land House,* nyaraka hizi ni nyingi sana na kwa idadi yake tunakisia kuwa ni nyaraka 1059. Hata hivyo, kamati pia ilipata muda wa kuangalia nyaraka 54 tu kati ya hizo na zinaonekana katika **Kiambatanisho Nam. KTN 14.** Hivyo basi, haikuwa rahisi kujua kila kilichopo, isipokuwa kamati katika hii imeweza kusisitiza kwamba na inaendelea kusisitiza kufanyika kwa uchunguzi wa kina katika jumba la nyaraka ili kuweza kufahamu nyaraka zilizopotea na mali nyengine na zilizokuwepo vile vile.

Kuchukuliwa kwa hatua kwa wahusika na kurejeshwa kwa nyaraka zilizopotea. Kamati inaunga mkono hoja ya Wajumbe waliochangia kwamba wahusika wote wachukuliwe hatua ambao wanahusika na kadhia hii ili sheria ichukuliwe na iwe fundisho kwa wengine.

Vile vile, kuhusu suala la kurejeshwa kwa nyaraka zote zilizoibiwa, hili ni jambo muhimu sana na ni lazima tufike pahala nyaraka zote zilizoibiwa zinarejeshwe Zanzibar kama ambavyo wenzetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walivyoweza kurejeshewa kinyago ambacho kilichukuliwa na hatimae kikarejeshwa katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hata hivyo, Serikali inatakiwa kuchukuwa hatua za zaida kwa sababu kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na Shirika la Kimataifa ya *UNESCO* inatoa utaratibu mzima ya kufuatwa pindi nchi inapopatwa na majangwa ya namna hii. Maelezo ziadi ya utaratibu huo yanaoneka katika **Kiambatanisho Nam. KTN 35,** ukurasa wa 128 hadi 129 wa ripoti ambayo tumeiwasilisha kwenu.

Mhe. Naibu Spika, Thamani ya nyaraka zilizoibiwa, hoja hii iliibuliwa na Mhe. Hija Hassan Hija wakati alipokuwa akichangia na kutaka kujua thamani halisi ya nyaraka zilizoibiwa ili iwe rahisi kujua nchi imeinga hasara kiasi gani. Ni kweli kwamba suala hili lina umuhimu wake hasa ikizingatiwa kwamba nyaraka zina thamani kubwa. Lakini kwa kuwa kamati haikupata fursa ya kukutana na wataalamu kutoka nchi mbali mbali isingekuwa rahisi kuweza kupata uzoefu na kujua utaalamu utakaotumika ili kuzitathmini nyaraka hizo. Kazi hii tutaendelea kuicha katika Serikali kwa ile timu ambayo itakuja kuundwa na hatimae kuja kuletewa ripoti yake kama ambavyo kamati imefanya.

Mhe. Naibu Spika, hata hivyo, ule upekee wa nyaraka hizi kwamba zinapatikana katika nchi hii duniani kote inatosha kuwawezesha kujua kwamba hizi nyaraka zina thamani kubwa sana, ule uwezo wa Zanzibar kujisifia duniani kote kwamba nyaraka hii ipo kwetu tu basi inatosha kuthibitisha kwamba ni utajiri mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, Uhusiano wa Zanzibar na Oman katika kadhia hii. Waheshimiwa Wajumbe kwa mara nyengine tena kama baadhi ya Wajumbe walivyochangia kwa mfano Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe. Hija Hassan Hija na kadhalika, wamezungumzia suala hili katika namna tafauti. Baadhi walitaka mazungmzo ya nchi na nchi yafanyike, wengine wakitaka Serikali ya Oman itoe tamko na wengine wamezungumza kama ambavyo walivyozungumza.

Waheshimiwa Wajumbe, naomba niseme tena kwa mara nyengine kamati katika hili ilikuwa ilifanya kazi ya uangalifu wa hali ya juu kabisa na kujua kwamba linaweza kupelekewa mgogoro wa kidiplomasia. Hata hivyo, ili kuhakikisha kwamba suala hili haliachwi kama lilivyo kamati inaamini kwamba kitendo alichokifanya ndugu Humoud hakina uhusiano na nchi yake ila ni utashi wake yeye mwenyewe.

Hivyo basi, wajibu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuitaka Serikali ya Oman kuwezesha kumpata Humoud na kwamba Oman haihusiki na kadhia hii, tunaamini itatoa ushirikiano wa hali ya juu kabisa.

Mhe. Naibu Spika, Nyaraka za Kijerumani, hoja hii ilitajwa na Mhe. Rufai Said Rufai ikieleza kwamba nyaraka hizi zote hazipo, lakini ki ukweli kilichotokea ni kwamba nyaraka hizi ziliomba na Wajerumani kwa lengo la kweda kuzifanyia ukarabati lakini baadae zilirejeshwa, isipokuwa wakati wa kurejeshwa hazikukaguliwa kujua kwamba je, ni nyaraka halisi au ni *copies* za nyaraka zilizochukuliwa. Hivyo, ndivyo kamati ilivyokuwa imezungumza na sivyo kama vile ambavyo Mhe. Rufai Said Rufai alivyokuwa amefahamu.

Mhe. Naibu Spika, Wahusika wa wizi wa nyaraka. Katika kufafanua hoja ni kwamba wahusika waliohusishwa na kadhia moja kwa moja ni ndugu Mwanakombo na Mwanahawa ambao wakati kamati inaanza kazi ya uchunguzi walikuwa tayari wamesimamishwa kazi ili kupisha uchunguzi.

Waheshimiwa Wajumbe, naomba kuchukuwa fursa hii kuwafahamisha kwamba hawa wahusika wote kamati iliwaita na kuwahoji na wamejieleza na wamepewa fursa ya kuzungumza waliyozungumza. Tunarejea tena kama kamati kusema kwamba utaratibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma ichukuliwe na haki itendeke pale ambapo itaonekana wana hatia wachukuliwe hatua na wasipokuwa na hatia waachiwe huru, warejeshwe kazini na wapewe haki zao zinavyostahili

Mhe. Naibu Spika, ndugu Humoud pia amehusishwa na wizi huu na ambaye hadi sasa hajapatikana. Hivyo, tunaendelea kusisitiza kwamba upatikanaji wa Humoud kutawezesha kupata taarifa zaidi za wahusika na sehemu ambayo nyaraka hizi amezipeleka na baada ya kumpa yeye na kuweza kufahamu hivyo, tutaweza pia kufahamu ni akina nani wanaohusika

Mhe. Naibu Spika, Suala la Fuad kupewa shilingi 20. Wako Wajumbe hapa walizungumzia suala la Fuad kwamba amepewa shilingi 20 na suala hili limezungumzwa na Mhe. Hamza Hassan Juma na wengineo, sasa naomba kutoa ufafanuzi ni shilingi 20 au riali 20.

Mhe. Naibu Spika, naomba niseme kuwa kwanza nampa pongezi sana kijana Fuad kutoka katika taasisi hii, kwa sababu kijana huyu ndie alieanzisha hii chachu katika ile taasisi yake. Kitendo cha kuitwa kwake ndugu Fuad ndicho kilichopeleka sasa wale wengine wakaweza kusema kwamba na mimi nimeitwa, mimi nimepigiwa simu na mimi kumetokea hivi. Kwa hivyo, nachukuwa fursa hii kumpongeza sana ndugu Fuad kwa ujasiri wake kuweza kuzungumzia hoja hii na hatimae ikaweza kuleta mjadala kwa wafanyakazi na jambo hili likaweza kujitokeza.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, suala la ndugu Khadija, Mhe. Salim Abdallah Hamad yeye alitaka kujua ni kwa nini baada ya kupigiwa simu usiku alikataa kwenda na mbio akaripoti kwa wakubwa zake, si kuna kitu kilikuwa kinaendelea hapa katika taasisi hii.

Mhe. Naibu Spika, katika hili naomba niseme kama ifuatavyo, suala la Fuad haya yametokezea baada ya wizi kugundulika. Tuseme kwenye ripoti ndugu Khadija alipigiwa simu ya wito wa Humoud mara nyingi kabisa hakuitikia na hakuitikia kama mwenyewe alivyoweza kusema kwamba hakuweza kuitikia kwa sababu aliyekuwa akipiga simu kwanza alikuwa hamjui.

Halafu kwa siku hiyo ambayo bwana alipiga simu wakati wa usiku, Bi. Khadija alisema katika maelezo yake kwamba yeye ni mke wa mtu, itakuwaje mtu ampigie simu usiku atamke aende akaonane naye katika eneo ambalo silo. Hii ndiyo sababu iliyosababisha Bi. Khadija, watu walipoanza kuzungumza na yeye ikabidi azungumze kwamba na mimi nilipigiwa simu na mjadala ukaendelea na hatimaye kuweza kufikia hapa tulipo leo. (*Makofi*)

Hoja nyengine ni hoja ya Mhe. Omar Ali Shehe kuhusu kamati haikukamilisha taarifa yake kwa kuwa hatukusema nani anahusika kama ni ubalozi au Humoud kama yeye.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa naomba niseme ni kweli tumesema kwenye ripoti kuwa hatuwezi kusema kwamba ni Humoud au ni Balozi wa Oman. Tumefanya hivyo ili kuacha vyombo vinavyohusika kwenye sheria vichukue mkondo wake.

Waheshimiwa Wajumbe, naomba tuwe na ufahamu kwamba kamati hii imepewa hadidu rejea mbili:-

1.Kuchunguza ule wizi au upotevu wa nyaraka ulivyotokezea katika ile taasisi ya nyaraka pale Kilimani.

2.Ilikuwa ni kutoa mwelekeo na kuishauri Serikali namna bora ya kuhifadhi nyaraka zilizokuwemo ndani.

Hizo ndizo hadidu rejea tulizopewa kwenda kuzifanyia kazi katika taasisi ya nyaraka. Naomba Waheshimiwa Wajumbe tulikumbukie hilo.

Baada ya hapo, tunakwenda katika suala la ndugu Humoud. Naomba nimalizie maelezo haya kwa kuzungumzia suala zima linalomuhusu mshukiwa mkuu wa tukio ambaye ni ndugu Humoud, raia wa Oman.

Naomba niseme kwamba kamati ikiendelea na kazi yake ya uchunguzi katika suala lililoiweka kamati katika wakati mgumu ni suala zima la bwana Humoud. Kwanza kwa kutaka kujua uhusiano wake kwamba yeye ni nani na anafanya nini Zanzibar. Hasa kwa kuwa Serikali ilikwisha kutoa tamko katika Baraza hili kwamba Humoud siyo mfanyakazi wa Ubalozi.

Hata hivyo, jitihada za kamati katika kuujua ukweli wa kadhia zilifikia maamuzi kwamba ndugu Humoud ni mfanyakazi wa Ubalozi na kuna ushahidi wa kutosha wa kimazingira unaomuhusisha Humoud na mazingira ya wizi wa nyaraka katika mamlaka ya nyaraka pale.

Hivyo basi, ninapenda niungane na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili kwamba Serikali ihakikishe kwamba Humoud anakamatwa anaeleza ni nani waliohusika kumpatia nyaraka na amezipeleka wapi baada ya kupewa nyaraka hizo. Hii ni kwa manufaa ya nchi yetu. Utaratibu wa kisheria wa kumpata Humoud upo katika maamuzi ya Serikali na si vyenginevyo. (*Makofi*)

Mwisho kabisa nimalizie kwa mujibu wa ripoti kwa kusema kwamba napenda kusema kwa kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu hili kwa kutuamini sisi wana kamati, vile vile na kutuunga mkono na hatimaye kuikubali ripoti yetu kama ambavyo tumeiwasilisha hapa Barazani. (*Makofi*)

Kwa kumalizia Waheshimiwa Wajumbe, ninataka wajumbe wangu mufahamu, kamati hii imepata kazi kubwa sana kuweza kukamilisha ripoti hii.

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi hii nikapata muongozo kidogo, kwa sababu sasa hivi Mhe. Mwenyekiti ana-*wind up* na anapo-*wind up* baadae itabidi kutoa hoja na hii hoja ina maana tukiikubali, ina maana hiyo kazi au maazimio itabidi yakafanyiwe kazi na Serikali.

Lakini sasa katika hoja ambazo tulizozitoa kuhusu kumkamata bwana Humoud, sisi tuliomba Serikali, kwa kuwa bwana Humoud yupo Zanzibar akamatwe na Mhe. Waziri Ofisi ya Rais kwa nilivyomsikia kama nilimfahamu vizuri, kama sijafahamu vizuri nitaomba anipe ufafanuzi, kwamba kutokana na sheria zilizokuwepo za kimataifa na za kitaplomasia, Serikali wanashindwa kumkamata na kumuhoji kutokana na kinga ya kibalozi.

Wakati mwenyekiti alivyoeleza katika zile sheria mbili za kimataifa, kwenye yale maazimio ya kimataifa kwamba; kuna sheria moja inamkinga na anaingia katika kinga bwana Humoud na kuna sheria nyengine kwa kuwa amekiuka maadili ya kazi yake aliyokuja kuifanya, sheria ile haimlindi.

Sasa hapa tunalichukulia lipi? Kwa sababu tunapotoa maazimio kama ile sheria ambayo bwana Humoud hampi kinga, kwa hivyo, ina maana tukitoka hapa azimio letu moja Serikali kumkamata bwana Humoud kwa kuwa yupo Tanzania. Sasa kabla hatujapitisha haya maazimio, tulikuwa tunataka tupate kauli au ufafanuzi wa Serikali. Lakini na vile vile Mhe. Mwenyekiti, alitusomea sheria mbili zile, ipi ambayo ilikuwa *alive* na inayofanya kazi, bwana Humoud ana kinga au hana kinga.

Mhe. Naibu Spika, ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Hamza. Mimi ninadhani Serikali ilitoa maelezo lakini kama unataka ya ziada tutamkaribisha Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais aeleze zaidi ili ufahamu halafu mwenyekiti amalizie.

Mhe. Waziri, maelezo ya ziada kabla hatujamaliza.

Mhe. Waziri wa Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa maelezo ya Mhe. Hamza Hassan Juma, kwa mujibu wa maelezo ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, bwana Humoud anayo kinga.

Ndiyo maana wakataka ziada ya ushahidi utakaowasaidia ili waweze kuwasiliana na Serikali na Oman ili kinga hiyo iondoshwe na hatua nyengine ziweze kuchukua mkondo wake. Na kama nilivyosema katika maelezo yangu kwamba kutokana na taarifa hii ya Baraza pamoja na ripoti ambayo Mhe. Waziri atakuwa nayo, hapana shaka yoyote, tutakuwa na ushahidi wa kutosha wa kuweza kuwasilisha Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje kupitia Wizara husika inayosimamia masuala haya ya Ushirikiano wa Kimataifa hapa Zanzibar.

Ninaamini kabisa kwamba ushahidi huu unatosha kuwaeleza wenzetu wa Mambo ya Nchi za Nje waweze kusaidia kuwasiliana na Serikali ya Omani ili mtu huyu sasa aondoshewe kinga na hatua nyengine ziweze kufuatwa.

Ninashukuru sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Hamza, umesikia?

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kuweza kukubali ile taarifa yangu na ufafanuzi wa Mhe. Waziri, nafikiri hata wananchi wataridhika kwamba hata Serikali yenyewe wapo *serious* na kwa kuwa Mhe. Mwenyekiti, amefanya kazi kubwa ya kukusanya ushahidi. Kwa hivyo, ule ushahidi uliokuwa unatakiwa na Wizara ya Mambo ya Nje, sasa hivi tayari upo mkononi na utawasilisha Wizara ya Mambo ya Nje na kinga ya bwana Humoud tunaamini itaondoka na Serikali itaweza kuchukua hatua za kisheria dhidi yake.

Mhe. Naibu Spika, ahsante nakushukuru. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Hamza, mwenyekiti tuendelee.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika, naomba pia nimshukuru Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti kwa kazi nzuri ya umaliziaji ambayo alikuja kuiasisi hapa ya maazimio na kuweza kuisimamia na inaonesha umakini wake Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti kwamba aliisikiliza kwa makini na anafuatilia kila kitu, ili awe aone taratibu zote zinakwenda kwa mujibu wa hali na sheria ambazo tumezitengeneza katika nchi yetu. (*Makofi*)

Lakini pia nimshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kuweza kutamka bayana kwamba amekubaliana na maoni ya kamati ya kwamba ndugu Humoud hana kinga ile ambayo alikuwa amepewa kama ambavyo Wizara ya Mambo ya Nje ilikuwa imezungumzia.

Baada ya maelekezo hayo, sasa naomba Waheshimiwa Wajumbe kwa heshima na taadhima na kwa unyenyekevu mkubwa sana kuweza kuikubali ripoti hii ili hatimaye Serikali iweze kuifanyia kazi, tena bila ya kuchelewa sana. Kwa sababu wananchi wana matumaini makubwa sana na Serikali yao na wanasubiri kwa hamu kubwa kuona utekelezaji wa ripoti hii, hususan baada ya kuona kwamba wananchi wanafuatilia kwa karibu sana suala hili.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelekezo hayo naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Sasa Waheshimiwa Wajumbe baada ya ripoti yote na Mwenyekiti kufanya majumuisho, sasa niwahoji Wajumbe wale waliokubali taarifa ya Kamati Teule ya Kuchunguza Upotevu wa Nyaraka pamoja na mapendekezo yake wanyooshe mkono ili Serikali iyafanyie kazi, waliokataa. Waliokubali wameshinda. (Makofi)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Kwa hivyo, tunampongeza mwenyekiti na kamati yake na sasa kazi tunaiachia Serikali, baada tutapata matokeo yake.

Baada ya kazi hiyo, leo tuna kazi ya pili.

HOJA YA BINAFSI YA MJUMBE

Kutaka Serikali Kuchukua Hatua za Kuwatimizia Wazanzibari wote Waliotimiza Sifa za Sheria Haki yao ya Kuwapatia Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi (*ZAN-ID)*

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu, kwa heshima kabisa naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma, aliyetujaalia leo tukawepo hapa tukifanya shughuli ya kuwakilisha waajiri wetu. (*Makofi*)

Baada ya kupitisha, kuipokea na kuikubali taarifa muhimu ya Kamati Teule kama ilivyowasilishwa.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijawasilisha hoja yangu binafsi, naomba kusema haya yafuatayo. Kumekuwa na malalamiko kwa *ZBC* kwamba kuna mtindo wa kuwafanya baadhi ya Wajumbe kuwa mababu. Kwa maana ya kwamba wanasema lakini pengine kwa sababu yanayosemwa hawataki, Wajumbe wale wanaonekana wakimumunya midomo, wakirusha mikono lakini sauti haipatikani.

Tunamuomba sana Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, hili lisitokee kwa sababu hichi ndicho chombo cha wananchi, wananchi wako sasa hivi katika redio, kwenye televisheni wanasikiliza wale ambao wamewatuma kufanya kazi wanafanya kazi. Sasa wasiposikika wakawa wanaonekana tu wanatupa mikono na kumumunya midomo, hii si haki.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe hawasikiki kwenye redio au kwenye televisheni.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Kwenye televisheni, wanaonekana kama mababu.

Mhe. Naibu Spika: Redio wanasikika.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Na hiyo redio ndiyo kabisa, maana yake utasikia mitambo imeharibika, kuna matatizo ya kiufundi. Haya ndiyo malalamiko ya wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri, kasikia.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Na Waziri amesikia kama yupo au kama hayupo, anayemuwakilisha yupo.

Mhe. Naibu Spika, jana Jumpili tarehe 29/03/2015, majira ya Magharibi, wakati wanachama na wafuasi wa Chama cha CUF wanatoka kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika Makunduchi...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa hii ndiyo ripoti. Hebu soma kwanza ripoti, unatupeleka siko, wewe nimekupa usome ripoti.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mheshimiwa, tuna kawaida...

Mhe. Naibu Spika: Ninasemaje, hebu sikiliza mimi ndiye ninayeongoza kikao. Ninasemaje nimekwita utoe Hoja Binafsi. Tatizo la kuwa watu hawasikii kwenye televisheni na redio nimekuruhusu, kwa sababu ni jambo la kawaida, unasema wananchi watusikie.

Sasa soma hoja yako halafu tutachangia pamoja. Ukianza kutoa hoja nyengine hamna humu, hatumalizi wala husomi hoja.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Naibu Spika, nakuheshimu sana na nakushukuru sana, lakini hata kwenye maswali na majibu, watu huwa wanatoa salamu, wanapongeza na unawaachia. Ninakushukuru sana na nitaendelea na hoja unavyotaka.

Mhe.Naibu Spika, hoja yangu binafsi ni kwa mujibu wa Kanuni chini ya Kifungu cha 27.

TAARIFA

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima, tunaishukuru redio Zanzibar hivi sasa wapo *alive* na wananchi wanasikiliza hoja.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, endelea.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Naibu Spika, kwa kutumia Kanuni ya 27 (3), 48 (2), 49(1), 50(1) na 50(2) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2012, nina heshima kubwa kwa wananchi wa Zanzibar tunaowakilisha hapa katika chombo chao hichi kitukufu kuwasilisha Hoja Binafsi kuhusiana na kuitaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuchukua hatua za kuwatimizia Wazanzibari wote waliotimiza sifa za kisheria haki yao ya kuwapatia vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi *(Zan-ID)* kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 Toleo la 2010, Ibara ya 6(1) inatambua kuwepo kwa Mzanzibari ambaye upatikanaji wake, upoteaji wake na urudishwaji wake atakuwa kama alivyoainishwa katika sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

Kwa kuwa Baraza la Wawakilishi limetunga Sheria Na. 5 ya 1985 ambayo katika Kifungu cha 3 na 4 kinatambua kuwepo kwa Mzanzibari pamoja na sifa na masharti yake.

Na kwa kuwa Baraza la Wawakilishi limetunga Sheria Na. 7 ya 2005 ambayo imeanzisha utaratibu wa usajili Wazanzibari Wakaazi na kuwapatia vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi *(Zan-ID)* kwa kila Mzanzibari aliyetimiza sifa na masharti ya kisheria.

Na kwa kuwa kwa mujibu wa Kifungu cha 6 cha Sheria hiyo Na. 7 ya 2005 ni wajibu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Mkurugenzi wa Ofisi ya Usajili wa Wazanzibari Wakaazi kumpatia kila Mzanzibari Mkaazi aliyetimiza sifa na masharti yaliyotajwa kwenye sheria hiyo kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi *(Zan-ID)*.

Na kwa kuwa kwa mujibu wa Kifungu cha 15 cha Sheria hiyo Na. 7 ya 2005 ambacho kiilifanyia marekebisho Sheria ya Mzanzibari ya Na. 5 ya 1985 kwa kuongeza Kifungu cha 4(a) ambacho kinakifanya kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi kuwa ni haki ya kisheria na kila Mzanzibari Mkaazi aliyetimiza sifa na masharti yaliyotajwa kwenye sheria hiyo na kwamba kitambulisho hicho kinatumika katika kumtambulisha Mzanzibari Mkaazi katika kupata haki zake nyengine ambapo kwa kutokuwa nacho anazikosa.

Na kwa kuwa kwa mujibu wa Kifungu cha 14 (1) (a) cha Sheria Na. 7 ya 2005 niliyoitaja hapo juu, ni kosa la jinai kwa Mzanzibari Mkaazi aliyetimiza sifa na masharti yaliyotajwa kwenye sheria kutokuwa na kitambulisho cha *Zan-ID*, kosa ambalo likithibitika adhabu yake ni faini isiyopungua shilingi laki moja au kifungo kisichozidi mwaka mmoja au vyote viwili faini na kifungo.

Na kwa kuwa kumekuwa na vitendo vya makusudi kwa upande wa watendaji wa Serikali kwa mamlaka zinazohusika kuwanyima idadi kubwa ya Wazanzibari Wakaazi wenye sifa zote za kisheria kitambulisho cha *Zan-ID* na wakati huo huo kuwapatia watu wengine wasio Wazanzibari vitambulisho hivyo, mambo ambayo yote ni kinyume cha sheria.

Na kwa kuwa jambo hilo limeshazungumzwa sana na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika mikutano ya Baraza la Wawakilishi na kuitaka Serikali ichukue hatua dhidi ya watendaji wake wanaoshiriki katika ukiukwaji wa sheria kwa kuwanyima Wazanzibari Wakaazi waliotimiza sifa za kisheria kitambulisho cha *Zan-ID*.

Na Mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuchukua ahadi ya kulishughulikia suala hilo. Na kwa kuwa ahadi hizi zilizotolewa na Mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hazijatekelezwa kwa vitendo hadi sasa, huku Wazanzibari wengi wakiendelea kuteseka kwa kunyimwa haki yao hiyo ya msingi kisheria.

Na kwa kuwa hivi sasa ambapo tunakaribia kupiga kura ya maoni kuhusu Katiba inayopendekezwa, kuna Wazanzibari wasiopungua 30,000 wanasubiri kusajiliwa na kupatiwa *Zan-ID* ambapo wengine wana Stakabadhi zao mikononi na wengine wana zaidi ya miezi sita hawajapata *Zan-ID* zao huku wakiendelea kuhangaishwa na watendaji wa Ofisi ya Mkurugenzi wa Usajili wa Wazanzibari wakaazi.

Kwa kuwa hivi karibuni Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar *ZEC*, itaendesha zoezi la uandikishaji wa wapiga kura wapya, kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, ambapo bila ya kuwa na *ZAN-ID* mtu hataweza kuandikishwa, na hivyo kumkosesha haki yake ya msingi ya kupiga kura na haki ya kutoa ridhaa yake kwa mamlaka ya serikali, huku tukitambua kwamba Ibara ya 9 fasili ya (2)(a) ya Katiba ya Zanzibar, inatamka kwamba wananchi ndio msingi wa mamlaka ya nchi, na kwamba nguvu za serikali na vyombo vyake vyote vitatoka kwa wananchi wenyewe.

Hivyo basi, Baraza la Wawakilishi ambalo kwa mujibu wa Ibara ya 5(a) ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, toleo la 2010 ndilo mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma, linaitaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Ofisi ya Msajili wa Wazanzibari Wakaazi kuchukua hatua zifuatazo.

1. Iwatake Masheha wa Shehia zote za Unguja na Pemba, kuwapatia Wazanzibari wote wenye sifa, fomu za maombi ya kusajiliwa kama Wazanzibari Wakaazi bila ya ubaguzi na bila ya usumbufu.

2. Iitake Ofisi ya Msajili wa Wazanzibari Wakaazi kuwapatia ndani ya mwezi mmoja, kutoka tarehe ye kupitishwa hoja hii, vitambulisho vyao vya *ZAN-ID* Wazanzibari wote ambao tayari wamekamilisha taratibu za kupatiwa *ZAN-ID* na ambao wamekuwa wakisumbuliwa kwa muda mrefu kwa visingizio vingi, bila ya kupatiwa *ZAN-ID* zao.

3. Iitake Ofisi ya Usajili wa Wazanzibari Wakaazi, kufanyia kazi maombi yote mapya ya *ZAN-ID*, yatakayowasilishwa kwake baada ya Masheha kutoa fomu hizo za maombi kwa waombaji, ndani ya miezi miwili tokea tarehe ya kupokea fomu za maombi ya kupatiwa vitambulisho vya *ZAN-ID*.

4. Iwashirikishe Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa kuchaguliwa na wananchi katika hatua zote hizo, ili kuona suala hilo linapatiwa ufumbuzi wa kudumu na kuepuka uzoefu wa ahadi zilizowahi kutolewa huko nyuma, ambazo hazijatekelezwa kwa nia njema kama inavyopaswa.

5. Iwasilishe taarifa rasmi ya utekelezaji wa hatua namba 1 hadi 4 zilizotajwa hapo juu, mbele ya Baraza la Wawakilishi katika mkutano. Hapa Mheshimiwa mwezi Machi ni huu, kwa sababu hoja hii niliipeleka mapema katika kikao kilichopita, kwa hivyo nikisema Machi hapa, naomba tufanye marekebisho, kwa sababu hoja hii ilikuwa ijadiliwe katika kikao kilichopita.

   Kwa hivyo, niisome kwamba iwasilishe taarifa rasmi ya utekelezaji wa hatua namba 1 hadi 4, zilizotajwa hapo juu mbele ya Baraza la Wawakilishi katika mkutano ujao.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mheshimiwa, hoja imeungwa mkono. Ninao wachangiaji wawili wa mwanzo, wa kwanza Mhe. Hassan Hamad Omar na wa pili Mhe. Ashura Sharif Ali. Tujali muda na twende kwenye *point* yenyewe.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ya kutoa mchango wangu kwenye hoja binafsi ya kadhia ya upatikanaji wa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi *ZAN-ID*.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala*, aliyenijaalia mimi kuwa katika uhai, uzima na afya inayoniruhusu kuzungumza ndani ya Baraza lako Tukufu hili.

Mhe. Naibu Spika, nikielekea katika mchango wangu huu wa kadhia ya vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, ni ukweli usiofichika kabisa kwamba kumekuwa na tatizo na usumbufu mkubwa katika Ofisi ya Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, kuwanyima haki watu wenye haki na kuwapa watu waliokuwa hawana haki vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, ukizingatia kwamba Vitambulisho vya Mkaazi ni kitambulisho muhimu sana kwa Mzanzibari na jamii kwa jumla.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu huu, niseme jambo hili Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tumelizungumza sana, lakini ni sawa sawa na *kutwanga maji kwenye kinu,* hayakai. Unapotwanga maji kwenye kinu hayakai, ndio maana nakwambia kuwa jambo hili halishughulikiwi inavyopaswa.

Mhe. Naibu Spika, itakumbukwa Mheshimiwa aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Baraza la Mapinduzi, Mhe. Mwinyihaji Makame, tulikamatana katika kipindi kimoja cha bajeti na tukakubaliana kwenda kuona na alitukusanya sote katika ukumbi wa Benjamin Mkapa kule Kisiwani Pemba.

Aliwaita Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Masheha, Wabunge, Wawakilishi na Madiwani sote kwa pamoja tulikuwepo. Basi tukasema jambo hili likome, kila mtu mwenye kutimiza masharti ya kisheria basi kupatiwa *Zan-ID* ni haki yake ya kimsingi. Lakini jambo la kusikitisha, kumekuwa na ubaguzi wa kutosha kabisa, wengine wanapatiwa na wengine hawapatiwi, kulikoni? Tunaulizana kulikoni, ni sababu gani za msingi wengine wapate na wengine wasipate, wakati masharti yote wameyatimiza. Sisi hatupiganii mtu aliyekuwa hakutimiza masharti, lakini aliyekuwa katimiza masharti basi ni haki yake apewe lakini mpaka leo kuna usumbufu wa kutosha.

Mhe. Naibu Spika, leo ukienda katika Ofisi ya Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi basi wanakwambia kwamba *material* haya yaliyoletwa hayakidhi haja sio mazuri, lakini hapo hapo wengine wanapewa, wanaambiwa, wanaleta maombi yao wanachukuliwa risiti zao wanakuja kupewa. Je, ni sababu gani wengine *material* yawe mabaya na wengine yawe mazuri. Hili ni jambo la makusudi limepangwa, na tunaiomba serikali jambo hili likomeshwe kwa watendaji wake, kwa sababu ni jambo la kisheria basi liende kisheria.

Mhe. Naibu Spika, nazungumza tena, sisi tunazungumza kwa wale waliotimiza taratibu za kisheria basi wapewe haki zao, hii ni haki ya kila mtu. Hivi serikali ina woga gani, hebu tuambieni kuna woga gani serikalini? Jambo hili lilipangwa hapa na likapitishwa ndani ya Baraza la Wawakilishi. Kama inavyozungumza Ibara ya 6(1) ya Katiba yetu ya Zanzibar, naomba ninukuu ibara hii inavyozungumza;

Ibara ya 6(1)

> "Kutakuwa na Mzanzibari ambaye upatikanaji wake, upoteaji wake na urudishwaji wake, utakuwa kama ilivyoainishwa katika sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi"

Nikiendelea na ibara hiyo hiyo ya 6(2);

> "Kila Mzanzibari kwa misingi ya Katiba hii anaweza kufaidi haki na fursa zote anazostahiki Mzanzibari na anapaswa kutekeleza wajibu, majukumu na dhamana ya Mzanzibari kama ilivyo kwenye Katiba hii au kwenye sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi".

Kila Mzanzibari anayo haki na wajibu wa kupata haki zake za kimsingi kama ilivyoainishwa na sheria pamoja na Katiba hii ya Zanzibar. Haya, ni sababu gani za msingi zilizowafanya wengine kuwanyima haki hiyo na wengine wakapata, tunaiomba serikali itueleze kwa kina jambo hili.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu, tarehe sikumbuki lakini ni mwezi wa Januari, 2015 Sheha wa Shehia ya Kiungoni Omar Khamis, watu walikwenda nyumbani kwake kama mwenye dhamana ya kutoa fomu na kuwapatia wananchi ili kwenda kupata vitambulisho. Mheshimiwa huyu alijifanya kama Mungu mtu, namtaja kwa jina Omar Khamis wa Shehia ya Kiungoni.

Akawaambia ili mpate vitambulisho basi mwende mkachukue mchanga mpeleke *nursery* na baadaye mje mchukue fomu ili mpate hizo barua za kwenda kuchukua vitambulisho. Mhe. Naibu Spika, wananchi walimpiga vichwa Sheha wakaenda wakachukua mchanga wakaleta *nursery*, na *wallahi* hakuwapa fomu za kwenda kuchukulia vitambulisho. Je, hapo napo mtasema ni uongo.

Ushahidi mkiutaka nitawatia melini wote watakuja hapa Baraza la Wawakilishi, ushahidi wangu siji na karatasi, nitakuja nao wote nitawalipia gharama zote na nitawaleta wote walionyimwa. Ni kwamba kama haitoshi, watu hawa walikwenda mpaka katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, na Mkuu wa Wilaya akasema atalishughulikia jambo hili na mpaka leo hii tunazungumza bado halijapata ufumbuzi.

Wananchi wamehangaika wamekwenda katika Kituo cha Polisi Mchangamdogo pia kulishtaki jambo hili. Kituo cha Polisi Mchangamdogo wakawajibu kwamba tutakwenda na *OCD* katika Shehia ya Kiungoni kwenda kulimaliza tatizo hilo, mpaka leo halijapata ufumbuzi hivi ninavyozungumza. Je, kuna usawa, huu si ni ubaguzi wa kutosha, kwa nini wengine wapate na wengine wasipate?

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu. Imekuwa kama *comedy*, tunazungumza tu mambo hayafanyiwi kazi, tunaomba yafanyiwe kazi, tukizungumza hatuzungumzi kwa utashi. Mhe. Haji Omar Kheri katika bajeti iliyopita, tulizungumza naye na akatupa ahadi mpaka tupungukiwe na kazi nyingi za Bunge la Katiba, lakini limemaliza mpaka leo hajatutembelea pamoja na Mhe. Subeit Khamis Faki yule pale.

Mhe. Naibu Spika, ili nithibitishe kwamba jambo hili ni kweli, ninavyo vivuli vya vyeti vya kuzaliwa kwa wananchi wa Jimbo la Kojani katika Shehia mbali mbali, zisizopungua 103, ninavyo vivuli hapa, ninayo orodha ya watu wasiopungua 50 waliokwenda kupiga picha na mpaka leo wengine wana miezi sita, wengine miezi nane na wengine wana miezi mitatu na mpaka leo hawajapatiwa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, vivuli vyake ninavyo hapa Barazani. Naomba mfanyakazi wako wa Baraza hili aje achukue akukabidhi Mhe. Naibu Spika, kama ni ushahidi tosha kwamba watu wananyimwa haki zao, nakuomba uje hapa. Njoo unakuwa mwoga, njoo uchukue vitu hivi!*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba umkabidhi. Hivi ni vya watu wa Kojani tu, lakini sio kama Kojani tu wanaonyimwa, Zanzibar nzima watu wananyimwa.

Mhe. Naibu Spika, sina haja ya kusema mengi katika kadhia hii, lakini muhakikishe kwamba inavyofanywa sivyo, kama ni serikali mpange mikakati ya makusudi, mujue mnawadhulumu watu, na Mwenyezi Mungu hatowasamehe hata siku moja. Kwa haya machache naomba nikae kitako, ahsante sana nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nianze kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, aliyetujaalia uhai lakini pia akatupa na uzima, akatuwezesha kuwepo kwetu hapa katika Baraza lako hili kutekeleza majukumu yetu, lakini haya yote ni kwa maslahi ya wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipatia na mimi fursa hii ya kuweza kutoa angalau mchango wangu mdogo katika hii hoja binafsi ambayo imewasilishwa mezani muda sio mrefu uliopita.

Mhe. Naibu Spika, nianze kusema kwamba serikali ni tegemeo la wananchi, na serikali yetu imekwenda katika mifumo ya kidemokrasia ambayo inawashirikisha watu kuiweka madarakani serikali hiyo, na serikali hukaa madarakani kwa ajili ya kuwatumikia watu.

Mhe. Naibu Spika, ni aibu, na ni fedheha kila mara inapofika wakati Wajumbe wa Baraza lako hili Tukufu, kusimama na kusema kwamba kuna haki za msingi za wananchi wa Zanzibar wananyimwa na serikali yao, hii ni aibu.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba, hivi serikali inavunja Katiba kwa makusudi, hii ni haki ya kikatiba, ipo katika Katiba yetu ya Zanzibar, mwananchi Mzanzibari atakayetimiza masharti umri wa miaka 18 apewe kitambulisho chake cha *Zan-ID*, hii ni Katiba.

Mhe. Naibu Spika, hivi tunauliza kuna sababu gani za msingi za kunyimwa haki zao hizi. Mhe. Naibu Spika, kitambulisho hiki wananchi wetu tumeamua kwamba wawe nacho, tuna sababu mbali mbali ambazo kwa wakati huu tunatumia, vijana wetu wanapofikia kufanya mitihani ya kidato cha nne, huwa wanatakiwa *Zan-ID* zao. Lakini kumekuwa na usumbufu mkubwa na kujenga tabaka mbili katika Taifa moja, vijana wengine wanakwenda wanapata na vijana wengine wanakosa, na ni vijana wa Taifa moja, hii ni hatari. Tunapandikiza chuki hata kwa vijana wetu wakati huu.

Mhe. Naibu Spika, tukijiuliza hivi jamani kwenye sheria na utawala bora ndio tumeshafika hapa, huo ndio utawala bora? Tumekubali wenyewe kufuata hii demokrasia na utawala bora, tunajigamba sisi haki za binadamu, tunafuata utawala bora, ndio huu wa kuwabagua watu wengine ukawapa na wengine ukawanyima.

Mhe. Naibu Spika, nasema kwamba umefika wakati serikali mjitathmini na mjikumbuke kwamba nyinyi ni wanadamu kama walivyo wanadamu wengine, lakini niwakumbushe kwa kuwa Mwenyezi Mungu mtukufu amesema; *Fadhakir Fainnadhikra Tanfaul Muuminiim.*

Nyinyi ni waumini, mjue kwamba mtakufa, na Mwenyezi Mungu atakuulizeni kwa dhamana alizokupeni, kama mnawanyima Wazanzibari na kuwabagua, mjue kwamba kuna siku mtakutana na Mola wenu, atakuulizeni juu ya dhamana hizo alizokupeni, juu ya viti hivyo alivyokuwekeni, yeye ndiye mwenye kuweka na ndiye mwenye kuondosha, muhakikishe mtakutana naye.

Hivi waumini nyinyi ndugu zangu wa Kizanzibari, kwa mapenzi makubwa mnawanyima watu haki zao, mmeweka sheria kwamba ukienda kukata tiketi ni lazima uwe na kitambulisho, umemkusudia nini yule ambaye unamnyima. Nchi yetu ni visiwa, tumezoea kuingia, kwenda na kutoka, ikiwa unamnyima maana yake nini, unamtia usumbufu makusudi, umekusudia kufanya haya kwa nia gani.

Mhe. Naibu Spika, nasema serikali, serikali chonde chonde na ubaguzi huu ambao utawagawa Wazanzibari kwa hatua kubwa, jambo ambalo hatulitarajii. Tunachokipenda ni umoja wetu kama ilivyo serikali yetu ya Umoja wa Kitaifa, iweze kudumu na kuweza kuleta maslahi kwa Wazanzibari wote.

Naiomba serikali ilichukulie uzito suala hili halikuwa la masihara. Mimi binafsi sikuwa nimejiandaa, lakini baada ya kukumbuka kwamba siku tuliyoachana hapa kulikuwa na hoja ambayo hati iliwekwa mezani, basi nilipata taarifa kwamba kuna hili, nikakumbuka asubuhi ya leo.

Waheshimiwa Wajumbe, mnauona ukindu na utembo wa kijijini kabisa wa kamba za migomba, nina *document* hizi zipatazo 250, hivi ni vyeti vya kuzaliwa, umri wao tayari umeshatimia kabisa hawa vijana, wameshasumbuka kwa Masheha wenu ambao serikali ndio wateuzi wa Masheha hao, mna maagizo binafsi.

Nawaombeni, chonde chonde na amani ya Zanzibar, Wazanzibari ni watulivu na ni wapenda amani, endapo mnafanya vitu hivi unamnyima haki yake, atadai, na hatimaye atabadilisha imani, jamani tutakwenda wapi wakubwa mtahama sisi wanawake na watoto wa Taifa hili twende wapi na vituko hivi vinaendelea na ndio maana nasema hili.

Mhe. Naibu Spika, jana baada ya kutoka katika mkutano wetu wa kidemokrasia kabisa kule Makunduchi, vijana wameathiriwa na wako hospitali ya Mnazi Mmoja tena kwa makusudi. Nawaambia amani ilioko Zanzibar ni hazina njema mnaichokoa chokoa, pakichafuka hapatatulia Zanzibar. Tumekuwa wenye sifa kubwa ya kutunza amani ya Wazanzibari, watu wamekuja kusoma kwetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi binafsi nilipata fursa ya kwenda kwa wenzetu kule Tanganyika, pamoja na Mhe. Mgeni Hassan kujadili amani ya Tanzania, na sisi kama Zanzibar tuliipataje Serikali ya Umoja wa Kitaifa, tukakubaliana kwa yale machungu tuliyokuwanayo nyuma, walitaka kusoma kwetu. Sisi walimu leo tunataka kuharibu, kwa sababu tu ya vijijambo fulani. Tukiwa tunafahamiana sisi sote ni watoto wa mjomba na shangazi, wewe ukiwa Mtumbatu mimi nakuwa Mmakunduchi. Jamani ndugu zangu, naiomba serikali kwa suala hili, mjue kwamba mnapoteza hata maendeleo ya Taifa letu, hawa vijana wengine wanakwenda kusoma wengine ni wasafiri, pamoja na hiyo mifumo yetu kwamba *Zan-ID* nazo hutumika katika upigaji wa kura ambapo pia nalo kikatiba ni haki yake atakapofikia umri wa miaka kumi na nane kijana kwenda kupiga kura kutoa maamuzi kwa ajili ya kuona kwamba nani anataka aongoze Taifa hili.

Hizo ni haki zao, kuna nini mpaka tunafikia hatua hii, niiombe Serikali, naiomba sana Serikali msijaribu kuchezea chezea haya mambo mkayaona madogo, checheya moja ya moto ikiwaka basi itaunguza na kumaliza Zanzibar nzima, na Zanzibar ni yetu sote lazima tuliheshimu hili.

Kama ingelikuwa watu hawa hawakutimia sifa ningekuwa sina hoja na wala nisingekuwa na la kusema, lakini nakwambieni kuna watu wengi kwa maalfu hawakupewa haki zao hizi, na wametimiza hasa sifa, kama mnayafanya kwa makusudi hapa duniani Mungu atawajibu kesho *yaumul qiyama*, ndio *ahkamul haakimin,* tujue tu nakumbusha na ni kawaida yangu inapofika mambo yakafika hapa huwa napenda sana kulisema hilo, nalisema kwa sababu kwamba inawezekana watu walighafilika na hii dunia lakini tujue sisi ni waondokaji. Mchezo wa dunia usifikie pahala ukanyima haki za watu na fursa zao, aliyekuweka ni Mwenyezi Mungu na akitaka uondoke huna hila ya kubaki ndugu zanguni.

Kwa vyeti hivi vilivyopo, kwa ushahidi na uthibitisho ambao upo mwingi kuliko huu, ukinambia nikakuletee mia mbili na hamsini (250), miambili na hamsini nitakuletea, ukiniambia mia tatu (300), elfu tatu (3,000)pia zitawezekana zitapatikana.

Hivi Serikali tunaposimama hapa mnasema mara nyingi jamani Wawakilishi wasiseme tu jambo ambalo hawana uhakika, ushahidi ndio huu, nataka nikae kitako na Serikali itujibu ni lini hasa itawapatia Wazanzibari hawa vitambulisho vyao, haki zao hizi ni lini hasa itawapatia haki zao hizi, ni lini hasa lazima serikali itujibu.

Hatuwezi kukaa kimya kuona vijana wetu wanataka kufanya mtihani wa *Form IV* hawawezi kupata haki hizo, tunataka kusafiri lazima uende na kitambulisho, unataka kuajiriwa masikini unaambiwa upeleke kitambulisho, huna masikini anakosa kazi anakosa kila kitu.

Naiomba Serikali kwa heshima zote, kwamba itujibu, ni lini itawapatia Wazanzibari hao vitambulisho hivi, hii ni haki ya kikatiba, hii ni haki ya kikatiba kabisa, Serikali mnavunja Katiba mnafuata ipi?

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, nakushukuru, Ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Naibu Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu katika suala ambalo liko mbele yetu, kabla sijazungumza lolote nataka niliambie Baraza lako Tukufu kwamba sisi ni Wajumbe wa Baraza hili, kwamba tuna haki ya kusema mambo ambayo wananchi wetu wanatulalamikia. Tunapata malalamiko ya muda mrefu kwamba haki zao za vitambulisho hawazipati na ni haki yao.

Mhe. Naibu Spika, nataka niseme kwamba suala hili la vitambulisho na ni haki yao na nataka niseme kwamba suala hili la vitambulisho tangu mwaka 2005 mpaka kufika 2010, na sasa hivi tuko 2015, malalamiko haya tangu siku hizo mpaka leo bado yanaendelea, kwamba watu hawapewi haki zao, lakini mimi nataka nimuulize Waziri

ambaye anayehusika, ivyo hivi vitambulisho vya Uzanzibari ukaazi ni haki yao au ni fursa. Natumia neno la Kiingereza au nitatumia maneno ya Kiingereza mawili yanayosema moja ni *right* na moja na *privilege* namuuliza Waziri, hivi vitambulisho wa Mzanzibari Mkaazi ni *right* au *privilege* ya wananchi, mimi ninavyoamini si *privilege* ni *right* yao, sasa kama ni *right* yao kwa nini hatuhakikishi sheria ipo tuliyoitengeneza sisi wenyewe kwamba watu wote wapewe. Kama ingelikuwa watu hawa wanapewa haki zao wasingekuwa na malalamiko haya, kwa hivyo kama ilianza mwaka 2005 malalamiko yanaendelea mpaka leo 2015, hatuoni kwamba hapa Serikali haijafanya uhalali kwa suala hili.

La pili, naunga mkono hoja hii binafsi ambayo imetolewa na Mjumbe mapema sana, kwamba na mimi naiunga mkono hoja hiyo kuhusiana na kutaka Serikali kuchukua hatua za kuwatimizia Wazanzibari wote waliotimiza fursa, waliotimiza sifa kubwa za kisheria haki yao ya kuwapatia vitambulisho vya Uzanzibari ukaazi. Sasa kama ni haki yao hii tayari tamko la mwanzo linatoka kwamba sheria iko tayari imetengenezwa, kwamba watu wapewe haki yao ya Uzanzibari ukaazi hilo la kwanza.

Lakini la pili vile vile Katiba yetu ya Zanzibar ya mwaka 1984 toleo la mwaka 2010 ibara ya 64 inatambua hapa linakuja suala la kutambua (*recognition),* ina-*recognize,* inatambua sheria hii kuwepo kwa Mzanzibari Mkaazi hilo ni moja, inatambua kuwepo kwa Mzanzibari mkaazi. Lakini la pili vile vile isitoshe kwamba Baraza hili hili la Wawakilishi limetunga sheria namba 5 ya mwaka 1985 ambapo kifungu cha tatu na cha nne kinatambua kuwepo kwa Mzanzibari, lakini zaidi ya hivyo imeonesha vile vile kwamba anapokuwa Mzanzibari pamoja na sifa zake pamoja na masharti yake, sasa mtu hawezi kuomba kitambulisho ikiwa sifa hana au ikiwa masharti hakuyatimiza.

Kwa hivyo ina maana hawa wananchi wetu malalamiko wanayotulalamikia ni kwamba sifa wanazo na masharti halali yapo vile vile.

Lakini jengine vile vile katika mwaka 2005 sheria ilitungwa tena vile vile sheria namba 7 ambayo imeanzisha utaratibu wa usajili wa Mzanzibari mkaazi, kwamba watapatiwa vitambulisho vya Mzanzibari mkaazi yaani hii tunaiita kwa jina la *Zan-ID*, na mimi nasema hii ni hasara kubwa sana kwa sababu tukiwakosesha huko mbele tumeweka sheria kwamba mtu atakayekuwa hana *Zan-ID* hatokuwa na kitambulisho cha Mzanzibari mkaazi basi mawili katika mojawapo linaweza kumpata; ama kuchezea kifungo cha mwaka mmoja au faini au yote mawili hii sheria imeshaweka wazi. Kwa hivyo tukimnyima ina maana huyu mtu tunataka tumtie adabuni, kwa hivyo hatuwezi kuwatia adabu hivi sasa watu kwa sababu hatujawa tayari katika kuwapa watu wetu vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ambalo nataka nilizungumze ni kwamba tuna Ofisi ya Mkurugenzi ambaye Mkurugenzi huyu kazi yake kuweka usajili wa Mzanzibari mkaazi, na huyu mkurugenzi anatakiwa yeye kwamba ampatie kila Mzanzibari ambaye ametimiza sifa na masharti ya Uzanzibari wake apewe kitambulisho.

Suala hili Mhe. Naibu Spika, limekuwa likipigwa dane dane, hakuna aliyekuwa hajui kwamba hii sheria ipo na kama hivyo nilivyoitolea.

Lakini vile vile katika mwaka huu wa 75 katika Baraza letu la Wawakilishi tuliongeza baadhi ya mambo hapa katika Baraza la Wawakilishi, kusema kwamba kifungu cha nne imefanya kitambulisho cha Mzanzibari kuwa ni haki yake ya kisheria, kila Mzanzibari ana haki ya kupata kitambulisho cha Mzanzibari mkaazi. Kwa hivyo sheria ziko nyingi tu mulizozitunga katika Baraza la Wawakilishi ili kumhakikishia kwamba mwananchi naye apate haki yake. Kama mfano wa *passport* kwa nchi za wenzetu, *passport* ni *right* yao, kila anayezaliwa hata azaliwe leo bila ya kufikia umri maalum, lakini ana haki ya kupata vitambulisho hivyo.

Kwa hivyo sifa zipo, masharti watu wanayo lakini bado watu wanaendelea kunyimwa haki zao. Katika yote hayo Mheshimiwa mimi nataka nizungumze haya yafuatayo, nataka niendelee katika upande wa watendaji. Imekabidhiwa watendaji katika Wilaya zetu wapo watendaji na hawa watendaji ndio wanaoleta usumbufu wa kuwapa vitambulisho vyao.

Mhe. Naibu Spika, hili suala lipo watu wanateswa katika wilaya zao wanapokwenda baada ya kutaka vitambulisho hawapewi na wanapewa tarehe njoo kesho njoo keshokutwa, hayo ni mambo ambayo yanatendeka katika Wilaya zetu. Sisi kama ni Wawakilishi tunazungumza na Afisi za Wilaya kuwaambia jamani ee watu mnawataabisha wanakuja na vitambulisho vipo hamuwapi, kwa hivyo hilo lipo Mhe. Naibu Spika, na leo tunalilalamikia tena katika

Baraza lako kwamba Wilaya inachukua nafasi ya kuwahangaisha wananchi wetu wasipewe vitambulisho vyao na wakati vitambulisho vipo wanapigwa *date* njoo kesho, njoo keshokutwa.

Mhe. Naibu Spika, nataka nikwambie kwamba mimi nina jimbo na wenzangu vile vile wana majimbo kila jimbo lina watu wengi tu, na sasa hivi idadi ni kubwa sana, sasa hivi tuna idadi kubwa. Mimi kwa upande wangu nina idadi ya watu ambao hawa ndio katika orodha zangu hizi hapa watu hawapungui 200 ambao wamesajiliwa, hii ni *new registration* ya juzi tu ambao katika mwezi wa Julai hadi leo Machi, 2015, watu hawa wanaofika mia mbili (200), na wa juzi tu hawa hawajapewa vitambulisho vyao ni siku nyingi, kuanzia Julai 2014 mpaka leo Machi, 2015, watu hawa hawajapewa. Lakini nategemea Daftari la Kudumu litakuwa haliko mbali, kwa nini suala hili linakuwa ni vikwazo, hili ni suala kubwa sana, kwa hivyo tunayo idadi kubwa katika kila jimbo watu wapo ambao wanateswa hawapewi.

Vile vile nilizungumzia kwamba dafrari la kudumu la wapiga kura halipo mbali tunategemea daftari hili labda mwezi wa Mei, 2015 litakuwa tayari, je ikiwa mpaka sasa watu hawajapewa vitambulisho vyao watapata vipi *vote* za *ID*, huwezi kupata *Vote ID* kama huna *Zan -ID*. Kwa hivyo kwa nini watu wananyimwa *Zan-ID,* hii ni mikakati ya makusudi kutaka kuwafanya watu wetu hawa wasiweze kupiga kura au kujisajili katika daftari la Mei ndio maana yake, hakuna sababu zozote za msingi kwamba *registration* baada ya Mwezi wa Julai au kuanzia mwezi wa Julai hadi leo Machi, 2015 hakuna vitambulisho vilivyotolewa katika Wilaya yoyote, aseme Mkurugenzi ambaye anashughulika na mambo ya vitambulisho kama ametoa vitambulisho kuanzia Julai, mwaka jana 2014 hadi leo Machi, 2015, kama kuna vitambulisho vyovyote vilivyopelekwa, hii ni mikakati maalum imepangwa.

Na watu wa Wilaya wanafanya mikakati maalum kuwazuia watu wetu wasiwape vitambulisho, Afisi za Wilaya sisi wenyewe Wawakilishi tumekwenda zaidi ya mara tatu mpaka nne na tumepangiwa utaratibu wa kuwa kila wiki kila jimbo liende likachukue, tunapeleka watu wanafanyiwa *registration* lakini vitambulisho hawapewi. Kwa hivyo hili ni suala kubwa, kwa hivyo Mkurugenzi ajue kwamba haya ni mashaka na hii inatakiwa iende *mas-ul, answerable* ni Mkurugenzi. Mkurugenzi ambaye anashughulika na *Zan-ID* na Mkurugenzi wa *Votes ID,* hawa watu wawili ndio dhamana wa masuala haya, na tunataka kwa hayo tunayosema wachukue hatua za haraka kuwahakikishia watu wetu kuwa wanapata.

Kwa hivyo nataka niseme vile vile masuala haya ya vitambulisho Mhe. Naibu Spika, tumeanza kuyazungumza hapa katika Baraza la Wawakilishi kwamba watu wapewe haki zao, bado haki zao hawajapewa, masuala haya yamezungumzwa katika Baraza la Mapinduzi pia kusemwa kwamba watu hawajatimiziwa haki zao bado hatua hazijachukuliwa.

Lakini vile vile hawa watu wetu kama tutawakosesha hizi haki za kupata vitambulisho hatuoni kwamba huyu mwananchi tunamkosesha haki zake nyengine, mbali ya kuwa yeye hana kitambulisho chake yeye cha Mzanzibari Mkaazi, anatakiwa awe na *Vote ID* ili ajisajili na aweze kuwa mpiga kura, lakini masuala haya yanapigwa dane dane kila siku, hizi haki hazitolewi na sheria zipo zinazosema, kwa hivyo tunasema tunakwenda kinyume na yale ambayo tumeyapanga, kwa hivyo tunasema suala hili ni muhimu, watu wetu wameshindwa kupewa vitambulisho.

Kitambulisho hicho hicho kinamtaka yeye mwenyewe kimsaidie wakati wa kusafiri, kama hana kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi hawezi kupata tiketi, hichi hichi kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi kama anataka kuendelea kusoma masomo ya juu, kama hana hawezi kuendendelea, hichi hichi kitambulisho kama anataka kuweka pesa zake benki hawezi kuweka pesa benki kama hana kitambulisho. Hichi hichi kitambulisho kama ana mzigo wake anataka kutoa katika posta au katika benki hawezi kufanya jambo lolote kama hana kitambulisho.

Jamani kitambulisho cha Mzanzibari mkaazi ni muhimu sana, kama ikiwa kitambulisho hichi ni haki yake kwa nini asipewe, au tuambiwe leo katika Baraza lako Tukufu, atwambie huyu Waziri kwamba vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi si haki zao ni fursa, tujue kama ni fursa tusingepiga kelele tungeacha hivi hivi lakini tunasema kwamba kama kitambulisho cha Mzanzibari mkaazi ni haki yake, kila mtu ambaye ametimiza sifa na ametimiza masharti yote kuna sababu zipi anyimwe na hilo ndio liliopo, tusingepiga kelele hizi hatuna haja ya kusema maneno haya haya tunayasema kwa sababu ya usumbufu.

Kwa hivyo mimi naiomba Serikali ichukue hatua za haraka, kwa sababu muda tulionao ni mfupi sana, kwa sababu Mei haiko mbali, na hili Mhe. Naibu Spika, ni daftari la mwisho la kudumu la wapiga kura ambapo watu wetu wengi wanahitaji kupata *vote* za *ID* ili waweze kuwa wapiga kura, lakini kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi

hajapewa ina maana na *vote* za *ID* hapewi, na ikiwa hapewi hawezi kuwa mpiga kura, hawezi kujisajili katika daftari la kudumu la wapiga kura. Kwa hivyo tunakuombeni wanaohusika wote, haya tunayazungumza kwamba ni sheria na ni haki yao basi hii haki yao wapewe.

Mhe. Naibu Spika, kwa haya machache nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, ahsante *(Makofi)*

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kupeleka ombi langu la kuchangia na ukalikubali, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa leo kuendelea na shughuli zetu za kawaida za mambo yetu ya Baraza, pia nimshukuru mtoa hoja binafsi kwa kuleta hoja hii muhimu inayohusu vitambulisho vya Mzanzibari.

Mhe. Naibu Spika, miongoni mwa mambo muhimu kwa Mzanzibari ni kitambulisho hiki, kwa sababu kitambulisho hichi kinakusanya mambo kadhaa muhimu kwa mtu kuwa nacho, na kwa sababu kimewekwa katika sheria, kwa hivyo kila mtu anayestahili kuwa nacho ni vyema akawa nacho akapatiwa bila ya usumbufu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nimejiwekea utaratibu fulani katika Jimbo langu hasa karibu na bajeti, mara nyingi huwa kuna tashtiti katika jimbo langu huwa nazisikia kuzungumza na wafanyakazi kutafuta mafaniko yao na changamoto zao, kwa hivyo baadhi ya mambo ninayosema au mambo yote ninayosema huwa nasema kwa ushahidi fulani baada ya kuwapitia. Na ndio maana mwaka jana kuhusu kusahihisha mitihani ile nikawa mgumu kuwa walimu kutoka Pemba wananyimwa nafasi zile, ile nilipata baada ya kupitia walimu na wakanihakikishia kuwa jambo hili ni kweli na ni kweli Serikali ilikubali.

Mhe. Naibu Spika, mara hii wakati wa bajeti bado lakini niliwaita masheha wangu walio katika jimbo langu. Jimbo langu la Mtambile lina shehia saba, kwa hivyo niliwaita masheha wangu saba kuzungumza nao kuhusu kadhia hii ya vitambulisho vya Mzanzibari, na nashukuru sita walihudhuria, mmoja alikuwa na udhuru na tulizungumza vizuri nikawapa malalamiko ya watu, Masheha bwana watu wanaokuja kutaka barua ya kitambulisho cha Mzanzibari, hamuwapi mnawazunguusha, mara fomu ipo mara haipo, njoo kesho, keshokutwa. Nikawaambia mimi na nyinyi tulifanya kikao na Mhe. Waziri Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora, namuuliza kwa nini sikudai cheti, sikumtazama mtu, wakati anasema kweli, mumpe barua, lakini leo lile agizo la Waziri mumelikebehi, hamtoi.

Mhe. Naibu Spika, tulizungumza mwisho akanambia, ni kweli vilikuwepo lakini baadaye alikuja kiongozi mkubwa zaidi, akafanya mazungumzo na sisi, na kwa kuwa mtu wa mwisho aliyesema hivyo ni mkubwa kuliko huyu waziri, akatutaka kwamba ni lazima mtu tumuhoji, tumtake cheti cha kuzaliwa na mpaka awe katimiza muda ndio tumpe hiyo barua. Ndiyo maana ikawa lazima sisi tudai cheti. Nikamuuliza alikuja nani? Akasema Mhe. Makamu wa Pili, hakwenda kuwazuia kuwa wasitoe, aliwataka wao lazima kwanza wadai cheti.

Mhe. Naibu Spika, mimi niliwaambia Waziri na Makamu wa Pili Makamu wa Pili ni mkubwa, nikamuuliza jee, ni kweli amewaambia kweli, akanambia naam. Mtu tumuhoji asiyekuwa na cheti kinyume na alivyokuwa akisema Waziri. Kwa hivyo hichi ni kikao nilichofanya na masheha wangu, tukazungumza vizuri tu, na majibu yao yalikuwa ya aina hiyo.

Mhe. Naibu Spika, lakini kwa hali yoyote ile, kitambulisho cha Mzanzibari ni haki ya kila Mzanzibari aliyetimiza masharti ya kisheria. Kwa kuwa mtu masharti ya kisheria kayatimiza, kwa nini tena haki hii aikose.

Na hawa ambao tayari wamesajiliwa danadana iliyokuwepo ya njoo, nenda, rudi, rudi, hawapewi. Muda tulioambiwa wa kisheria au wa kikanuni ni wiki mbili. Watu wanakwenda hata zaidi ya miezi miwili, mitatu hawapewi, hivyo vilivyokuwepo na mara nyengine wanaambiwa tayari tumeshavirudisha Unguja.

Mhe. Naibu Spika, mara moja nilipokuwa katika Kamati ya Viongozi Wakuu tulikwenda Pemba kule Kaskazini kulikuwa kuna hoteli inajengwa. Kwanza ule uongozi wa hoteli ulituzuia kuingia ndani, lakini kwa sababu Mwenyekiti wangu ni mahiri sana, alipapatua mpaka tukaruhusiwa kuingia kwenye hoteli ile. Tukawahoji wahoji wafanyakazi, tukamkutia mtu mmoja lafudhi yake ya kuzungumza ni ya Kikenya kama anaonesha kuwa ni raia wa Kenya. Tukamuhoji bahati mbaya alikaa kimya, tukamuuliza kitambulisho cha Mzanzibari alikuwa anacho. Mimi na Mwenyekiti wangu tukatoleana macho, pwaa, pwaa pwaa.(*Makofi)*

Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Viongozi Wakuu kwa siku hizo alikuwa Mhe. Hamza Hassan Juma. Hatukumnyang'anya kwa sababu hatuna wajibu huo, lakini kitambulisho hicho cha Mzanzibari mtu ambaye sio Mzanzibari wala sio Mtanzania, hata awe Mtanzania lakini sio Mzanzibari, alikuwa anacho. Kwa hivyo, vitambulisho mara nyengine wanapewa wasio husika, *why*? Apewe asiyehusika mtoto aliyekuwepo Makombeni awe hana haki, awe na haki anayetoka Mombasa au kwengine kokote huko nje ya nchi.

Mhe. Naibu Spika, mimi haya siyabuni, nasema yaliyotokea, na kama tunakwenda hivyo, tunawanyima watu haki zao za Kikatiba, haki zao za kisheria kwa matakwa yetu ya kibinafsi.

Iko siku sisi tulio hapa tutaondoka, tukiondoka Mheshimiwa tuna kazi kubwa, sote sisi kuwepo hapa tumekubali kuwa ni viongozi. Ukikubali uongozi ni kuwatimizia tunaowaongoza haki zao. *Wallahi* tutakwenda kuhojiwa, la kujibu hatuna, kwa sababu siku hiyo mdomo utazuiwa, na viungo vyengine ndivyo vitakavyosema. Tunakwenda kusema nini? Watu wana haki zao hatuwapi kabisa, kabisa, kabisa! kwa nini?

Mhe. Naibu Spika, ningeiomba serikali inayojiita kuwa ni sikivu, kama ni sikivu ningeliomba tatizo hili mlitatue. Ikiwa halikutatuliwa itakuwa sio sikivu, ikiwa ni dai letu la kusimamia kuwa serikali yetu ni sikivu, inasimamia matakwa ya wananchi, haimdhulumu mtu. Kama haimdhulumu mtu ningewaomba hawa ambao vitambulisho ni haki yao, na hivyo vyeti vinavyotakiwa vya kuzaliwa wanavyo, waliokuwa hawana waachieni mbali, tuseme hawana vyeti hata kama mtu ana umri kama wangu mwambieni kama huna cheti hatukupi. Lakini mwanangu ambaye cheti anacho kwa nini hamumpi, *why*?

Mhe. Naibu Spika, wale ambao wanastahiki serikali nawaomba mumpe. Tunasema serikali hii ni tulivu, iko kwa niaba ya wananchi na ni kweli ipo kwa niaba ya wananchi, hata kwa wananchi mara nyengine tunawanyima haki zao. Lakini ipo kwa sababu tumeichagua, kwa hivyo chaguo letu lisitudhuru.
Wengi waliotangulia kusema tumesema kuwa kitambulisho ni ushahidi. Kwanza kinaonesha kuwa wewe ni mkaazi wa Zanzibar, halafu ni petu sio mkaazi tu.

Pia ni ushahidi kuwa unapotaka huduma unadaiwa kitambulisho. Kuna mtu kafanya matatizo unakwenda kumchukulia dhamana polisi, hachukui dhamana kama huna kitambulisho cha Mzanzibari. Ukifanya uhalifu ukidaiwa kitambulisho cha Mzanzibari kama huna peke yake hilo tu ni kosa.

Mhe. Naibu Spika, tumeweka sheria kama huna kitambulisho ni kosa, sisi serikali tunamfanya raia wetu awe ana kosa ambalo mwenyewe alivyo awe hana kosa, halafu unasema unamsimamia, unamsimamia nini? Kitu chenyewe tumesema lazima uwe nacho, kaja kukiomba humpi, halafu anafika pahala anakutwa na tatizo anadaiwa kitambulisho hana, anaingia hatiani, jee, kosa alilolifanya ni lake lakini hili la pili lililokuwa hana kitambulisho limesababishwa na serikali iliyopo.

Mhe. Naibu Spika, ningeiomba serikali jamani yale ambayo sio lazima kuwa hilo ni tatizo, tusilifanye kuwa ni tatizo. Jambo ambalo si tatizo, kwa nini tufanye kuwa ni tatizo? Hivi sasa tuko na mifumo ya kijinga jinga, *don't trouble the trouble unless the trouble troubles you*. Usitafute ugomvi acha ugomvi ukutafute.

Mhe. Naibu Spika, ningeiomba serikali hawa ni Wazanzibari, ni raia wa Zanzibar, hii ni haki yao. Ningewaomba mimi kwa unyenyekevu kabisa, kila mwenye haki hii aliyetimiza masharti, jamani apewe. Na vile ambavyo vipo tayari, serikali inadai kwamba watu hawachukui.

Mhe. Naibu Spika, *wallahi* watu wanakwenda hawapewi, sio kama hawachukui. Wengine wanakwenda kwa sisi tuliopo Pemba wanaambiwa kwamba vimeshapelekwa Unguja, sijui hawa wa Unguja wanaambiwa vipi. Kwa sababu vya Unguja haviwezi kwenda Pemba, lakini vya Pemba vinaweza vikaletwa Unguja. Kwa hivyo tujitahidini, jambo ambalo sio lazima liwe tatizo, tusilifanye tatizo.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante nakushukuru, sasa nafasi nampa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, baadaye Mhe. Saleh Nassor na kama muda utabaki Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Naibu Spika, na mimi nianze kuwaeleza machache ambayo ninayoyajua mimi.

Mheshimiwa mimi naomba sana Waheshimiwa wenzangu tusiwe na jazba katika kutoa hoja kama hizi. Ni kweli kuwa panapo haki itafutwe kwa mujibu wa sheria ya kutafuta haki.

Mhe. Naibu Spika, mimi nijitolee mfano mdogo tu. Mimi nilikuwa nakaa Kwahani na sasa nimehamia Fuoni. Familia yangu yote imechukua barua rasmi kwa Sheha na kupeleka kwa Sheha wa Fuoni, lakini mimi mwenyewe sijachukua kwa sababu bado sijaamua, nina upenzi wa Kwahani. Sikuwa na hamu ya kutaka chochote wala sikuchukua chochote pale, kwa sababu bado sheria haijanipa, nayo hii sheria tuiangalie.

Mhe. Naibu Spika, unapotaka kwenda pahali, tatizo liko wapi, kwa nini usichukue barua ya Sheha wako, ni tatizo dogo tu wala sio kubwa. Mimi nafikiria tunashindwa kuwaelimisha wananchi wetu, Hili somo la kuwapa wananchi wetu hapo ndio tunaposhindwa. Kwa nini iwe hivyo, sheria ipo wazi.

Mhe. Naibu Spika, nakumbuka mnamo mwaka 2005 au 2006 nilikuwepo Pemba kwenye Kamati, waliambiwa watu wasiende kujiandikisha, huu ukaazi wetu wa Zanzibar, waliambiwa watu wasiende kujiandikisha kabisa, lakini baadaye watu wakaelimika.

Sasa hebu tizama huku waliambiwa wasiende kuchukua, wasijiandikishe, lakini baadaye watu wakaelimika kujua hichi kitu kumbe kina umuhimu. Sio kosa, na ndio inavyotakiwa. Sasa na sisi tuwaelimishe wananchi utaratibu wa kukipata kitambulisho, inaweza ikawa ni halali lakini kumbe uhalali wako una dosari. Watu wametoa *documents* hapa na kila kitu, na mimi natoa *documents* zangu nakuonesha.

Mhe. Naibu Spika, niliwahi kusema siku nyingi sana mimi hapa, siku moja nilikuwa nasema habari ya vitambulisho wamepewa nani, wamepewa nani. Kwanza niwashukuru sana Mkurugenzi na watendaji wake, wameifanya kazi, waliokuwa hawahusiki wote wamenyang'anywa. Hilo nampongeza sana kwa sababu binadamu hana mikono mirefu isipokuwa mikono yake ya kuchangiwa, akisikia habari anafuatilia wanafanya kazi, tena wanafanya kazi *serious* kabisa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo siku ya pili nikampata kijana mmoja, tena naomba hata serikali inisaidie nimeingia niseme hatiani, lakini wanisamehe kwa kutokujua.

Kijana yule alinijia rasmi, akanambia ni mimi mmoja nanyimwa kitambulisho na Ofisi itakuwa shahidi. Nikamchukua yule mtu mguu kwa mguu. Tumekwenda zetu mpaka kunakohusika. Halafu leo watu mnakula madua makubwa makubwa, mnatutia, tizameni sasa madua yenu yanavyoangamiza, tusiombe madua. Mimi siku zote nasema jamani tusitoe madua makubwa, ndani ya roho hatujui undani wake ukoje, tumuogope Mwenyezi Mungu vile vile.

Mhe. Naibu Spika, pande zote tumuogope Mwenyezi Mungu, usione huku na huku ukamuona mwenzako anakwenda vizuri.

Mheshimiwa nilipofika pale yule mtu kutaja jina picha kataka kajiandikisha mara mbili. Mimi uso kwaa, shahidi mwenyewe muhusika, watu wanakwenda na mtandao bwana. Kaenda kataja jina tofauti, alilotoka nalo Pemba jengine na alilokuja nalo hapa la Magomeni jengine. Mimi nikamwambia kama sheria kwanza niachieni nitoke na mtu wangu. *Wallahi* nikawaambia naomba radhi, niachieni nitoke na mtu wangu niende naye nje tena mtajua nyinyi wenyewe hapo baadaye.

Mhe. Naibu Spika, yule alinambia Mheshimiwa nihifadhi ndani ya gari yako mpaka nifike halafu niachie mbele ya safari. *Wallahi* nikamuachia mbele ya safari, kumbe ni kosa nalo hilo na mimi nikawa nimeshiriki. Niseme ukweli kwa sababu yule mtu alikuja akanililia ananambia haki yake anaitaka. Lakini mwisho nikauliza nyinyi mnafanya jambo hili kwa taratibu gani, ili mtu akitaka ile haki aipate. Wakasema sisi huwa tunatoa fomu za malalamiko, halafu tunakaa jopo kwa mujibu wa sheria. Halafu tunaangalia kuna wengine wanakuwa wadanganyifu.

Mhe. Naibu Spika, wale ni watu wapekuzi ni sawa sawa *x-ray,* ni sawa sawa na *CT- Scan,* kwa sababu hawaridhiki, ukiwaambia tu kwamba mimi nakaa Wete wakati wewe umo ndani ya Unguja. Unasema Fuoni kumbe wewe uko *original* Fuoni kumbe sio Wete.

Sasa mimi nafikiria hili, ndio maana nikasema kwamba tusiwe na jazba. Jazba haitufikishi mbali, twende na utaratibu, tutafute sheria zilivyo, tuweke sawa.

Mhe. Naibu Spika, wakisha kukaa wale wanatizama, tupe vyeti vyako, unatoa vyeti. Mheshimiwa naomba nitoe cheti cha mfano hapa. Juzi Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria alisema ukweli kwamba kuna watu, kakiri kwamba kuna vyeti feki vinatolewa. Sasa leo tizameni watu wanavyokula halbadiri zao, si vizuri.

Mhe. Naibu Spika, hapa kuna bwana Ali Khamis Tupa, huyu wa Kichanjani Ole Wete Pemba. Hii ni *certificate* ya kuzaliwa kabisa, lakini kuna cheti ambacho *serial number* ya huyu bwana Ali aliyekuwa *original* ya kuzaliwa ambaye amepewa mtu kutoka Kojani. Halafu mseme ni sheria halisi, huyu *serial number* 1/698/91 lakini huyu mwenye *original* ambaye yeye hati yake ni ile ile *stroke* hiyo hiyo, ina maana kumetoka vyeti namba ya mtu imechukuliwa ya cheti cha mtu mwengine, *serial number* nyengine. Sasa ndio maana tukasema tusitafute mambo.

Lakini nina mwengine kumbe huko nyuma alikuwa keshafanya cheti, sijui kakitupa. Lakini hajakitupa, kwa sababu alipokwenda kaenda kafanya cheti chengine. Kwenda kule akakutwa ana vyeti viwili, alipohojiwa kwenye lile jopo akakutwa ana vyeti viwili. Jamani mimi nafikiri Wawakilishi tuwe walimu kwa kuelimisha. Sheria tunaichezea wenyewe, tusije hapa tukawa wakali, mimi mumeniona nimekuwa *polite* kabisa, kwa sababu nataka tuelimishane kisheria, twende taratibu.

Unaambiwa unapotaka kwenda kwa Sheha zisifike siku thalathini. Nalo hilo tuna ujeuri huo tuseme ukweli. Kwa nini unaona tabu kwenda kumwambia Sheha mimi jina langu fulani bin fulani, nimekuja hapa natoka mahali fulani, barua yangu mimi hii hapa kwa Sheha wangu. Kwa sababu siku hizi lazima tufanye hivyo, tukitaka tusitake, kwa sababu kuna mambo mengi yanaingia humu, watu wanakuja kufanya uhuni, watu wanakuja kufanya nini. Mtu anafanya makosa mbali anakuja kujificha mahali mbali, kwa nini sasa usijulishe.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba sana hili suala tunapotaka kulifanya hapa, lazima tuwe wakweli na sisi kwa upande wetu. Kwa sababu nimefanya ziara siku zile hapa nilitoka na Mhe. Dokta Mwinyihaji. Leo nina vitambulisho ndani ya jimbo langu, mpaka leo hii wenyewe hawajulikani. Hebu nambieni tangu 16/11/2010, mpaka leo vipo, hivi tuseme vimetokea wapi. Maana yake mambo mengine tujiulize, ndio maana tukasema kuwa. Nimekwenda mwenyewe *physically* nimeviona, tatizo na ufuatiliaji wetu unakuwa mfupi.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninachowaomba wenzangu tukakamaa, tukapigana madua, eeh! Mwenyezi Mungu baba, anamuona kila mtu, kila nafsi ya mtu anaijua. Usioneshe ulimwengu kama wewe umetakasika katika dua na kufanya nani aah! *Yarabi* Mwenyezi Mungu, tustaghfiru kwa Mungu wetu jamani, hatari hii. Wewe unajidai kumuombea dua mbaya kumbe mwenyewe una uso mwengine, *laillaha illa allah*, *innaa lillaahi wainnaa ilayhi raajiun*.

Mimi ninachoomba jamani dhima tutaibeba sote hili mulielewe, usimnyoshee kidole Makamu wa Pili, usimnyoshee kidole Mshimba, usimnyoshee na mwengine, sote tutaibeba dhima hatoki mtu hapa. Lakini leo tumekuwa sisi wakali kwa jambo hili dogo tu. Maana mimi ninashangaa kwa mujibu wa ninavyoifahamu sheria ilikuwa leo Serikali hii sisi tupo pamoja hapa ilisema *okay fine* basi tutajirekebisha mchezo umeisha. Mimi sioni kama kuna hoja nzito ya kufika watu kukaripiana hapa, mimi sioni hoja nzito.

Mhe. Naibu Spika, mimi sioni kama hoja nzito hapa, isipokuwa kuna marekebisho ambayo tunayarekebisha kwa jamii. Mheshimiwa pale alikiri, kweli *certificates* zipo ambazo za *fake* hizi hapa zipo kibao, tena nyingi sana kwa kweli Mheshimiwa na zote zinatokea upande wa huko unakuja zake huku, ee ndivyo ilivyo.

Mimi ninafikiria Mheshimiwa niombe sana wenzangu, tusilichukue hili kama ni janga la kutaka kufarakana, tusichukue suala hili la kufika pahali tukataka hoja za kujibizana, twendeni katika utaratibu wa sheria, tutafuteni ufumbuzi, tuangalie koseo liko wapi.

Leo mimi haiwezekani mwananchi wangu atake kuja pahali nishindwe kumfahamisha kumwambia wewe unatoka Kitope unakwenda Jang'ombe lakini halalisha kwa Sheha wako, kwani kuna tatizo gani kuchukua barua

ukampelekea Sheha, tatizo liko wapi, hapa ndio ugumu, tatizo liko wapi? Mimi sidhani kama Sheha ukimwambia hasa bwana wee mimi natoka Kwahani kwenda Jang'ombe Sheha akakataa, jamani masheha wetu hawana ujinga huo hata siku moja. Unapochukua barua ile ukaenda kule na kule kuna sheria zake, atakupokea, ataku-*register* atakwambia kaka pumua sasa, tatizo liko wapi sasa hapo. Lakini utalazimisha sheria lazima unavyotaka wewe, wewe utoke huko uje moja kwa moja ukachukue kitambulisho, nani atakupa namna hiyo, hakuna hiyo!

Hiyo jamani hata Ulaya haifanyiki namna hiyo. Hakuna Ulaya utaratibu huo, uende leo ukapewe leo leo hata hao wanaondoka wakaenda huko basi wanachukua muda au wanakwenda mahkamani mpaka inafika pahali kesi zinahukumiwa kwenye mahkama, muda wote na tena uwe na *strong reason* ya kufanya jambo lile hata upate uhalali wa ukaazi, itakuwa sisi Zanzibar tumekuwa uchuro.

Mhe. Naibu Spika, mimi niwaombe sana jamani tusiwe na jazba, Mwenyezi Mungu atulinde, Mwenyezi Mungu atuhifadhi, hayo ni mambo ambayo tunatakiwa waislamu tujiombee. Tunaambiwa waislamu kila mara tukumbuke mauti, tunaambiwa kila mara tumdhikiri Mtume Muhammad *Salallahu Alayhi Wasallam,* hayo ndio mambo ambayo tunayotakiwa. Lakini sio leo hapa tuseme tumnyooshee kidole huyu, huyu kafanya hivi, hawa watu wa vitambulisho wanafanya jambo la ukweli. Tena wamesaidia katika mambo makubwa sana, wamegundua mambo mengi hawawezi kusema ni hatari wakija wakiyasema, wakisema *real* na nini tutafungwa wengi, aibu si mchezo, watatufunga jamani, hebu tuwe *cool down,* twendeni kidogo kodogo.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache, mwenzangu alisema sheria, sheria, sheria unaitizama shilingi upande mmoja wa sheria lakini hatari kwa upande mwengine. Yarabi Mwenyezi Mungu atujaalie kwa usalama salimini. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia fursa hii. Kwanza nikushukuru kwa kunipatia fursa, pili napenda kutoa pole kwa marehemu pamoja na wale majeruhi ambao walifariki pamoja na kupata maumivu makali na vilema, pale ambapo jana wakati wanarudi katika mkutano wa hadhara kule Makunduchi baada ya kushambuliwa vibaya sana na majanjawiri na hatimaye wengine kupoteza maisha na wengine kujeruhiwa vibaya. Kwa hivyo, kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Wawi, na wananchi kwa ujumla wapenda amani wa nchi hiii, napenda kutoa pole kwa familia, Chama cha Mapinduzi, pamoja na wananchi wote katika nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, mimi mwaka 1977 wakati tunaunganisha Afro Shirazi na Tanu pale walinambia wazee wangu pale kwamba chukua kadi ya CCM, mimi nikawaambia nataka niangalie miaka kumi kwanza. Kina Mzee Ali Haji Pandu, bwana Mloo walinishauri sana kwamba nichukue kadi ya Chama cha Mapinduzi nikaacha kuchukua, niliangalia imani ya Chama cha Mapinduzi huku nyuma waliandika katika kadi yao kwamba CCM inaamini mambo matatu.

Kwanza binadamu wote ni sawa, kila mtu anastahiki heshima na kutambuliwa utu wake, na tatu kwamba ujamaa na kujitegemea ndio njia pekee ya kujenga jamii ya watu walio huru na sawa. Nikaanza hii namba tatu kukataa ya ujamaa na kujitegemea.Nilikataa Chama cha Mapinduzi pale. Halafu namba mbili nikataka kujua usawa wa binadamu ni miaka 10 nipime huu usawa wa binadamu ndani ya nchi, Chama cha Mapinduzi watasimamia vipi usawa wa binadamu. Hatima yake haikufika miaka 10 wale walionishauri wengine wakapelekwa jela kina Mzee Mloo wakafukuzwa kwenye Chama cha Mapinduzi wakapata mashaka chungu nzima, ndio mpaka sasa mimi sikuwa mwanachama wa Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Spika, sasa niende kwenye hoja baada ya dibaji hiyo. *Zan-ID* ni kitu muhimu sana katika nchi hii, ni haki ya kikatiba kwa mujibu wa hoja ya Mhe. Hamad Masoud, ni haki ya kikatiba ya Mzanzibari aliyetimiza masharti. Inasikitisha sana kwamba *Zan-ID* ni mtaji wa kisiasa wa Chama cha Mapinduzi, inasikitisha, tena dhambi kubwa sana kwa mujibu wa Mwalimu Julius Nyerere alisema dhambi ya ubaguzi ni mbaya sana.

Ukianza kuwabagua Watanzania katika misingi ya jiografia, Mpemba, Muunguja, Mzanzibari, Mtanganyika humalizii hapo unakwenda zaidi Mheshimiwa. Inasikitisha sana, sana, sana, kuona haki hii ya *Zan-ID* ambayo ndio kila kitu kitambulisho cha uzanzibari mkaazi katika nchi hii, ndio kila kitu Mheshimiwa. Ili usome, mtoto apate elimu hawezi kupata mkopo kama hajapeleka *Zan-ID* akapata mkopo wa elimu ya juu. Huwezi kupata ajira kama hujapeleka kitambulisho cha *Zan-ID* Mhe. Naibu Spika. Baya zaidi hata biashara kama hujapeleka kitambulisho cha *Zan-ID* hupati leseni ya biashara, leo huu unatumika mtaji wa kisiasa.

Mheshimiwa huwezi kuzima moto kwa kutumia petroli siku zote kabisa kabisa, kama moto unawaka ukamwage petroli uzime unazidisha. Mimi ninaamini kuna siku Chama cha Mapinduzi mtafahamu, ikiwa Skyrim Botha Afrika Kusini ameshindwa kupambana na wimbi la mabadiliko, basi naamini siku moja na nyinyi mtafahamu kwamba binadamu wote ni sawa, na kila mtu anastahiki heshima na kutambuliwa utu wake.

Utaratibu

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa tunachojadili hapa ni hoja binafsi ambayo inataka haki ya mzanzibari na wala hatukijadili Chama cha Mapinduzi, kinachozungumzwa hapa ni aina ambayo *Zan-ID* itakavyotoka na kuilazimisha Serikali kupata mambo ambayo mleta hoja amekusudia. Hivyo, naomba muongozo wako kwa sababu afute kauli ya kuwa Chama cha Mapinduzi ndio mtaji, hatujadili Chama cha Mapinduzi tunachojadili ni *Zan-ID*.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante, Mhe. Saleh tunajadili hoja ya vitambulisho vya Mzanzibari Chama cha Mapinduzi hakihusiki. Tukianza Chama cha CUF, Chadema, CCM tutatoka kwenye hoja, nakuomba sana twende kwenye hoja tuimalize hii hoja, ninakusihi sana. Kwa hivyo endelea na hoja.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru sana na mimi ninakuheshimu sana. Mhe. Naibu Spika, ninakuheshimu sana, sana, sana na naendelea na hoja. Tunasema kwamba *Zan ID* inatoka katika misingi ya ubaguzi wa kijiografia, inatoka katika misingi ya ubaguzi ya upemba na uunguja pamoja na ubaguzi wa kisiasa.

Kwa mfano Mheshimiwa kuna wazanzibari ambao wameshatimiza masharti yote ya kupata *Zan-ID*. Mimi binafsi kuna Sheha wa Matale, kuna vijana 27 aliwaahidi kuwa siku ya Jumatatu katika mwezi uliopita waende kuchukua barua za kuchukua *Zan-ID*. La kusikitisha Sheha wa Matale aliwaacha pale mpaka saa tano hajaja, saa sita hajaja mpaka saa kumi Ofisi inafungwa yeye hajaja. Nikampigia simu mimi akanambia hayo masuala hayo huwezi kunilazimisha sijui wakawatoa Matale hadi pale Ofisi ya Vitambulisho Chake Chake. Huo ni udhalilishaji mkubwa, na kwa kweli Mhe. Naibu Spika, kwa hali hii basi ni tatizo, unapomnyima mtu *Zan-ID* umemnyima ajira, umemnyima elimu, umemnyima kazi; kila kitu umemnyima. Watoto wa kizanzibari sasa hivi wananyimwa kila kitu.

Mhe. Naibu Spika, mimi katika jimbo langu la Wawi katika shehia tatu karibu watu 280 takriban wametimiza kila kitu na hawajapata *Zan-ID,* nimehangaika nao kwa masheha nimehangaika nao mpaka sasa nimebakia tu hivi, haya tuache hiyo. Kuna watu ambao wana *certificates* zile za kupata *Zan-ID* zile risiti. Kwa sababu kabla ya kupata *Zan-ID* ukishatimiza sifa unapewa risiti. Mimi ninao vijana 80 katika shehia tatu za Jimbo la Wawi hawajapata na risiti wanazo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa watu ambao wanazo *Zan-ID* zimepitiwa sasa na muda zinataka kubadilishwa, walikuwa nazo nyuma wamekwenda Ofisi pale wakazi-*surrender* zile na hadi leo huu ni mwezi wa sita hawajapata *Zan-ID* hilo ni tatizo. Tukisema kwamba zinatumika kisiasa tujue ni tatizo.

Mhe.Naibu Spika, inasikitisha sana kuona kwamba hapa jana tulikuwa na hoja ya kuibiwa nyaraka. Eti tunamsema Hamoud kaja Ofisi ya Ubalozi mgeni na nini kachukua nyaraka muhimu tu za nchi. Leo sisi wageni tunawakaribisha, wamakonde kutoka Nampula wanapewa *Zan-ID*. Wamakonde kutoka Msumbiji wanapewa *Zan-ID* kusudi ni mtaji wa kisiasa waweze kupiga kura katika uchaguzi unaokuja. Sasa huyu ushampa *Zan-ID* mtoto huyu anaenda anasoma, anachukua digrii ya mwanzo, digrii ya pili unampa Ofisi nyeti ya nchi, tunakuja kumlaumu kwamba Humoud katoka Muscat kaja hapa kutuchulia nyaraka, tunawapandikiza wenyewe.

Sisi Mapinduzi ya 1964 haikuwa lengo lake kunufaisha wageni, lengo la Mapinduzi ya 1964 ilikuwa tufaidie sisi wazanzibari. Leo wamasai wana *Za- ID* Mpemba wa Umangani, mpemba wa Ole hana anakuonesha hapa mmasai wewe unashindwa kupata. Hivyo mnatubagua na dhambi ya ubaguzi ni kubwa, ikiwa leo mnatubagua wapemba hatupati *Zan-ID* hizi hapa, haya ma-*document* hivi ni vyeti.

Mhe. Mshimba amesema kwamba vyeti hivi ni feki, kuna vyeti feki vina muhuri wa Serikali? nembo ya Serikali? Haya mshamba wa Vitongoji kama mimi nitaipata wapi hii, si huko huko Serikalini mmetupa sisi. Sasa kama ni ujinga ni ujinga wa Serikali sio wetu sisi, msitunyime haki zetu kwamba eti hizi ni feki. Mimi nashangaa sana yeye huyo ndiye aliyesema kwamba kuna mwaka jana yeye Mhe. Mshimba kasema kuna wamakonde wanapewa leo

anageuza, ndio nikakataa kwenye Chama cha Mapinduzi mimi inasikitisha sana. Lakini wimbi la mabadiliko Mheshimiwa haliepukiki, hakuna anayeweza kupambana na wakati, *wakati ni ukuta,* wale wanasiasa waliokuwa hawajui ninawaambia *wakati ni ukuta*, na mkipambana nao basi mtaumia wenyewe.

Ninawaombeni sana sana Waheshimiwa kwa kweli mnatupa tatizo, haki yetu ya msingi hamtupi kwa sababu wengine ni Wapemba, kwa sababu wengine ni CUF, hawa ninaowataja kwa mfano Jimbo la Amani hivi vyeti hivi *registered* kwa sababu tu wanatoka Pemba hawakupewa, huo ndio ubaguzi alioukataa mwalimu Nyerere, leo nyinyi mnauendeleza kweli nyinyi ni CCM ambao mnaamini kweli kwamba Muasisi wa Chama Kile Mzee Nyerere alikataa ubaguzi, msitubague, msijidanganye Chama cha Mapinduzi kwamba nyinyi ndio peke yenu mliofanya mapinduzi ata hasa na sisi CUF wanamapinduzi kuliko nyinyi wengine kabisa kabisa.

Huko CCM kuna mahizbu tunawajua, kuna ma-ZPPP tunawajua, na Afro Shirazi tunawajua. Sisi Pemba Afro Shirazi wengi huku mnatunyima haki zetu za msingi, damu za wazee wetu, walipoteza damu zao wazee wetu. Na tija ya damu za wazee wetu hatuipati mnawapa wamakonde, mnawapa wamasai na Mwenyezi Mungu atatulipia *inshaallah*.

Naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi hii mchana huu kuchangia. Lakini kwanza awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema sote katika Baraza lako hili Tukufu mchana huu.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuchangia hoja binafsi ya Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi Jimbo la Ole chini ya kanuni ya 27 kifungu 3, 48(2), 49(1), 50(2), ya kanuni ya Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2012. Kuitaka Serikali kuchukua za kuwatimizia wazanzibari wote waliotimiza sifa za kisheria, haki ya kuwapatia vitambulisho vya mzanzibari mkaazi *Zan-ID*.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme Serikali ina nia njema na ina azma nzuri kwa wananchi wake wote kupata hivi vitambulisho vya *Zan- ID*. Mhe. Naibu Spika, mimi sina wasiwasi kwa hili kabisa, na nasema hivi kwa nia safi na Mwenyezi Mungu shahidi anaona kwa upande wa jimbo langu la Bububu hali ninaijua vilivyo, jinsi ya vitambulisho vya Mzanzibari wananchi wanavyovipata wanavyohangaika na wanavyovipata kwa zile sifa ambazo za kutimiza. Nitazungumza baadhi ya sifa ambazo nimeziona binafsi kabisa uhalisia wake na wananchi kwa nini wakawa hawapati na wengine wakawa wana sifa wanapata.

Kwanza niwapongeze masheha wangu wote. Masheha wa Bububu, Sheha wa Mwanyanya, Sheha wa Sharifumsa kwa kazi yao nzuri na kwa jitihada zao kubwa na kwa mashirikiano baina ya mimi pia na wao kiuwezo wa kifedha au kwa mambo yote ya mahitaji, kuhakikisha wale wananchi kupata yale mahitaji ambayo na sifa zile kupeleka kule kwenye vigezo, ambapo wapatiwe zile *Zan-ID*. Kwa hili nawapongeza sana masheha wangu hao kwa juhudi zao kubwa.

Mhe. Naibu Spika, Wazanzibari wote wapewe bila ya ubaguzi, lakini niseme suala moja lazima tutimize vigezo na zile sifa ambazo zimewekwa katika kutimiza ambapo huwezi kupata hiyo *Zan-ID*. Lakini wengine kwa hali niliyopitia na nikaiona, wengine uwezo hata vile vyeti vya kuzaliwa hawana, na vyeti vile mpaka leo wengine hawana na wapo jimboni kwangu.

Mhe. Naibu Spika, kuna baadhi mimi mpaka fedha nimewasaidia wakatafute vyeti vya kuzaliwa, kwanza kuonesha uhalisia wao wa kuzaliwa wapi. Hiyo hali nimeiona na nimehakikisha mwenyewe kwa hali moja kwamba wananchi wanapata tabu kwa ajili ya vyeti.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine tatizo linaloonekana pale changamoto kubwa kuna wananchi wanatoka Kisiwa chetu cha Pemba ndugu zetu wanakuja kuhamia Jimbo la Bububu, lakini unakuta wanakuja pale ndani ya miezi miwili au mitatu wanataka wapate vitambulisho hivyo na sheria haikubali. Sasa nasema suala kama hili utalichukulia vipi, tuwe wazi na tuwe wakweli, wewe utoke eneo hili uende eneo jengine ukitaka kuandikishwa itawezekana vipi.

Mimi nasema jambo hili tuliwekeni wazi Waheshimiwa Wajumbe, tusiseme uongo, kuna watu wakitimiza sifa, mimi mwenyewe nimeshachukua hatua hizo binafsi kwa kuwasaidia siangalii chama, siangalii mfuasi wa chama gani, muhimu ile haki yake aipate yule mwananchi.

Mhe. Naibu Spika, kuna vitambulisho niseme mpaka leo hii havijachukuliwa, vipo, wenyewe wameomba lakini hawajavichukua, sijui kwa nini hilo suala tumeshaambiwa sisi tuwafuatilie hawa vitambulisho vyao. Kwa sababu uchaguzi unakuja mbele Mhe. Naibu Spika, na kama kitambulisho kile huna huwezi kujiandikisha utakuwa huna sifa ya kupiga kura, na uchaguzi unapokuja hawa wananchi watachagua kiongozi gani wanayemtaka bila ya kulazimishwa, ni hiyari yao wataangalia nani anaweza kutusaidia kuteletea maendeleo katika nchi yetu ili waweze kumchagua.

Kwa hiyo, mimi sioni sababu yoyote kwa yule mwananchi asipewe kitambulisho, hiyo haki yake ya msingi, na serikali imesema mwanzo ina nia njema ya kuwasaidia wananchi wake, kwa nia safi na nia thabiti kabisa si ya kubabaisha.

Mhe. Naibu Spika, kwa hiyo niseme suala moja muhimu sana nieleze wazi kabisa kwamba tuwaambie wananchi ukweli, jambo zuri liwe la uzuri, jambo la uongo liwe la uongo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nina basi langu la wanafunzi, na lile basi Darajani sasa hivi lipo lile basi wanapanda watoto ambao wao wenyewe wazee wao ni CUF tunawajua, na wengine ni CCM, lakini lini tumefanya ubaguzi huo wa kusema watoto wa CUF humu washuke, lini? Kama Mjumbe aliyepita alivyosema hicho kitu hakipo Mhe. Naibu Spika tunafanya kwa nia njema, kwa ajili ya watoto wetu wale wasome ili waje kuongoza nchi hii waweze kwenda skuli, na mnajua nyote wajumbe tatizo la njia ya Bububu usafiri ni mgumu sana, wale wanafunzi wanapata tabu sana utasikia masikitiko makubwa ukiwaona wanavyohangaika jioni. Lakini hakuna ubaguzi wa kusema huyu mtoto labda ana kadi ya CUF au ya CCM, hicho kitu hakipo Mheshimiwa. Kwa nia njema ya serikali imesema mwanzo, na sisi tunaendeleza ile nia ya serikali, ya kuwalinda watoto wale kupata ile huduma bila ya kuangalia itikadi zao.

Mhe. Naibu Spika, pia kuna jengine jambo muhimu sana. Leo alikuja mwananchi mmoja ana shida, na mwananchi yule anatoka Kisiwa cha Pemba lakini anakaa kwenye Jimbo langu la Bububu. Akaniambia nilikwenda jimboni mimi pale lakini kusema mimi ninaogopa, nikamwambia unaogopa? Ni leo asubuhi sio jana, leo asubuhi kabla ya kuja Barazani nazungumza naye.

Alikuja nyumbani kwangu kunifuata nikazungumza naye kama dakika kumi na tano, nikamwambia una shida gani kwani ungeenda jimboni kwa sababu kuna mtendaji wangu jimboni pale yupo anasaidia mambo ya shughuli mimi niko kwenye Baraza. Akaniambia nimekwenda pale Mheshimiwa lakini naogopa kusema, nikamwambia unaogopa kusema nini? Akasema mimi sina kadi ya CCM, anasema yule mwananchi nikamwambia wewe kadi ya CCM kwa nini huna, akasema ah mimi sina kadi. Nikamwambia sawa, huna kadi ya CUF, akasema sina, nikamwambia Mhe. Naibu Spika hiki kitu ni cha kweli, nikamwambia tafuta kadi mbili uwe nazo mfukoni, ukija kwangu onesha kadi ya CCM, ukienda kwa CUF onesha kadi ya CUF. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nakwambia hivi kwa sababu nataka yule mwananchi afanikiwe jambo lake, asiogope, hii ni haki yake ya msingi. Nikamwambia sikiliza basi, mara ya pili kama wewe huna kadi ya CCM mimi nitakupa, na ya CUF pia uwe nayo kwa sababu sikulazimishi lazima uje CCM, tizama mwenyewe una hiyari yako. Akaniambia sawa basi nitafutie ya CCM unipe, nikamwambia nitakutafutia. Lakini sijampa wazo kama lazima atoke CUF aje CCM, uwe nazo mbili mfukoni, ukienda uoneshe hii na ukienda CUF uoneshe yao, ili wewe uwe na maendeleo yako. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nimesema hivi kwa machungu, kwa sababu shughuli kama hizi na sisi tuna lengo la kuwasaidia wananchi, sio kuwabagua, Wazanzibari wote tunafahamu ni ndugu, sasa kwa nini leo tufanye hivi wabaguane. Mhe. Naibu Spika, hiki kipande sio kama suala ambalo la…

Mhe. Naibu Spika: Wajumbe tumsikilize mchangiaji, tumsikilize mchangiaji

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ukiwa nacho hiki unafungua *account* benki, ukiwa nacho hiki unaweza kusoma mpaka wale wanafunzi wa *form IV,* vyote wanavyo na mimi mfano wangu wanafunzi wangu wa kwenye basi nani aliyekuwa hana kitambulisho cha Mzanzibari.

Leo mimi nitakwenda kuwauliza kama kumi hawana nitawatafutia mimi kwa gharama zangu, kwa sababu hiki kitambulisho ni muhimu kwa maisha yake yule mwanafunzi, anaweza kufungua *account*, kusafiri, kinamsaidia, kusoma zaidi kinaweza kumsaidia. Lakini sisi tumeangalia kwenye uchaguzi, uchaguzi kuna miezi mitano mbele hawa wananchi ni sisi viongozi tunatakiwa wawe na vitambulisho vya kutupigia sisi kura, lakini wananchi wana uamuzi wao wa kumchagua mtu wanayemtaka sio kwa ajili ya mambo mengine. Mambo ya uchaguzi watachagua wao, lakini kitambulisho kazi yake kubwa kumsaidia yeye mwenyewe yule mtoto au kijana yeyote kitamsaidia kwa mambo mengi kabisa.

Mhe. Naibu Spika, serikali mimi sioni kwamba hili lina usumbufu, mimi naamini serikali ina nia njema kabisa kuwapa vitambulisho. Mimi Jimbo langu la Bububu kuna watu wanaishi kwa itikadi zote mbili; CCM na CUF, lakini wote nawasaidia kupata vitambulisho hatuangalii itikadi hizo, hatuangalii kabisa, mimi siamini serikali hii kama inaangalia mambo hayo.

Mhe. Naibu Spika, lakini niendelee zaidi hii yote ni siasa tu, na yote kwa sababu uchaguzi uko mbele unakuja tunataka wananchi wetu kama kuwatumia, kuwatumia watupigie kura kwa sababu ya vitambulisho hivi. Lakini wananchi waamke, sasa hivi waangalie hata wanapokwenda kumchagua mtu waangalie kwa maslahi na maendeleo anayoyafanya kwa ajili ya maslahi yake na kumuondoshea shida yule mwananchi, tusiangalie sana kwenye uchaguzi.

Mhe. Naibu Spika, kwa mpango huu tunavyokwenda juzi Waziri wa Fedha ndugu yangu Omar Yussuf alisema hapa tunafanya siasa ndani ya Baraza la Wawakilishi, kweli. Mhe. Naibu Spika, mimi inaniuma sana, na siasa hii tukiifanya hivi, hii nchi tutaipeleka pabaya sana.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kusema jana kulikuwa na mkutano hapa, na Mjumbe ulimzuia lakini naomba radhi niseme mimi kwa sababu limenigusa hili suala.

Jana kulikuwa kuna mkutano Makunduchi wa CUF na wa CCM ulikuwa hapo Kiembesamaki, lakini kwa bahati mbaya au nzuri sijui ilitokezea vipi wakapigwa wale wafuasi wa CUF. Nasema naweka wazi Mhe. Jussa akanirushia picha saa nne kasorobo kwenye simu yangu humu, watu watatu wamepigwa wa CUF. Sasa mimi nikasema kuna nini mbona sielewi hapa, akanirushia picha zile kuna mtu akanipigia simu, wewe umepeleka gari yako wakapigwa wale wananchi wa CUF.

Gari ya Jimbo la Bububu imetoka imeenda kupiga wale watu wa CUF, mimi nikamwambia mimi suala hilo silijui, lakini pale pale nikapiga simu jamaa nataka kujua hii gari iko wapi sasa hivi, nikapiga Hospitali ya KMKM nikauliza hii gari imetoka leo, kwa sababu gari inalala pale sote tunajua. Nikaambiwa gari hii leo haijatoka hapa tangu asubuhi gari hii haijatoka, na Mhe. Naibu Spika shahidi Mungu na Mtume, nasema hivi ukweli kabisa, gari haijatoka ile imelala pale tangu jana kutwa, leo asubuhi ndio imekwenda shamba mazikoni ile gari. Sasa kwa nini tunatuhumiwa vitu kama hivi vya uongo kwa sababu ya siasa.

Mhe. Naibu Spika, hii hapa simu yangu nimetumiwa *messages* za vitisho sana humu, tumetukanwa sana CCM. Gari na sisi viongozi sote tumetukanwa, imo humu *message,* Mhe. Panya muoneshe hapo, lakini hii sio siasa tunayoifanya mambo yaliyokuwa hayajafanyika halafu unasingiziwa uongo tutaipeleka nchi pabaya.

Mhe. Naibu Spika, tusifanye siasa za chuki, tujenge siasa iliyokuwa nzuri tulete maendeleo ya nchi yetu hii, tunapoteza yetu makubwa, tunahangaika kwa ajili ya wananchi, kwa ajili ya jimbo kupata maendeleo sio kwa maendeleo kwa ajili ya binafsi yangu, kwa ajili ya wananchi wale kuwasaidia, na Mungu atanilipa mimi, lakini gharama kubwa naitumia leo nakuja kuambiwa unafanya uhujumu wa suala hili na hili.

Mimi kama uchaguzi wa Bububu nahakikisha Mhe. Naibu Spika kama nitashinda basi nitashinda kwa ridhaa ya wananchi wale wale, kwa kuipongeza Serikali yangu ya Mapinduzi, kwa nini nasema hivi, naipongeza serikali hii, na nitaendelea kuipongeza Mheshimiwa mpaka nitakufa. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu nasema hivi Serikali ya Mapinduzi leo nasema wazi wananchi wasikie naishukuru na naipongeza na nilimwambia mpaka Waziri wa Fedha nilimwambia tupo China sisi Mhe. Abubakar shahidi. Nilimwambia mimi serikali inanilipa milioni saba kwa mwezi, pesa hizi tunawasaidia wananchi, nilimwambia na nitaenda kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Bububu lakini wao ndio wamenileta mimi kupata hizi fedha.

Kwa hivyo, leo hizi fedha zinawasaidia wale watu wa Jimbo la Bububu, mimi sina pesa zaidi ya hapo lakini serikali hii inatoa milioni saba kunipa mimi…

Mhe. Naibu Spika: Malizia Mheshimiwa malizia.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Mbali posho Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme tu serikali haina nia mbaya na wananchi wake kwa ajili ya upata vitambulisho hivi vya *Zan- ID.*

Mhe. Naibu Spika, nimalizie jambo la mwisho kabisa. Mhe. Naibu Spika, mimi uchaguzi wangu ulikuwa miaka mitatu imeisha iliyopita, lakini mpaka leo mimi nilikuwa kwenye kesi ya uchaguzi pale Mahakama Kuu, mpaka juzi, leo ya nne au ya tano ndio nimeshinda uchaguzi ule mimi Mhe. Naibu Spika.

Mimi nakuja hapa Barazani nakwenda Mahakamani kupeleka ushahidi, Wanasheria wangu wananita mpaka juzi kesi tumeshinda. Mimi sasa hivi nishashauriwa yule aliyenishtaki mimi mgombea wangu Issa Khamis Issa mimi nimshtaki kwa gharama zangu alizonitia. Kanitia gharama, hivi Mhe. Naibu Spika milioni tisa nimegharamika kuwalipa ile kesi na wanasheria wangu, lakini nimeshauriwa mimi nimshtaki yeye anilipe mimi gharama zangu. Lakini mimi nikawaambia mimi siwezi kumshtaki kwa sababu sisi sote ni ndugu, nimshataki kwa nini, yeye kama kanishtaki kaona hali halisi Mahakamani nimeshinda, kwa wananchi pia nimeshinda, sasa anataka nini. Nikamwambia lakini basi mimi simshtaki na nikamtumia nikamwabia baba Mhe. Jussa mimi siwezi kumshtaki kwa ubinadamu wangu niliokuwa nao, siwezi kufanya hivyo, kama uchaguzi nimeshinda basi nimeshinda mpaka Mahakamani sasa.

Mhe. Naibu Spika, mimi nampongeza Mjumbe kwa hoja yake hii, kwa nia yake njema kwamba wananchi wapate vitambulisho, sina tatizo kwa hilo na serikali naamini kabisa ina nia thabiti kabisa ya kuwasaidia wananchi wake.

Mhe. Naibu Spika, nimalize neno moja la mwisho. Mimi nimshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, namshukuru sana, kwa nini nasema hivyo Mheshimiwa? Juzi katangaza hapa katika majumuisho ya Kamati yetu ya Ardhi, Mhe. Rais kasema mita zote kwenye vianzio vya maji zitolewe na kila mwezi Wizara ya Fedha ilipe milioni 500.

Kwa nini Mhe. Naibu Spika Mhe. Rais kasema hivyo? Kwa sababu ni kuwaondoshea wananchi wake shida, ili waondokane na tatizo la maji, na ilikuwa tatizo kubwa ni hili lakini hili moja ni kuonesha kama Serikali ya Mapinduzi ina nia njema na wananchi wake. Na mfano huu mimi sijaona Mhe. Naibu Spika tumekwenda Arusha kutizama wenzetu lakini mfano huu aliotoa Mhe. Rais ni wa kimaajabu kabisa, na kwa nia yake njema kabisa kwa kutaka wananchi wake wasisumbuke na huduma hii ya maji ndio kaamua kufanya hivi, kila mwezi serikali ipewe *ZECO* milioni 500 ili wananchi wasipate tabu kwa sababu vianzio vya maji viweze kutoa maji kama kawaida.

Kwa hiyo, Mheshimiwa kwa hili mimi nampongeza, na hii ni ishara tosha ya uchaguzi unaokuja kama haya malengo ya Mhe. Rais yatathibitisha kama ana nia njema na nchi hii na kwa wananchi wake.

Mhe. Naibu Spika, kwa kusema hayo mimi nakupongeza sana na nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, mwanzo nilisikia kwamba unamtaja Mhe. Bikame lakini nadhani umenipa dakika zaidi ya saba.

Mhe. Naibu Spika: Dakika kumi, utabakisha kumi.

Mhe. Hija Hassan Hija: Naam!

Mhe. Naibu Spika: Kumi jioni, kumi utachangia sasa hivi.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nadhani ni kumi na tatu kwa sababu ile pale ni saba.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nisema kwamba nampongeza Mhe. Hamad Masoud Hamad na naomba unipe nafasi watu wanisikilize vizuri sana kwa sababu nataka kutoa mchango.

Mhe. Naibu Spika: Wajumbe tusikilizane, Wajumbe tusikilizane.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nimpongeze Mhe. Hamad Masoud Hamad kwa jinsi ambavyo ametumia haki yake ya kikanuni, yenye kutoa mchango ambao kwa kweli utaliweka pazuri Taifa hili kama kutakuwa na serikali na wananchi na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao watakuwa wasikivu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nimpongeze Mhe. Ibrahim Makungu kwa jinsi ambavyo amechangia mchango wake mzuri, kwa upande wangu. Inawezekana wenzangu wataona mchango mbaya lakini mimi naona mchango mzuri. Kwa sababu ametoa hisia ambazo zinaonesha kwamba anayoyasema anayaamini.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza nitoe pole sana kwa wale wanachama wa CUF jana ambao walipata mtihani, mimi ni miongoni mwa watu waliofika pale Mnazi Mmoja mpaka saa sita, na ni kweli wengine waliumia vibaya macho, kiasi ambacho tuna wasi wasi kwamba watakuwa wamepoteza kiungo cha macho wengi sana. Na nitoe mkono wa pole kwa yule aliyefariki na niwaombe wenzangu baada ya Baraza hili twende mazikoni pale Kilimahewa tukamtakie mwenzetu dua aende katika safari ya milele na Mwenyezi Mungu amjalie maisha mazuri huko akhera.

Mhe. Naibu Spika, lakini ninachopenda kusema ni kwamba, uongozi ni dhamana, na dhamana lazima itekelezwe kwa mujibu wa sheria, na kwamba viongozi wengi duniani wana tabia ya kusahau dhamana zao.

Mhe. Naibu Spika, ni jambo la kawaida kwa viongozi kusahau pale wanapokuwa katika madaraka. Mimi na mwenzangu yeyote yule nimechukua gazeti la Zanzibar Leo hapa mkononi mwangu ninalo ukurasa wake wa tatu Mhe. Naibu Spika Zanzibar Leo la tarehe 11/03/2015 limetoa taarifa ya mke wa Rais Bagbo kwamba sasa mke huyu amefungwa jela miaka 20, nilipoangalia makosa yake ndani ya gazeti hili Mhe. Naibu Spika ni kwa sababu alichochea vurugu, kosa la kuchochea vurugu mke wa Rais amefungwa miaka 20 jela.

Sasa jiulize ikiwa amechochea vurugu miaka 20, je, yule aliyeua miaka mingapi? Kwa hiyo, niwanasihi viongozi wenzangu kwamba tusijisahau, hakuna mtu aliye juu ya sheria na kama hukuhukumiwa leo utahukumiwa kesho au kesho kutwa. Hakutegemea mke wa Rais ambaye ametawala zaidi ya miaka kumi na tano au ishirini leo yuko jela kwa kosa la kuchochea vurugu. Nasaha zangu kwa viongozi wenzangu, Wawakilishi wote na serikali kwa ujumla watahadhari na dunia, dunia ni mpito na kila mtu iko siku ataonja machungu ya dunia.

Mhe. Naibu Spika, mimi si msemaji wa Chama cha CUF, wala si Mnadhimu wa Baraza la Wawakilishi upande wa chama lakini wala simshutumu ndugu yangu Mhe. Bhaa kwamba ndiye ambaye gari yake jana ilifanya makosa hayo au vipi, lakini mashuhuda ambao walishuhudia kwa mujibu wa *plate numbe*r na picha za gari zilizopigwa waliohusika walioshuhudia wapo.

Kwa hivyo, kama ni ukweli Baraza hili basi Kamati Teule nijiridhishe kufuata *plate number* na picha zikatafute mmiliki wa gari lile ni nani. Ikiwa mmiliki wa gari ile ni Hija Wazanzibari waambiwe mmiliki wa gari ile iliyofanya fujo ni Hija, ikiwa ni Juma Duni aambiwe Juma Duni umepeleka gari kufanya fujo, lakini *plate number* zipo kwa picha na ushahidi upo. Kwa hivyo, mimi sitaki niseme Mhe. Bhaa au nani, lakini ninachosema Mhe. Saleh amesema pale kwamba duniani moto hauzimwi kwa petroli. Viongozi mnajaribu kuzima moto kwa petroli ningewanasihi mkachukua maji baridi mkazima moto…

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Hija twendeni kwenye hoja tumalize.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, huo utangulizi na wenzangu mmewapa nafasi kama hii lakini sijui…

Mhe. Naibu Spika: Twende kwenye hoja.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, mimi nawashangaa Wawakilishi, na daima nitasema hata kama watu wanakasirika. Mwakilishi ambaye ni kigeugeu hafai kuwa mwakilishi, mwakilishi ambaye hajui aliyoyasema jana ni sawa sawa na Haji Vale hafai kuwa mwakilishi, mwakilishi ambaye hajui anachokisema ni mtihani mkubwa, na

wananchi jamani, wananchi chonde chonde wachagueni wawakilishi wanaojua kusema na wanaojua maana ya kusema.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Makame Mshimba ni mtu wa mwanzo Baraza hili aliyesema kwa mujibu wa *hansard* kwamba ana ushahidi wa watu wageni kupata vitambulisho. Leo Mshimba yule yule ndiye anasema hakuna mtu aliyepewa vitambulisho. Sasa mimi sisemi zile fomu, nina nyaraka vitambulisho 350 vyote vina saini ya Wakurugenzi wa Vitambulisho wa Wilaya, sio fomu ya sheha, sio fomu ya kiapo, tayari wamepiga picha tena na risiti kopi tangu 2013 mwezi wa 4.

Mhe. Naibu Spika, hiyo sio fomu, ni risiti, serikali imeshindwa kuwapa, lakini mwezi wa 7/2006 nilivyokwenda Mbeya nimewasikia Wakristo wanaimba nyimbo, mimi si mkristo lakini Mhe. Marina anaweza akatusaidia kwamba usimpime mtu kwa maneno, mpime mtu kwa matendo, mtu haokoki kwa maneno unaweza ukasema hapa mimi muislamu, mimi mkristo kumbe maneno tu lakini matendo ndio muhimu.

Kwa hiyo, tuwapime serikali kwa matendo sio maneno, haya ndio matendo Mhe. Naibu Spika. Na juzi hapa niliposema serikali wanasema uongo watu wote wakaandika magazeti Hija katukana.

Mhe. Naibu Spika, uongo hauna nembo, uongo hauna alama, kama ile chapa ya serikali, uongo ni matendo. Kwa hivyo, mimi Mhe. Naibu Spika naiomba serikali iniambie risiti hizi ambazo walitoa wenyewe walitumia fedha za umma (*public money*), wakachapisha, wenyewe kwa nini hawawapi. Leo anakuja Mwakilishi hapa aliyekula kiapo kwenye Katiba kwamba hakuna ushahidi, uongo, wewe kweli mwakilishi, mwakilishi au mtihani. Kwa hivyo, ushahidi huo Mhe. Naibu Spika, ahsante nakushukuru.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Hija utamalizia jioni, Waheshimiwa Wajumbe hoja ina wachangiaji wengi, mpaka hivi sasa ina wachangiaji 27 na humu hamna waziri ni wajumbe peke yao, na waliochangia ni saba pamoja na mtoa hoja. Sasa naomba jioni tuje tupange muda maana hoja hii nataka imalizike leo.

Kwa hiyo, tujitahidi tuje mapema, wale walioleta karatasi za kuchangia waje mapema, tatizo tulilonalo tukija jioni tunaanza na watu watano, wanne si utaratibu mzuri. Sasa hivi tumeenea kwenye Baraza na jioni saa 11:00 tuwe tumeenea tuanze kumaliza michangio yetu.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya hayo nawashukuru kwa kunipa mashirikiano, naahirisha kikao mpaka saa 11:00 jioni leo.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Kipindi cha asubuhi alibakisha dakika kumi Mhe. Hija Hassan Hija, kwa hivyo namwita Mhe. Hija Hassan baadae afuatie Mhe. Abdalla Juma Abdalla na Mhe. Wanu Hafidh Ameir ajiandae.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii ya mwanzo jioni ili nimalize dakika zangu kumi ulizoniahidi, ingawa ni chache mno lakini nitatimiza wajibu wangu kwa mujibu wa maelekezo yako.

Mhe. Naibu Spika, asubuhi nilimalizia kusema kwamba hoja hii si hoja ambayo yenye kuhitaji utashi wa kisiasa. Nilizungumza asubuhi kwamba mimi nina risiti ambazo serikali yenyewe wamepitisha, wamewapiga picha na wametumia fedha za umma lakini hadi hii leo hawajapewa hati zao za kitambulisho. Nitafanya utaratibu nimpe Mhe. Waziri ili aone jinsi ambavyo serikali ilivyotumia fedha za umma lakini hawakupewa vitambulisho watu husika. Sasa huku unawalipa watu mishahara, unatumia nyenzo za serikali, lakini unashindwa kuwapa watu haki yao ni kinyume na utaratibu.

Mhe. Naibu Spika, hoja yangu ya pili suala la vitambulisho vya Wazanzibari ni suala la kisheria au ni suala la haki? Sheria ya vitambulisho inasema wazi kwamba mtu yeyote ambaye hana kitambulisho basi sheria ilimtaka kuwa

akamatwe na apelekwe Mahakamani. Sasa kwa nini serikali haiwakamati wale wote ambao hawana vitambulisho, ili wakapelekwa Mahakama wakaenda kujitetea wakajua nini msingi wa kukosa vitambulisho. Lakini hawakamatwi kwa makusudi kwamba wanajua watakapowakamata, watatoa ushahidi kuwa wamenyimwa kwa makusudi vitambulisho na ndio maana serikali inafanya kama hili suala hawalijui.

Vile vile, sheria inasema kwamba yule ambaye anamnyima mtu haki basi anapaswa kuwa ni mkosa, na akikutikana na hatia lazima aende Mahakamani, ni kwa nini basi wale wanaowanyima haki wananchi wetu hawawezi kukamatwa na kupelekwa Mahakamani ili sheria ikachukua mkondo wake.

Mhe. Naibu Spika, asubuhi nilisema hapa kwamba ni vyema suala hili lisifanywe kiutashi, haki ya mtu lazima ilindwe na lazima itetewe kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar na kwa mujibu wa Katiba zote za ulimwengu huu na maazimio ya kimataifa. Sasa mimi nataka nitoe mfano wa wiki hii ambapo Mhe. Hamad Masoud Hamad nataka aungane na Mhe. Waziri tufanye ushahidi wa haya tunayoyazungumza, nimechukua *sample* ya shehia mbili tu za Wilaya ya Mkoani; hii ya kwanza Shehia ya Makoongwe.

Mhe. Naibu Spika, shehia hii natoa mfano wa watu saba, Waziri wa Katiba na Sheria aniambie lini watu hawa wamepata vyeti vya kuzaliwa ili wazuiwe vitambulisho na hatimaye akatoa vitambulisho.

Mhe. Naibu Spika, naomba niwataje kwa madhumuni ya *hansard* watu hawa ambao tayari wamewapiga picha wiki hii bila ya hata ya kuwa na cheti cha kuzaliwa na bila ya hata ya kuwa na sifa za kujiandikisha. Mtu wa mwanzo ambaye amepewa hati hiyo na hana cheti cha kuzaliwa ni Bibi Mwamize Ali Bakari, ni kutoka Makoongwe na huyu pia naambiwa ni mgonjwa wa akili. Bi Mwamize Ali Bakari hana cheti cha kuzaliwa lakini tayari amepigwa picha. Sasa Waziri wa Katiba na Sheria atwambie kwa nini akapata haki bibi huyu wakati hana cheti cha kuzaliwa.

Wa pili ni Bi Salma Abadalla Magonja na Bi Masha Abdalla Magonja ni mtu na ndugu yake, wamepiga picha lakini hawana vyeti vya kuzaliwa, watwambie serikali kwa nini wakapigwa picha na hawana vyeti vya kuzaliwa.

Wa nne ni Bwana Salim Bakari Makame, Bibi Asha Mshamara, Kazija Said Masoud na Zainabu Makame Juma, wote hawa watu saba kutoka Makoongwe, mwezi huu wa Tatu wamepiga picha bila ya kuwa na vyeti vya kuzaliwa, ni kwa nini waruhusiwe kupiga picha bila ya kuwa na vyeti vya kuzaliwa wakati sheria hairuhusu hivyo.

Sasa kama hilo linafanyika ndio wananchi wa Zanzibar wakalalamika kwamba, ni kwa nini watu A waruhusiwe kupiga picha bila ya utaratibu wa kisheria na watu wengine wasumbuliwe wakati wana sifa zote za kisheria, ndio malalamiko haya ambayo wananchi wanalalamika, na ndio maana ikawa mgogoro baina ya wananchi wanaokosa haki na wanaopata haki. Hiyo ni Shehia ya Makoongwe.

Shehia ya Kiwani jimboni kwangu anitajie watu 11 niko tayari hata kesho tukawaite watuoneshe vyeti vya kuzaliwa na kwa nini wamepiga picha. Wa mwanzo ni Bwana Shaibu Makame Ali, wa pili ni Bwana Kombo Abdalla Vuwale, Tatu Bwana Abdalla Omar Ali, wa nne Mohamed Haji Othman, Hamada Salim Ali, Othman Abdalla Omar, Said Khalfan Said, Nassor Abdalla Vuwale Shaibu Juma Nyandu, Salum Hamad na Mkubwa Ussi Vuwadi. Hawa wote wamepigwa picha mwezi wa Tatu bila ya kuwa na vyeti vya kuzaliwa.

Mhe. Naibu Spika, hawa wote ukiwachunguza sipendi kusema hivi lakini lazima tuseme, wote ukiwachunguza hawa ni wanachama wa Chama cha Mapinduzi. Kwa hivyo, hiyo hoja kwamba wanaopewa vipande hivi ni CCM ni hoja ya msingi, kwa sababu ushahidi ni huu, na kama hawa wana sifa Mhe. Waziri tuondoke mimi na wewe kesho tukawakusanye Jimbo la Kiwani watuoneshe vyeti vya kuzaliwa, ni kwa nini wakapewa vyeti vya kuzaliwa na kwa nini wakapewa vipande vya Mzanzibari Mkaazi wakati hawana vyeti vya kuzaliwa.

Kwa hivyo, hao ukiwachunguza wote ni CCM, hivyo kila mtu ana haki ya kusema kwamba kumbe haki hii si haki ya Wazanzibari ni haki ya wanachama wa Chama cha Mapinduzi. Kwa msingi huo kama ni haki ya CCM maana yake hatupaswi sisi kuzidisha kodi za wananchi kuhudumia upande mmoja wa chama kinyume na utaratibu.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu ya muda mdogo ningependa niseme mambo haya yafuatayo. La mwanzo ni kwamba hoja hii ya Mhe. Hamad Masoud nadhani watu wazima wasingeliweza kulumbana. Serikali ingetoa maazimio tukakubaliana, kwa sababu kuna watu wanadai kwamba kuna watu wana haki hawajapewa haki zao na kuna wachache wenye nguvu wanadai kwamba watu hao hawana sifa, basi wala tusiunde kamati teule lakini tuunde timu

maalum ya serikali na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuwaite watu hadharani waoneshe ushahidi wao kama kweli wao wamenyimwa haki zao na kama hawana sifa basi wataachiliwa, lakini hatuwezi kuacha watu wenye sifa na kuchukua watu ambao hawana sifa tukawapa haki, baadae ukatangaza kwamba unalinda utawala bora, unalinda misingi ya haki na eti atakayefanya vurugu utamdhibiti. Nadhani anayefanya vurugu huyu anayenyima haki ya mtu ndio wa mwanzo wa kudhibitiwa, kwa sababu ndiye amefanya vurugu katika nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, nimuombe Mhe. Waziri kabisa, kwamba afanye busara zake, na kama kweli ni muungwana basi awaite hawa watu mbele ya timu ya Baraza la Wawakilishi bila ya ubaguzi, achague timu ya Wawakilishi kutoka CCM na *CUF* kupitia kila wilaya tuone hao watu ili kulinda haki za watu ili kesho na keshokutwa mambo haya yasitufuate mbele ya safari.

Hili suala ni gumu, watu wanapewa hati kinyume na utaratibu na mimi nina-*challenge* hawa niliowataja nina zaidi ya hawa ambao ninao, twendeni Jimbo la Kiwani tukawaite mbele ya umma watuoneshe vyeti vya kuzaliwa, ni kwa nini wamepewa haki ya kupiga kura, ni kwa nini wamepewa haki ya vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi wakati hawana vyeti vya kuzaliwa. Hayo ndio malalamiko ya msingi ya wananchi mbali mbali ambao tunasema kwamba, kumbe haki hii ya msingi ni haki ya Chama cha Mapinduzi na wengine hawana haki hiyo.

Mhe. Naibu Spika, kama hivyo ndivyo ni lazima tuseme kwamba serikali kupitia Chama cha Mapinduzi wanavunja sheria, ni lazima sheria ilindwe. Lazima tukubaliane kwamba hili ni tofauti na utaratibu wa kisheria, na waziri anayehusika kwa kweli likizuka fujo yeye atakuwa ndiye aliyesababisha fujo jambo ambalo wananchi wa Zanzibar hawalipendi. Watu wamekuwa mahodari wa kutetea hoja lakini na wapinge hoja.

Mimi nimetaja majina hapa, mtu aseme hawa watu wana vyeti vya kuzaliwa, ni jukumu la Waziri wa Katiba na Sheria, ni jukumu la waziri wa vitambulisho kwa nini wakapewa haki hawa hawana vyeti vya kuzaliwa, kwa nini wakapewa haki hawa umri wao ni mdogo na wananyimwa watu zaidi ya 30 elfu kwa mujibu wa hoja ambao hawana vitambulisho.

Mhe. Naibu Spika, Jimbo la Kiwani peke yake lina watu zaidi ya 400 wenye sifa halali kabisa hawana haki hii ya msingi. Sheria zipo, katiba ipo, Mwanasheria Mkuu yupo, sheria inavunjwa, katiba inavunjwa hakuna hoja yoyote watu wamekaa tu, kwa nini? Ni kwa sababu ya CCM, ni kwa sababu ni viongozi. Uongozi ni dhamana, na lazima dhamana ilindwe, lazima tukamate majukumu yetu.

Mhe. Naibu Spika, niunge mkono hoja hii ya Mhe. Hamad Masoud kwa kusema kwamba, niwaombe viongozi wenzangu hili jambo wasilione dogo, hili jambo litasababisha mambo makubwa huko mbele, lazima haki ilindwe na niwaombe sana viongozi wenzangu kwamba wasisahau uongozi ni dhamana, lazima dhamana itekelezwe, na anayekwepa dhamana basi atajibu dhamana mbele ya Mwenyezi Mungu na mbele ya Mahkama pale haja ikitokezea. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe naomba tushauriane kwamba baada ya kumaliza Mhe. Hija Hassan tuna Wajumbe 20. Sasa nitatoa dakika kumi kumi, atayezidisha kidogo itakuwa 15 ili sote tuchangie. Kwa hivyo, mtu nikimwambia bado muda fulani anifuate ili tuweze kupata nafasi watu sote 20 tuliobakia. Nadhani tumeelewana, sasa nafasi tunampa Mhe. Abdalla Juma Abdalla.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi jioni hii kwa kusema mawili matatu kwenye hoja hii muhimu ambayo inahusu haki za wananchi wetu. Kwanza nataka nimpongeze sana mtoa hoja, tunampongeza kwa sababu katimiza wajibu wake, kwa sababu moja katika kazi za Waheshimiwa Wawakilishi ni kutetea haki za wananchi. Sasa haki ya kupata kitambulisho ni haki ya mwananchi kikatiba, sasa inaponyimwa basi tuna wajibu wa kuwatetea. Kwa hivyo, nampongeza sana kwa kutimiza wajibu wake.

Pili, nataka niwatanabahishe viongozi wenzangu, sote ni viongozi hapa, kila mmoja ana majukumu yake, lakini tusisahau kama sisi viongozi tumebeba *commitment* kubwa sana mbele ya jamii na tumeapa kuilinda Katiba ya Zanzibar, Katiba ya Jamhuri ya Muungano, ambamo humo ndani ya katiba ndimo mwenye haki za watu. Sasa tunapaswa au tunawajibika kulinda katiba, na kama hatukuilinda katiba maana yake hatukulinda haki za watu, na kama hatukufanya hivyo kwa sababu ni viongozi basi tujue kama kesho akhera Mwenyezi Mungu atatuuliza.

Mimi Abdalla Juma najua nitaulizwa lakini *wallahi* na Mhe. Mohamed Abood ataulizwa, Mhe. Balozi ataulizwa, rafiki yangu Mtumbatu mwezangu Haji Omar Kheri ataulizwa, Dkt. Mwinyi ataulizwa, Mhe. Abubakar Khamis naye ataulizwa na atakayetuuliza ni Hakimu wa Mahakimu wote, na *wallahi* kama hatukutekeleza wajibu wetu tutahukumiwa. Sifa za Hakimu huyu hatoi hukumu kwa kujuana na mtu wala hampi *favor* mtu yeyote isipokuwa yule aliyetimiza haki. Sasa tufanye tufanyayo, lakini tujue tutakwenda zetu huko mbele ya Mwenyezi Mungu na tutaulizwa kuhusu haki za watu ambao tumewasimamia.

Mhe. Naibu Spika, laiti ingekuwa kuna mawasiliano kati ya sisi tulioko hai na wale waliokufa, *wallahi* tusingefanya haya hata siku moja, lakini Mwenyezi Mungu kaweka pazia mpaka uende ndio utakutana nayo. Bahati mbaya sana ukishafika huna muda hata wa sekunde tano za kufanya vyenginevyo, kwa hivyo shauri zenu.

Mhe. Naibu Spika, wananchi wengi sana wanalia na masheha, tumekuwa tukiwasema sana masheha hapa kwamba hawatimizi wajibu wao, wanaminya haki za watu na hii nyimbo toka siku tuliyoanza kuiimba humu mpaka leo tunaendelea. Sasa masheha wanawanyima watu fomu wengine wanapiga chenga, wakiona unawafanyia ghasia sana ukienda nyumbani humkuti anakwambia niko kazini, ukienda wilayani hayuko utaambiwa yuko nyumbani, ukienda nyumbani hayuko, ukimpigia simu anazima, alimradi anapiga chenga ili aendeleze lile agizo alilopewa. Maana yake wanasema hasa ukiwabana kweli kweli wanakwambia bwana tumeagizwa, nani aliyekuagizeni? Ah wakubwa! Utasikia wakubwa tu hakwambii nani. Lakini inaonekana na tulipokuwa tunapitisha sheria hapa ya Tawala za Mikoa tulisema masheha hawafai.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu sheha aliyesoma haburuziki, ipige *proposal* angalau sheha awe na *Form IV* nyote mtakakataa hapa. Sasa sheha mbumbumbu asiburuzike vipi, yale maagizo aliyopewa anafanya vile vile hana kipimo cha kupima kama hili nilifanyalo mimi nakiuka haki za mtu, agizo hili si la haki, hana kipimo hicho. Kwa hivyo, wewe ukishamwambia fanya hivi ndio atafanya hivyo hivyo, na uzuri wenyewe ukimuhoji atakwambia naagizwa mimi hana lugha nyengine ya kukwambia. Sasa kwa kweli wananchi wananyimwa haki sana.

Mhe. Naibu Spika, nina vyeti vya kuzaliwa hapa havipungui 70, vyote hivi ni vyeti vya watu waliotimiza umri lakini sheha anapiga chenga hawapi vitambulisho mpaka leo. Wanasema wanaojitetea kwamba hawatampa mtu mpaka aliyetimiza masharti.

Sasa mimi nilikuwa najiuliza hasa haya masharti ni yepi, maana yake cheti cha kuzaliwa mtu anacho, kama ni sharti la ukaazi wa miaka mitatu mtu keshakaa kwenye shehia yake miaka 20, hivi sharti gani jengine? Lakini baadae nikafanya *research* nikagundua alaa kumbe sharti moja kubwa ambalo kila mtu analitaja hapa, kila anayesimama tena anaagiza mtu bwana mimi naagiza hapa, kila aliyetimiza masharti apewe fomu kumbe Mhe. Naibu Spika, sharti ni kuwa CCM? Maana yake hawa wote hakuna mtu hata mmoja aliyenijia mimi nikamuuliza wewe CCM au *CUF* akanambia mimi ni CCM, wote ni *CUF* ndio wanaonyimwa, kumbe sharti kubwa la kupata hiki kitambulisho hadi uwe CCM? Sasa kama ni hivyo tubadilisheni sheria, tuifanyie marekebisho tuweke vifungu mule moja katika masharti muhimu ya kupata kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi basi mtu awe CCM, hebu tufanyeni hivyo ili iwe sheria tusipige makelele, ikishakuwa sheria basi, lakini kama sharti ni kuwa CCM hawa mnawanyima haki zao, na *wallahi* kesho akhera mtaitoa kwa nguvu nakwambieni.

Mhe. Naibu Spika, kuna usemi hapa ambao hawajatimiza miaka mitatu, sijui hawakuomba *transfer*. Mimi kule jimboni kwangu nina watu hawajaondoka wamezaliwa pale, wakakulia pale, mpaka leo wako pale, sasa miaka mitatu hiyo maana yake nini?

Mhe. Naibu Spika, nina watu katika shehia ya Matale, kule jimboni kwangu kuna shehia moja inaitwa Matale na ninaomba sana Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ naomba a-*mark* hiyo. Kama kuna sheha mkorofi kule jimboni kwangu siku za nyuma nilikuwa namtaja mwengine leo nakutajia sheha wa Matale, huyu sheha mbaya sana, katika sheha mkorofi kule ni huyu. Kwa sababu *Wallahi laadhim* yeye anafika pahala anakwambia fanya unavyotaka basi, simpi! Sasa jamani tumkamate roho tumfikiche? sheha wako wa Matale huyu nina watu 70 wana vyeti vikubwa na wote ni wakaazi wa Matale hawajawahi kuondoka hata siku moja hawapi mpaka leo hajawapa. Sasa naomba sana a-*mark* hilo.

Shehia ya Kilindi ina watu wanafika 30 huu ni mwezi wa sita washapigwa picha, wameshapewa vile virisiti vyeupe mpaka leo mwezi wa sita huu wanapigwa danadana, ukienda ngoja kesho, ngoja keshokutwa sijui kuna baridi mpaka leo hawapewi.

Shehia ya Kipapo ina watu 27 wameandikishwa huu mwezi wa tatu kila siku danadana, Shehia ya Pujini nina watu 24, kuna Shehia ya Kumvini ina watu 14 na wote hao tayari wameshapigwa picha, lakini ile kupewa kile kitambulisho mpaka wameshachoka.

Sasa jamani hii tunayofanya kwa kweli sio haki, wala mimi sikubaliani hata siku moja na hoja isemayo, na hii mara nyingi huwa anaitumia Mhe. Waziri, hoja isemayo kwamba mtu aliyenyimwa akate rufani kwa Mkurugenzi.

Mhe. Naibu Spika, mtu masikini ya Mungu yuko shamba kule Pujini keshanyimwa fomu na Sheha unamwambia asafiri aje Unguja kuja kupeleka rufani yake kwa Mkurugenzi, huko si kumnyanyasa ni kitu gani. Basi Mkurugenzi bora aje kule Pemba afanye ziara ya kuja Pemba, kuna siku moja alikuja kule na tukamlalamikia akatwambia kuwa hakuna watu ambao hawapewi hali tukamwambia wapo, akasema nileteeni kama wapo, tukamuuliza utakuwepo Chake chake Afisini lini, akasema siku fulani nitakuwepo, tukampekelekea watu 2000 alikimbia hata ile Afisi hakuikaribia, alitafuta upenyo akaenda akaagiza majeshi katawanyeni watu, watu wakapigwa marungu pale wakatawanywa. Sasa jamani hii ni haki?

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nimalizie kwa kusisitiza tu, kwamba kwa kweli kinachoendelea sio sahihi, tunawanyima watu haki zao kwa sababu za kisiasa, kwa sababu ni siasa tupu huku.

Sasa bahati mbaya sana vitambulisho hivi vimeunganishwa na mambo mengine, vimeunganishwa na huduma nyingi, mtu hawezi kuzipata mpaka awe na kitambulisho. Sasa kama ni hivyo, hebu tutenganisheni kama kitambulisho ni kwa ajili ya siasa basi haya mambo mengine yatafutiwe utaratibu mwengine, au hiki kitambulisho kitolewe ndani ya siasa tukiachie mambo mengine, na siasa iwekewe masharti mengine.

Lakini hebu *imagine* ile sheria inasema wazi mtu aliyekuwa hajajisajili kama Mzanzibari mkaazi anapaswa achukuliwe hatua, na akikamatwa akithibitika na kosa hilo la kutojisajili maana yake anapigwa faini shilingi laki moja au anafungwa mwaka mmoja, sheria ile ndio inasema hivyo. Haya hebu tuwaulizeni nyinyi watu wa serikali mumeshashitaki wangapi, na watu tele wapo, na kama hamjawashitaki, hamjawashitaki kwa sababu gani. Hawawezi kuwashitaki, kwa sababu wao ndio wanaowanyima.

Sasa Mhe. Naibu Spika, mimi nafikiri sasa wa kuwashitaki ni Masheha, kwa sababu masheha ndio wanaowasababisha watu wasipewe vitambulisho. Hebu sasa wananchi wote wawaburuze Masheha mahakamani wakajibu kwa nini hawatoi vitambulisho, maana wao ndio sababu kama hujapata ile fomu ya Sheha hutapi kitambulisho. Halafu wakati wananyimwa Wazanzibari wenye haki ya kitambulisho kuna watu wengi mno wasiokuwa na haki ya kupewa vitambulisho lakini wanapewa kwa sababu za kisiasa.

Mhe. Naibu Spika, mimi namalizia, lakini nawaomba sana wenzangu, maisha ya hapa duniani ni mafupi sana, na kama kuna jambo jema lolote utakaloliona; kama ni nyumba nzuri, kama ni mshahara mnono kama uluwa kama ni kitu gani, haya ni madogo sana kuliko yalioko akhera.

Tutekelezeni haki za watu hapa tutaondoka, na tukifika huko *wallahi* kama hatutekelezi haki za watu tutajuta sana. Maisha mafupi sana haya, wangapi walikuwepo hapa sasa hivi hawako tena, wangapi waliokuwa na uluwa sasa hivi ni masikini za Mungu mitaani wanaomba. Kwa hivyo, yasitudanganye wala yasitughilibu haya.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba kuunga mkono hoja hii mia juu ya mia, na nawaomba wote wanaohusika na kadhia hii ya kutoa vitambulisho basi wajitahidi wawapatie watu haki zao, ili hii nyimbo ifike mwisho, imeshaimbwa zamani sana hii nyimbo, na inachafua hata amani ya nchi yetu.

Inafika pahali hata wale wananchi wamepoteza imani na serikali yao, hawataki kutoa hata ushirikiano na serikali yao.

Siku moja nilipita hapo wakati wanafanya sensa pale hapa kwa Sheha kidevu nikakuta mgogoro mkubwa mpaka Polisi wamekutanika pale. Haya nikamuuliza Sheha vipi jirani yangu, mimi tunajuana sana, aah wananchi hawataki kuhesabiwa bwana.

Mhe. Naibu Spika: Sasa humalizii unaendelea kuchangia.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Wananchi bwana hawataki kushirikiana na serikali, hawataki kuhesabiwa wanasema ati hatuwatambui. Nikamwambia kwani mnawatambua kweli, mngewatambua basi na wao wangetoa ushirikiano hasa, hebu *baada ya kisa mkasa,* fanya vitu vyema na yeye akujibu vyema.

Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii na mimi nikasema machache juu ya hoja hii binafsi ya Mjumbe, ambaye anaitaka serikali kuchukua hatua za kuwatunzia Wazanzibari wote waliotimiza sifa za kisheria haki yao ya kuwapatia vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na afya, lakini pili nikushukuru wewe kwa nafasi hii.

Mhe. Naibu Spika mimi nitakwenda moja kwa moja katika hoja, lakini kabla sijaenda huko naomba niseme machache. Kabla sijaanza kuchangia naomba niweke sawa kidogo hoja ya Mjumbe ili tufahamiane uzuri.

Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa 3 mtoa hoja anasema kwamba:-

"Hivyo basi, Baraza la Wawakilishi, kuna maelezo hapo lakini nitaingia mstari wa pili kutoka mwisho ambao anasema "*linaitaka serikali*".

Mhe. Naibu Spika, naomba nimuweke sawa kidogo mtoa hoja, hapa hatujakubaliana bado, kwamba hoja hizi ambazo wameleta kwamba ni za Baraza. Hoja bado ni yake binafsi, mpaka pale tutakapokubaliana kwamba sasa ya Baraza ndio sisi kama Baraza la Wawakilishi tutaitaka serikali kufuata haya ambayo Mjumbe binafsi ameweka, hilo la kwanza.

Lakini la pili Mhe. Naibu Spika, nataka niseme kwamba hakuna aliye msafi, kila mtu anakosa. Kama wewe unafikiri mwenzio mchafu katika hili wewe una machafu mengine, na sisi sote tutakwenda kwa Mungu bila hata ya kupelekana, kila mtu muda ukifika tutakwenda kwa Mungu wala haina haja ya kupelekana. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, sasa niingie kwenye hoja kiujumla nakubaliana na mtoa hoja, kuwa haki ya kupata kitambulisho ni ya kila mtu kama ilivyo haki nyengine; haki ya kuishi, haki ya kuheshimiwa na haki nyengine zote. Lakini haki hiyo ni kama vile ilivyowekwa kikatiba, sheria ambazo zimetungwa na Baraza la Wawakilishi, hakuna haja ya kuishurutisha serikali ifanye hivi ifanye vile, na kwa mantiki hiyo Mhe. Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia hoja moja moja za Mjumbe, niseme kwamba siungi mkono hoja hii, na siungi mkono kwa sababu ambazo nitazitaja. Na sitachangia hoja zote, nitachangia hoja ya kwanza, pili na tatu, hizo zitatosha kuua hoja ya nne na ya tano.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, utoaji za *ZAN ID* unaongozwa na masharti ya kisheria, na kwa mujibu wa sheria hiyo masharti yamewekwa ya kusajiliwa mtu na ya kutosajiliwa mtu.

Mhe. Naibu Spika, Baraza halina uwezo kutokana na sheria zile, halina uwezo wa kuingilia utaratibu wa kisheria uliowekwa na sheria zile, ikiwa mtu atakosa kusajiliwa.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, Baraza linatakiwa kufuata utaratibu wa kisheria na sio kutoa maamuzi kinyume na sheria ambazo zimetungwa na Baraza hili hili. Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, kwa mantiki hiyo, hoja ya kwanza sikubaliani na nashawishi wenzangu wasiikubali hoja hii, kwa sababu masharti ya kupata vitambulisho yamo katika sheria, hapa

Baraza hatuna uwezo wa kuweka upande sheria hii, na tukaitaka serikali ifuate maelekezo ya hoja ya Mhe. Hamad Masoud Hamad ambayo ameitoa.

Lakini Mhe. Naibu Spika, katika hili hili niseme kama ni kupata haki sheria ngapi hapa tunapitisha na watu hawapati haki zao. Tumepitisha sheria ya mtoto hapa kuna sheria kibao ambazo zinamlinda mtoto, watoto hawapati haki zao na wanabakwa kila siku, na kila siku hapa tunasema na nyinyi si watetezi wa wananchi, mbona hamjaleta hapa hamjaishurutisha serikali kwamba aaah kwa hili linatokea watoto wetu wanaharibika, na hawa ndio Taifa la kesho tuweke pembeni sheria tufuate haya tunayotaka sisi, hamjaleta hapa na nyinyi ndio mnaowatetea wananchi.

Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika mimi sioni mantiki ya hoja ya Mjumbe, hoja ya kwamba kutaka Masheha wote kuwapatia Wazanzibari wenye sifa fomu za maombi, utaratibu upo, uende kwenye sheria wafuate, hamna ambaye yupo juu ya sheria, sote tuko sawa sisi tumefuata utaratibu na tutakapata vitambulisho na wao wafuate utaratibu na wao watapata vitambulisho, haina haja ya kushurutishana hapa!

Mhe. Naibu Spika, hoja ya pili haki ya mtu kupewa kitambulisho sitaki kusoma na-*save* muda, kwa sababu sitaki kusoma hoja za Mjumbe zinavyosema naomba nitoe maelezo ya moja kwa moja.

Hoja ya pili inasema kwamba naipinga kwa sababu ya mtu kupewa kitambulisho ni haki ya kikatiba, na masharti yake yamewekwa vizuri katika Ibara ya 6 ukurasa wa 2 Wajumbe watizame pale ipo kabisa imeeleza vizuri sana.

Pia Mhe. Naibu Spika, kama mtu hajaridhika na haya yaliyoelezwa katika kifungu cha sita, kifungu cha 25(a) cha Katiba hii hii ya Zanzibar kinatoa fursa kwa mtu yeyote ambaye hajaridhika na kitu chochote ambacho kimo kwenye sheria kwenda Makahama Kuu na sio Baraza la Wawakilishi. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, sisi hapa hatuhukumu kesi za katiba, kesi za katiba zinahukumiwa kwenye mahakama kuu ya Zanzibar. Sasa kama katiba imeweka utaratibu wa kupatiwa vitambulisho na Mjumbe hajaridhika na yale masharti ambayo yamewekwa katika katiba hii, aende Mahakama Kuu asije hapa, hawezi akaja na hoja hii ya *page* nne (4) kututaka sisi tuvunje Katiba, kwa sababu tu kaja na makaratasi haya ya *page* nne (4) kututaka kwamba tuishurutishe serikali ifanye hivi, *we can't*!

Kama yeye anahisi kwamba watu hawapati haki, aende Mahakama Kuu akashitaki katiba imetoa fursa lakini sio hapa Baraza la Wawakilishi, sisi hatuna majaji, tuna wataalamu wa mimea, kuna wakulima ilimradi tumo mchanganyiko lakini hakuna majaji. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kabla sijaingia hoja ya 3 kama nilivyosema kwamba haina haja ya kuitika serikali hapa tukaishurutisha lazima ifanye hivi lazima ifanye. Baada ya Mjumbe kututaka sisi watu wazima na akili zetu tuvunje utaratibu mzima wa katiba uliowekwa, ni vyema Mjumbe akashajihisha wananchi kufuata taratibu hizi za katiba na sheria zilizowekwa kuliko kuja hapa Mhe. Naibu Spika, akatutaka sisi kama Wajumbe ambao wengine walitunga sheria hizi, na naamini mtoa hoja na yeye alikuwemo katika Baraza lile kama alitoka nje kama walivyo imekula kwao! (*Makofi*)

Lakini sheria imeshapita, na sheria ikishapita yaani ile *goodness* ya sheria na *badness* ya sheria hatua ya ile sheria yenyewe kama sheria ina matatizo alete *amendment* hapa turekebishe sheria. Lakini sio kututaka sisi watunga sheria sisi tukavunja zile sheria. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, hiyo haiwezekani. Lakini naona imeshawasha taa namaliza hoja ya tatu.

Hoja ya tatu (3) kwamba utaratibu wa usajili wa Wazanzibari wakaazi ni wa sheria. Masharti yameelezwa kwenye sheria namba 7 ya mwaka 2005 ambayo ilitungwa na Baraza hili hili, na kama nilivyosema na yeye Mheshimiwa alikuwemo, nafikiri kipindi chake cha tatu karibu tutampa risiti, kipindi chake cha tatu.

Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa usajili wa Wazanzibari wakaazi ni wa sheria, Baraza haliwezi kuiagiza Afisi ya Usajili wa *Zan-ID* kufuata masharti tofauti na yale ambayo yamewekwa na sheria, kama nilivyosema

mwanzo kwamba sisi ndio watunga sheria, halafu pale pale unakuja na hoja yako ya *page* nne (4) kututaka sisi tuvunje sheria ambazo wamezitunga wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, hilo haliwezekani, na mimi kwa mantiki hiyo niseme kwamba siungi mkono hoja hii hata kidogo, na nashawishi Wajumbe wenzangu kutounga mkono, kwa sababu hatuwezi tukatumia sehemu hii hii ambayo tuliyotunga sheria tukageuka tukawa vigeugeu tukaja kuvunja sheria hapa hapa.

Mhe. Naibu Spika, maneno yetu yaendane na matendo yetu. Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo niseme tena kwamba siungi mkono hoja, na naomba Wajumbe wenzangu wasiunge mkono hoja! (*Makofi*).

Mhe. Salim Abdallah Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana kweli kweli na mimi kupata nafasi ya kuchangia machache katika hoja hii binafsi ambayo wenzangu wengine hawaiungi mkono, mimi naunga mkono zaidi ya mia moja kwa mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, naona tunazungumza Katiba, naomba kwanza nisome kifungu namba 4 cha Katiba ya Zanzibar kwa ruhusa yako na kwa Kiswahili kama ifuatavyo:-

> "Katiba hii ni Katiba ya Zanzibar na itakuwa na nguvu za kisheria nchini kote na isipokuwa kutokana na kifungu cha 80 ambavyo ni vifungu ambavyo Baraza la Wawakilishi havina uwezo wa kuvibadilisha isipokuwa kwa kura ya maoni, ikiwa sheria yoyote itatafautiana na katiba basi katiba hii ndio itakayokuwa na nguvu na sheria hiyo itakuwa batili kwa kiwango kile ambacho kinahitalifiana".

Sasa Mhe. Naibu Spika, hii Katiba hii tukiacha hicho kifungu cha 80 kuna kifungu namba 7 cha Katiba, kifungu kidogo cha kwanza kinaeleza:-

Kila Mzanzibari aliyetimiza umri wa miaka 18 anayo haki ya kupiga kura katika uchaguzi unaofanywa wa Zanzibar na wananchi na haki hii itatumiwa kwa kufuata masharti ya kijifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki pamoja na masharti mengine ya Katiba hii ya Sheria iliyotungwa Zanzibar kuhusu mambo ya uchaguzi.

Mhe. Naibu Spika, hicho kifungu kidogo cha (2) kinasema hivi:-

> "(2) Baraza la Wawakilishi linaweza kutunga Sheria na kuweka masharti yanayoweza kumzuiwa Mzanzibari asitumie haki ya kupiga kura kwa kutokana na yoyote kati ya sababu za hapa chini zifuatazo:-"

Naomba nizitaje ili tuzijue Mhe. Naibu Spika, ijapokuwa tunazijua lakini na wengine wasikie. Nayo:-

1. Kuwa na uraia wa nchi nyengine

2. Kuwa na ugonjwa wa akili uliothibitishwa na Mahakama Kuu

3. Kutiwa hatiani na kuendelea kutumia adhabu kwa kosa jinai katika Chuo cha Mafunzo isipokuwa kwamba mtu aliyewekwa rumande atakuwa na haki a kuandikishwa kama mpiga kura

4. Kukosa au kushindwa kuthibitisha au kutoa kitambulisho cha umri, uraia, uandikishwaji kama mpira kura na kadhalika.

Sasa wapo wapo waandikishwaji wapiga kura hapa chungu nzima ilitokea wakati wote wakafutwa kwa kuwa hawana cheti cha kuzaliwa. Ni kwenda kinyume na Katiba. (*Makofi*)

Utambulisho wa umri wakati Tume ya Uchaguzi inapofanya kazi zake inashirikiana sana na Tume ya Uchaguzi ya Muungano. Mtu akiangaliwa tu kuwa unatimia umri wakati kishatimiza masharti mengine anaonekana huu ulazima

wa cheti *registrar* unatokea wapi. Kwa hivyo, sisi hao waliokuwa wakiandikishwa hapo nyuma sheria hizi zilikuwa zipo na wala hazijabadilishwa, zilizopita ni mbinu tu kupunguza wapiga kura. Hivyo tuseme tu lakini ukweli utabakia pale pale. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa ruhusa yako, kwanza naomba tena kuzungumza ili tujifahamu tunavyochangia Katiba yetu inatwambia nini. Kuna kifungu cha 12 ambacho kipo ukurasa wa 7(1) katika Katiba hii ya Zanzibar unaeleza hivi:-

> "7(1) Watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki bila ya ubaguzi wowote kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria."

Haufanani na wala sivyo na nitaeleza hapo baadae. Kundi moja likafanyiwa, kundi moja likadhalilishwa, hivi sivyo. Ninaendelea kwenye kidogo cha (2) kwenye Sheria Na. 12:-

> "(2)Hakuna sheria itakayokuwa na kifungu chochote ambacho ni cha ubaguzi wa moja kwa moja au kwa taswira yake."(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nikenda katika Sheria ya Vitambulisho kwenye Sheria Na. 6 inasema hivi na nitasoma kwa Kiingereza:-

> *"Duties of the Director of Registration."*

Yaani hapa ni wajibu wa Mkurugenzi wa Vitambulisho na hii inaeleza hivi:-

> *"Subject to the provision of this act and direction of the Minister, the Director shall register everyone"....* na kuendelea.

Yaani kutokana na sheria hii na maagizo ya Waziri, *direction* maana yake ni maelekezo ndiyo Mkurugenzi atafanya shughuli za vitambulisho.

Ninasema Mhe. Naibu Spika, tena kwa nia safi kama Mhe. Waziri anayehusikana atataka wananchi wapewe vitambulisho, *Wallahi* wote watapewa na kama hataki, hata tukafanya nini hapa watakuwa hawapewi lakini tujue kuwa tunawakosesha Wazanzibari haki yao ya Kikatiba. (*Makofi*)

Kujulikana kuwa una haki za Wazanzibari mbali hiyo iliyokusudiwa ya kuzuiwa kupiga kura. Mhe. Naibu Spika, Sheria hii ya Vitambulisho kuna Sheria Na. 15 naomba niisome ambayo ni ya marekebisho. Inasema:-

> *"The following act are hereby amendment:-*
>
> *(a)The Zanzibar act No. 5 of 1985 is hereby by amendment by adding section IV or immediately after section IV as follow".*

Section IV inaeleza habari ya uteuzi tu wa *Director*. Sasa kuna kifungu kidogo cha (4) kinajazwa kinasema hivi:-

> "*Any Zanzibaris"* Yaani kila Mzanzibari, *resident in* Zanzibar, mkaazi wa Zanzibar, *who has attained the age of eighteen years* ambayo kakamilisha umri wa miaka kumi na nane *and above* na zaidi ya hapo, *shall be registered and to be given an Identity Card which shall be issued by Director,* ataandikishwa kama ni Mzanzibari na atapewa kitambulisho, tena kitambulisho hicho atapewa na Mkurugenzi" Hivi ndivyo sheria inavyoeleza. *(Makofi)*

Sasa kwa nini kutokee watu wanaandikishwa, kwa nini kutokee watu hawaandikishwi na kwa nini tuunge mkono sheria ambayo ni ya udhalimu. Sasa Mhe. Naibu Spika, ninakwambia tena kuna Sheria Na.12(5) kinasema hivi, katika kifungu hiki neno "kubagua", maana yake ni kutimiza haja kwa watu mbali mbali hasa kwa kutegemea utaifa wao, kabila, ujinsia, ulemavu, mahala wanapotokea, mwelekeo wao kisiasa, rangi au dini ambapo watu wa aina fulani wanaonekana kuwa ni dhaifu na duni au wawekewe vikwazo na pingamizi ambazo wale watu wa aina

nyengine hawawekewi na wanapewa fursa na faida ambayo hawapewi watu wa aina nyengine. Katiba yetu inakataa hayo. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, sasa kama sisi ni waongo tukuleteeni hao watu. Mimi ninamuomba Mhe. Waziri twende Pemba jimbo baada ya jimbo, tumpelekee watu awaone. Hapa hapa Unguja wachalia mbali Pemba, tunakaa hapa tunawapotezea watu haki zao na sisi tuna muda wetu tutaondoka, tunafanya dhulma na sijui niseme vipi, lakini ni dhulma iliyokuwa haivumiliki. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nikupe taarifa kutoka kwenye jimbo langu.

Mhe. Naibu Spika: Bado dakika 5.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Ukinikata Mhe. Naibu Spika, unanionea na nitakubali. (*Kicheko*)

Mhe. Naibu Spika, jimbo langu katika mtu anayeshughulikia vitambulisho wala sikwenda kwenye CUF wala CCM, ni Wazanzibari kwa sababu mtu akishachaguliwa wote waliomo ni watu wake basi mimi ni mmoja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kwanza nililipa shilingi milioni mbili na thamanini elfu (2,080,000/=) kuwalipia Wazanzibari sitini na tano ili wakachukue vyeti vyao vya kuzaliwa na kila cheti kimoja nilikilipia shilingi elfu thalathini na mbili, walipata wachache tu siku ile Mkurugenzi aliyokuja, wengine waliopelekwa mpaka hii leo unafika mwezi wa sita hawajapata, wameshatoa pesa zao, siyo kidogo. Hii si dhulma ni nini na ukitaka majina nitakuletea. (*Makofi*)

Mimi ninasema tena wala sifichi Sheha wangu wa Mtambwe Kaskazini, kuna wananchi waliokuwa wameshatimiza masharti na wana vyeti vya kuzaliwa *registered* sitini wameshafika hivi, sasa wanaokwenda kwake wakirudi na kauli ni kuwa mimi siwezi kumpa mtu barua akenda akapigisha picha kupata kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi mpaka atoe elfu kumi na mbili. Na kama Mhe. Waziri anakataa na twende ijapokuwa hivi sasa na tutakwenda kumjuulisha huyu aliyemwambia. Hii si udhalimu ni nini. Kama Mhe. Waziri anataka Sheha angelifanya ujinga huo wa kumnyang'anya mtu haki yake. (*Makofi*)

Kuna Wazanzibari waliokuwa hawapungui kumi na moja katika Shehia ya Mtambwe Kusini. Hawa kila wanapokwenda huambiwa njoo kesho, njoo kesho wameshakamilisha kila kitu lakini Sheha kutoa barua hataki. Hiyo siyo dhulma ni nini, ni watu ishirini.

Kuna Wazanzibari kumi na moja Shehia ya Mzambarauni, kuna Wazanzibari kumi na saba Shehia ya Piki na sita Kisiwani, wote ni mia moja na kumi na nane wana vyeti vya kuzaliwa wametimiza masharti na wakenda wanahangaishwa hasa huyu Sheha wa Mtambwe Kaskazini, yeye kazidi hasa anasema lazima apewe elfu kumi na mbili na kama ninasema uwongo na twende mpaka hivi sasa na watu wenyewe wapo. (*Makofi*)

Halafu tukisema kuwa hakuna tunakusudia nini, tunawaambiwa wananchi uwongo kwa nini. Sisi hatukuja hapa kusema uwongo kwa sababu tunajua Kanuni inasema uzungumze jambo ambalo ni la ukweli, mukituita waongo munatuonea bure. Kwa hivyo mimi ninasema Waheshimiwa, ninaloomba kwa vyovyote itakavyokuwa sisi ni binadamu tumefanya mchakato tumekosea, turudi kwa Mwenyezi Mungu tujirekebishe tusiwanyang'anye watu haki zao. (*Makofi*)

Jengine Mhe. Naibu Spika, ambalo ni la kusikitisha sana kweli kweli.

Mhe. Naibu Spika: La kumalizia hilo.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Kuna watu Mhe. Naibu Spika, wachilia mbali hao waliokuwa wana vyeti vya kuzaliwa, kuna wengine mpaka leo wana risiti hawajapewa vyeti vyao. Mimi katika jimbo langu, watu ambao wameshapewa risiti ni mia mbili na nne. Risiti za vitambulisho kwenda kuchukua na mpaka leo hawajapewa hata mmoja, nenda kesho, nenda wapi, nenda wapi na keshokutwa ndiyo mwisho uandikishaji. (*Makofi*)

Pamoja na kuwa hutaki niendelee sana Mhe. Naibu Spika, ninakwambia la kusikitisha kabisa na Mhe. Waziri alikubali na akitaka majina nitampa. Akitaka watu *physically* nitamuonesha, *wallahi* kuna watu walikwishapewa hizi risiti wamekwenda kunyang'anywa bwana, wanaonekana hawa kumbe tulikosea walinyang'anywa na wao wakawa

waoga wakazitoa. Majina ninayahifadhi lakini ninayo na akiyataka nitampa na akitaka twende pamoja tutakwenda. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, hukunipa nafasi lakini ninaloomba hebu tuwe wakweli, sisi ni watu wazima, sisi tumechaguliwa hapa kwa kupitia vyama lakini lengo letu ni kuwaletea haki wananchi. Haya mambo ya kukaa hapa kichama, huyu anasema ndiyo, huyu siyo hayatufikishi popote. Wananchi wanatusikiliza wanaokosa haki zao wapo pale pale na siku zote ukweli utabakia kama ulivyo ukweli.

Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana tunakushukuru na wewe. Sasa jamani tujali muda bado wachangiaji wengi. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad afuatie Mhe. Marine Joel Thomas baadae Mhe. Asha Abdu Haji na Mhe. Mgeni Hassan Juma.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote na mimi ninachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia jioni hii kuwepo hapa na kuendelea na ule ule utaratibu wetu wa kazi zetu za kuwatetea wananchi wetu pamoja na kuipa ushauri na kuielekeza Serikali, ili iende vyema katika kutekekeleza majukumu yake.

Mhe. Naibu Spika, la pili ninapenda kukushukuru wewe kunipa nafasi hii angalau na mimi kupata dakika chache za kuweza kutimia na mimi maelezo yangu juu ya hoja iliyopo mbele yetu. Lakini pia nisiwe mchache wa fadhila nimpongeze sana Mhe. Hamad Masoud Hamad kwa makusudi juu ya hoja yake binafsi kwa ajili ya kilio ambacho kipo kwa muda mrefu, na kikubwa sana kwa wananchi wetu kunyimwa au kusumbuliwa sana katika utaratibu mzima huu wa kupata vitambulisho vya Uzanzibari.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mimi ninaamini kwamba wote ni wakosa ni kweli kabisa kabisa, lakini mkosa mwema ni yule ambaye anajirekebisha baada ya kujua kosa lake. Kwa hivyo ninaiomba Serikali juu ya hili ilipe nafasi kubwa sana ili kilio hiki cha Wazanzibari walio wengi kifanyiwe dawa. Ninaamini kwamba watu wengi katika Shehia zetu, kwenye majimbo yetu na Zanzibar yetu wanapata matatizo miongoni mwao kuhusiana na suala zima hili la ufuatiliaji wa kupata vitambulisho vya Uzanzibari Mkaazi.

Mhe. Naibu Spika, ninashukuru kwamba kuna wengi katika wachangiaji wametoa vielelezo tosha kuonesha kwamba hii kadhia ipo na wala haizungumzwi tu kwa kubuni, bali inazungumzwa kwa vielelezo ambavyo vipo. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli niishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na yote tuliyonayo, Serikali chini ya Baraza hili imekuwa ikizungumza mambo mbali mbali ambayo yanakuwa ni kero na Serikali inakubali kuwepo kwa kero hizo. Lakini tunashindwa au Serikali inashindwa kufikia maamuzi muafaka kwa wananchi juu ya kero ambazo zinakuwepo.

Mhe. Naibu Spika, kero nyingi zimetajwa, tokea zilipokuwa zikiundwa kamati mbali mbali, zikiwemo Kamati Teule na kamati nyengine za kisekta ambazo zinatoa maelezo mbali mbali na kasoro mbali mbali, kubwa na zito juu ya watendaji mbali mbali ambao wanarudisha nyuma na wanakwaza mambo mbali mbali ya faida yanayopatikana katika nchi hii. Lakini tunanyamaza kimya.

Ndio maana Mhe. Hamad Masoud Hamad akaleta hoja hii kwa sababu ya kero hizo hizo ambazo zinaenea katika maeneo yetu. Mhe. Naibu Spika, zamani kulikuwa na vitambulisho, walikuwa wanaita wenyewe pasi ya uraia. Mhe. Naibu Spika, pasi ya uraia ilikuwa ni kitambulisho vile vile cha Mzanzibari.

Pasi hii walikuwa wakitakiwa wananchi watembee nacho katika maeneo yao tofauti wanayokwenda. Na vituo vya Polisi zilipokuwa zikipita gari za abiria na mpaka leo mabango yale yapo, gari ya abiria simama kwa ajili ya kupekuliwa na Polisi. Miongoni mwa masuala ya Polisi waliyokuwa wakiuliza kitambulisho cha pasi yako ya uraia unayo, ninayo toa, anatoa mzee mfukoni anaonesha anaambiwa haya, ambaye hana pasi ya uraia Polisi walikuwa wanamshusha kwenye gari na baadae wanamuhoji.

Sasa Mhe. Naibu Spika, katika hoja ya Mhe. Hamad Masoud Hamad kwenye ukurasa wa pili imeeleza hapa na kwa kuwa kwa mujibu wa kifungu cha 14 (1) (a) cha Sheria Na. 7 ya 2005 niliyoitaja hapo juu ni kosa la jinai kwa Mzanzibari Mkaazi aliyetimiza sifa na masharti yaliyotajwa kwenye sheria kutokuwa na kitambulisho cha *Zan-ID*.

Kosa ambalo likithibitika adhabu yake ni faini isiyopungua shilingi laki moja au kifungo kisichopungua mwaka mmoja au vyote viwili faini na kifungo.

Mhe. Naibu Spika, sheria hii imetungwa muda mrefu na mpaka leo sheria hii haijafutwa ipo. Labda mimi ningeuliza tu. Ni Wazanzibari wangapi ambao wamefungwa au wangapi wamepigwa faini kwa kukosekana kuwa na kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi. Mhe. Naibu Spika, ikiwa sheria hii haijachukua nafasi yake, mimi ningeiomba Serikali au ningeiomba Idara inayohusika na masuala haya kuanzia leo ifanye kazi ya kuwahoji, kuwasaili pamoja na kuwachukulia hukumu za kisheria zile zilizotajwa katika sheria hii, ili yule ambaye hana kitambulisho cha Mzanzibari akaeleza sababu zake za msingi zilizopelekea kukosa kitambulisho.

Mhe. Naibu Spika, lakini vitambulisho hivi kuwa tunavitaja tu katika mazingira yetu tofauti bila ya kuchukuliwa hukumu ya aina yoyote, basi bado sheria hii hatujaitendea haki.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba tatizo lipo. Mimi baada ya kutoka hapa katika Baraza hili, nilikwenda eneo la Darajabovu, pale tulifiliwa hivi juzi, nilikwenda kuonana na jamaa ambao tulipata msiba. Lakini pale nimekutana na baadhi ya watu ambao walikuwa wanaisikiliza hoja yetu tokea asubuhi. Kuna rundo hili la vyeti kopi hizi, la vyeti vya kuzaliwa ambavyo vyeti hivi watu wanakwenda kwa Sheha kupewa fomu ya kwenda kutafutia vitambulisho lakini, lakini wanapigwa danadana njoo kesho njoo keshokutwa, njoo Jumatano njoo tarehe 7. Mhe. Naibu Spika, hili ni tatizo na watu wananyimwa vitambulisho wala hili sio jambo la kubuni ndio ukweli halisi ulivyo.

Mhe. Naibu Spika, katika Jimbo langu la Chambani, watu wanapigwa danadana. Hivi karibuni kuna watu wengi wamekwenda katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya pale katika Idara hii ya Vitambulisho na vyeti vyao vya kuzaliwa wengi tu, lakini kila cheti cha kuzaliwa wanachopeleka wanaambiwa cheti hicho ni *fake*.

Mhe. Naibu Spika, vyeti hivi *fake* vinapatikana wapi na kwa nini idara inayohusika na utoaji wa vyeti haichukui hatua juu ya suala hili la vyeti *fake*. Vyeti vya kuzaliwa kuna muhuri ambao tunauita muhuri wa moto, hivi mtu wa Chambani ataupata wapi muhuri ule wa moto na kama kuna watu wanatoa vyeti *fake* mihuri hii wanaipata wapi.

Kwa hivyo, tunaiomba serikali iwe makini sana juu ya suala hili na kwa kweli kama kuna watu ambao wanatoa vyeti fake basi serikali iwachukulie hatua, isiwapotezee watu wetu muda, isiwapotezee watu wetu fedha za kwenda na kurudi. Mtu mchana mzima anaitafuta shilingi 1,000 tu ya kutafutia dagaa au kitu chengine inamshinda. Kutoka Chambani kwenda Mkoani kwenda na kurudi nauli yake ni shilingi 3,000, kazi ya mtu wa Chambani ya kupata shilingi 3,000 kwa siku siioni mimi.

Kwa hivyo, tunaomba mamlaka inayohusika kwa kweli iweke mazingira mazuri ili ihakikishe kwamba masuala haya ya vyeti fake yanachukuliwa hatua na watu kupata vyeti ambavyo ni sahihi, ili kuwaepushia watu ule usumbufu wa kwenda na kurudi pamoja na kupewa vyeti bandia ambavyo havistahiki kuwa ni vyeti ya kuzaliwa sasa hivi.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba tumefika pahala ambapo kama hatukuwa makini, basi nchi yetu tunaweza tukaipeleka pahala pabaya sana. Mhe. Naibu Spika, naishauri sana serikali kwa hali yoyote iangalie utaratibu gani wa kufaa, ili kuvizima vilio hivi vya walio wengi juu ya kadhia ya kunyimwa vitambulisho vya Uzanzibari Ukaazi.

Mhe. Naibu Spika, kwa mchango wangu huo na kwa taa yako hiyo ambayo umeiwasha, niseme mimi nitakuwa miongoni mwa wale wanaoiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Mjumbe kwa kujali muda. Sasa nafasi tunampa Mhe. Marina Joel Thomas, baadaye Mhe. Asha Abdu Haji, halafu Mhe. Mgeni Hassan Juma na baadaye Mhe. Subeit Khamis Faki.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia hoja binafsi ya Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, Mhe. Hamad Masoud Hamad, ya kuhusiana na kutaka serikali kuchukua hatua za kuwatimizia Wazanzibari wote waliotimiza sifa za kisheria haki yao ya kuwapatia vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi.

Mhe. Naibu Spika, kwanza siungi mkono hoja hii na ninasema siungi mkono kwa sababu Mhe. Naibu Spika, sheria zipo wazi, utaratibu upo wazi ni muhimu kufuata sheria na taratibu zilizowekwa.

Nikitoka hapo Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mkurugenzi wa Usajili wa Vitambulisho vya Mzanzibari. Mkurugenzi huyu anafanyakazi nzuri ni ngumu lakini anatekeleza majukumu yake ipasavyo, pamoja na watendaji wake wote wanastahili pongezi na sifa. Nawapongeza pia Masheha kwa kusimamia majukumu yao ipasavyo, Masheha ndio wanaowajua watu wanaokaa katika maeneo yao, kwa hivyo nawapongeza kwa kazi hiyo.

Mhe. Naibu Spika, nimesema sheria ipo wazi, kwa sababu sheria hii ambayo imetaka kuanzisha Ofisi ya Msajili na Kadi ya Vitambulisho ilipitishwa hapa Barazani Mhe. Naibu Spika, mwaka 2005. Katika sheria hiyo Mhe. Naibu Spika, ilimtaka kila mtu mwenye umri wa miaka 18 na kuendelea akajiandikishe, ili apate kadi za utambulisho wa Mzanzibari.

Sheria hiyo Mhe. Naibu Spika, ya mwaka 2005 sheria namba 7, imeeleza pia sifa za kuwa nani ana haki ya kupata utambulisho, sifa zote zimeeleza. Pia sheria hiyo hiyo Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 13(1) imeeleza kama mtu hakuridhika na maamuzi ya Mkurugenzi anayo haki ya kukata rufaa. Sasa tatizo likowapi. Mtu hakupata haki kwa nini asifuate taratibu zilizowekwa katika sheria hii, kwa nini asikate rufaa akapeleka sehemu inayostahiki akapata haki yake, kuliko tunakaa tunalalamika huyu kanyimwa. Mtu anakuja na vyeti anasema huyu kanyimwa haki, kwa nini asifuate taratibu ambazo zimewekwa katika sheria hii na sheria tumeipitisha hapa katika Baraza lako tukufu Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, tumewasikia mawaziri katika majumuisho yao ya Tawala za Mikoa, Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ alisema kuna vitambulisho vingi, karibu zaidi ya laki tatu au laki mbili hapa vimekaa havijulikani wenyewe, vitambulisho ni vya nani na pia kuna tatizo la vyeti vya kuzaliwa fake, nani anafanyakazi hiyo.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, taratibu zinakiukwa na zikifuatwa taratibu Ofisi ya Usajili wa Vitambulisho vya Mzanzibari, haina wasi wasi wowote inatoa haki yake kwa yule mtu ambaye atafuata taratibu zilizowekwa na sheria.

Mhe. Naibu Spika, Sheha ni kiongozi wa serikali, ni kiongozi wa ngazi ya chini ya serikali na Sheha kawekwa kwa mujibu wa sheria ya Tawala za Mikoa. Sheha huyu ndiye anayewajua wananchi wake wote ambao wanakaa katika eneo lile, na ndio maana mtu akitaka kitambulisho cha Mzanzibari anatakiwa apite kwa Sheha, apate barua ya Sheha ili aipeleke katika Ofisi za Usajili wa Vitambulisho za Wilaya. Lakini mkaazi huyo pengine kahamia pale katoka kwenye Shehia nyengine, hajenda kuripoti kwa Sheha na moja ya majukumu ya Sheha kufuata sheria na taratibu zilizopo, kufuata miongozo na pia kukusanya takwimu mbali mbali za Shehia.

Mhe. Naibu Spika, ukenda kwa Sheha kuna *register* ya Shehia, *register* hiyo inakusanya mambo ya vizazi, takwimu ya vizazi, takwimu ya vifo, kuhama na kuhamia katika Shehia. Mtu yeyote anayetakiwa kukaa katika Shehia ametoka katika Shehia nyengine basi anatakiwa aripoti kwa Sheha na akiripoti kwa Sheha anatakiwa atoke na barua ya kule ambapo anatoka. Lakini sisi tatizo letu hatufuati taratibu hizo, tunakaa tunawalaumu Masheha hawafanyi kazi zao. Lakini kwa kiasi fulani na sisi wananchi hatufuati taratibu na sheria. Mtu anahamia kwenye Shehia mpya miaka miwili kakaa kimya, anapopata tatizo ndio anamjua Sheha. Sio utaratibu huo, tunawalaumu bure Masheha hawa Mhe. Naibu Spika. Masheha wanafanyakazi zao vizuri kabisa.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala zima wajumbe wanasema vitambulisho vinatolewa kwa Mmasai, Wamakonde. Ndio watapata haki hiyo, kwa sababu Mmasai anafanyakazi kwenye hoteli miaka 10, 20 au miaka 6, na pengine anakaa katika eneo lile karipoti kwa Sheha. Kwa hivyo, katimiza sheria ya ukaazi Mhe. Naibu Spika.

Kwa hivyo Mmakonde ana haki ya kupata kadi ya utambulisho, Mmasai, Mruguru, Mnyamwezi kama katimiza sheria ya ukaazi ana haki, katimiza miaka mitatu mfululizo katika Shehia ile ana haki.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia naomba nisipoteze muda wako, *Zan-ID* sio mtaji wa kisiasa kama wenzangu walivyosema, sio mtaji wa kisiasa wa Chama cha Mapinduzi, hii ni haki ya kila Mzanzibari, sio kama ndio mtaji wa Chama cha Mapinduzi, hapana. Hii ipo kisheria na kila Mzanzibari ana haki ya kupata kitambulisho cha Mzanzibari, mradi anafuata taratibu na sheria zilizopo.

Kwa kumalizia Mhe. Naibu Spika, siungi mkono hoja hii, kwa sababu taratibu na sheria ziko wazi. Wananchi tunatakiwa tufuate taratibu na sheria zilizowekwa katika sheria hii ambayo imeanzisha Ofisi ya Usajili na Utambulisho wa Mzanzibari. Ahsante Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Asha Abdu Haji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa hii kuchangia hoja hii binafsi ya mjumbe. Kwanza kabisa naunga mkono asilimia mia juu ya mia hoja hii. *(Makofi)*

Kwa kweli kwa kuwa vitambulisho vya *Zan-ID* ni vitambulisho vya haki ya kila Mzanzibari na kwa kuwa vitambulisho hivi Mzanzibari ambaye keshatimiza umri wa miaka 18 na kila jambo keshakwenda kwa Sheha, keshapewa barua na kila kitu, lakini kwenda Wilayani hapati kitambulisho, kila siku nendarudi nenda rudi na hii ni haki ya kila Mzanzibari apewe kitambulisho cha Mzanzibari, wakati keshatimiza umri wa miaka 18.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa vitambulisho vya *Zan-ID* anapewa mtu ambaye katimiza umri wa miaka 18, najiuliza kwamba hawa watoto ambao wanakwenda kupiga kura, ambao hawajatimiza umri wa miaka 18, vitambulisho hivi wamevipata wapi na huwezi kupata kitambulisho cha kupigia kura bila ya kupata kitambulisho cha *Zan-ID*, kitambulisho hiki namuuliza Mhe. Waziri wanavipata wapi watoto hawa ambao hawajafikia umri wa miaka 18. Ushahidi ninao na watoto wangu binafsi ninao, na wako ambao wameshapiga kura hawajatimiza umri wa miaka 18, jamaa zangu nawajua wanapiga kura hawajatimiza umri wa miaka 18 na wanachukuliwa na ushahidi ninao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hebu mpeni raha mchangiaji.*(Makofi)*

Mhe. Asha Abdu Haji: Sasa Mhe. Waziri mtaniuliza maana yake wako upande wa kwenu. Suala hili vitambulisho havijatolewa kwa upande wa wageni. Kule kwetu kuna wageni wengi ambao ni wa upande wa Tanzania Bara, wageni wale wakikaa wakifika muda kama wa miezi miwili wanapewa vitambulisho vya ukaazi na sio haki yao kupewa vitambulisho vile, ni haki ya wakaazi Wazanzibari, Wazanzibari wenyewe hawapewi vitambulisho vile kwa sababu gani?

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri akija hapa hoja hii akijibu basi anijibu swali hili kwamba kwa nini wanapewa watoto vitambulisho vya kupigia kura na vitambulisho vya ukaazi, lakini hawapewi watu ambao wameshatimiza umri wa miaka 18. Naunga mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, nimshukuru Allah Muumba Mbingu na Ardhi aliyetujaalia uzima na afya. Lakini nikushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii adhimu na mimi kuweza kuchangia hoja binasi ya Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi wa Jimbo la Ole Mhe. Hamad Masoud Hamad, inayozungumzia suala la kuitaka serikali kuchukua hatua za kuwatimizia Wazanzibari wote waliotimiza sifa za kisheria, haki yao ya kuwapatia vitambulisho vya Mzanzibari.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza nimejiuliza na ninajiuliza na ningemtaka mjumbe anifahamishe vizuri, kwa nini hoja hii imekuja katika wakati huu. Kwa nini hoja hii ambayo kwa kipindi kirefu masuala haya tumekuwa tunayazungumza, lakini kwa nini ameona muda huu ndio muda muafaka wa kuileta hoja hii Barazani.

Mhe. Naibu Spika, wengi wamechangia na wengi wamezungumza, lakini kinachojitokeza kwamba sheria zinazompa haki Mzanzibari kuweza kupata kitambulisho zipo na ziko wazi kabisa na wala hazina utata. Hata kama wakati huo wa kale ambapo vitambulisho hivi vilianzishwa kuna baadhi ya wananchi waliambiwa wasiende kujiandikisha. Lakini leo tumeona umuhimu wa kuwa na vitambulisho na sio jambo la ajabu, kwa sababu dunia nzima kila mtu anatakiwa awe na kitambulisho ili atambulikane yuko wapi na sasa ni nani. Lakini sasa tumeona umuhimu wake na umuhimu wake unajitokeza katika mambo mbali mbali. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hofu yangu kubwa ni kwamba suala hili tunaliingiza katika siasa na hilo linanifanya mimi kuikataa hoja hii. Kwa sababu sheria ipo na yeyote ambaye atatimiza vigezo vinavyostahili atapewa kitambulisho, sheria inasema kanuni ya 3 na 4 nambari 7 ya mwaka 2005 kwamba Mzanzibari mwenye sifa za sheria ya kujisajili, anaweza kujisajili katika wilaya wanazoishi na baadaye kupata uthibisho wa Sheha.

Mhe. Naibu Spika, sheria nambari 7 ya mwaka 2005 ya kifungu 13(1), inampa fursa yule ambaye amenyimwa kitambulisho aende mahakamani ili aweze kupata haki yake. Sasa nauliza tena na naomba nimuulize anayetoa hoja.

Hivi ana kumbukumbu ngapi mpaka kutimia mwaka 2015, ni watu wangapi Wazanzibari ambao wamekwenda kudai haki zao mahakamani kuhusiana na vitambulisho.

Mhe. Naibu Spika, nauliza hivyo kwa sababu sote sisi ni wanasiasa na hapa sio jukwaa la kutafutia kura, sisi ni *policy makers* kazi yetu ya kutunga sheria tumeshaifanya, lililobakia ni utekelezaji. Sasa utekelezaji huo utafanywa kutokana na sheria zilizokuwepo. Sasa sisi hapa hatuna nafasi katika hili na ndio maana nikasema kwamba isiwe hapa ndio kiriri cha siasa, kwamba kila mmoja hapa.

Tunajua kipindi hiki sote tuko taabani, tunakimbilia, kila mmoja anataka nafasi yake aikamate. Kwa hivyo, hii isiwe ni *issue* ya vitambulisho, hapana. Mimi ningemuomba sana mtoa hoja na wengine, kama kweli haya ambayo wanayoyazungumza wanayaamini basi wafuate sheria. *(Makofi)*

Jengine Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha miaka miwili na nusu nilikuwa kwenye Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa na tuliwahi kwenda Pemba, tulipokwenda kule tulikuta vitambulisho vingi bado havijachukuliwa. Je, suala hilo Mhe. Naibu Spika, mtoa hoja analijua, naomba atuambie hao ambao hawajapata hivyo vitambulisho vyao anachukua hatua gani ya kuhakikisha vitambulisho hivyo vinawafikia, hilo ni jengine.

Kwa kuwa mimi najua kwamba haki hii ni ya kila Mzanzibari, mimi ningeiomba sana Serikali na wengine wamezungumza suala la vyeti feki na kuna mjumbe mmoja alisema kwamba kwa kuwa kuna nembo ya Serikali katika vyeti hivyo inakipa uhalali kile cheti kuwa ni cheti halali, nakataa. Nakataa viko vyeti ambavyo si halali vya kuzaliwa, vipo tena ni vingi sana vinatengenezwa kama njugu tunaviona hakuna kitu ambacho sasa hivi kutokana na utaalamu tuliokuwa nao inashindikana kufanyika. Kwa hivyo kuwepo nembo ya Serikali hazifanyi cheti kile kuwa halali, hata siku moja.

Sasa ningeiomba Serikali umeshafika wakati wa kutafuta vitendea kazi maalum vitakavyoweza kubainisha vyeti vile ambavyo sio halali. Hili ni tatizo moja sio kila mtu mwenye cheti chake ambacho kakitengeneza vichochoroni kitaweza kumsaidia kupata kitambulisho cha Uzanzibari, lazima Serikali ijikite katika hili ili kuondoa hiyo migogoro.

Mhe. Naibu Spika, mimi nafikiria nimeshasema ambayo ilikuwa lengo langu hasa kuitaka Serikali zaidi kusimamia suala zima la vyeti ambavyo tunavyo katika mitaa yetu, ambavyo kwa kweli vitatuletea matatizo makubwa. Tunafahamu kwamba kitambulisho cha Mzanzibari ni haki ya Mzanzibari, kila Mzanzibari akiwa na sifa.

Kwa hivyo, naiomba Idara inayohusika watimize wajibu wao lakini na sisi kama binaadamu jamani sisi hapa hatukuja kuhukumiyana, kila mmoja kakamata msahafu kwa upande wake, na kila mmoja ana imani yake. Tunapoanza kumpeleka kila mmoja wetu kwa Mungu sote tunamjua Mungu vilivyo. Tumelelewa katika misingi ya imani ya dini sote kila mmoja ana imani yake, tusipelekane kwa Mungu kwa sababu ati vitambulisho wengine hawapati, lakini tuombeyane Mungu kama kuna makosa basi yarekebishwe, hilo ndio la msingi.

Pia tuliombee kwa Mungu taifa letu, tuwe na amani na upendo hilo ndio la msingi tusisomeyane halbadiri wala tusiapizane tunapokwenda ni pafupi na sote tutakwenda, hakuna atakayebakia, na sote tutahukumiwa. Mheshimiwa nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, jioni hii ya leo kunipa na mimi fursa ya kuchangia hoja binafsi ya mjumbe kuhusu sula la vitambulisho. Ukweli kwanza utabakia kuwa ukweli na kitu kilichokuwa hakina ukweli hata ukikizika ardhi ya saba kitakuja juu na kitaonekana. Suala hili tumeshapiga kelele sana zaidi ya bajeti sita zilizopita. Kuingia tu, kwanza hili suala halikuanza leo, limeanza zamani na bila ya kufichana huu ni mtaji wenu, wakubwa huu ni mtaji wenu na mtaji wenu hamuwezi kuung'amua kwa sababu huu ni mtaji wa viongozi. Kwanza masheha tunawalaumu sana, ni kweli tunawalumu masheha.

Masheha wanapokea amri kutoka juu lazima tuambizane ukweli, hapa tuliondoka na Mhe. Waziri Mhe. Mwinyihaji Makame mara ya kwanza tulipokuja tukasema humu barazani, bahati nzuri Baraza la Wawakilishi ndio kinywa au ndio mdomo wa wananchi wa kusemea; leo tunaambiwa tukaseme Mahakamani, wakati mwa kusemea ni humu Baraza la Wawakilishi na Baraza la Wawakilishi ndilo linaloona kama sheria hii haifai inataka marekebisho, tunakuja tunasema kwamba sheria hii inawakandamiza wananchi inataka marekebisho.

Leo mnatwambia tuende Mahakamani na wakati Baraza la Wawakilishi ndio mdomo wetu wa kusemeya Mhe. Naibu Spika, suala la vitambulisho tunapiga kelele na halikwamuki kwa sababu ni mtaji wa watu wakubwa hili suala hili, tukitaka tusitake limeingizwa kwenye siasa kwa makusudi. Kwa sababu vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi vilikuwa havimo kabisa kwenye suala la uchaguzi na ndivyo tulivyoambiwa kwanza.

Baada ya kuona wakubwa kwamba mtaji huu ndio tunaowashinda kwa kuwafunga bao, ndio maana vimeingizwa katika suala la uchaguzi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nina *photocopy* za vitambulisho vya watu ambaokuwa wameshapiga picha, washapewa risiti, maana nyie mkikaa mnasema kwamba ipo sheria ifuatwe tatizo sheria haifuatwi na wanaovunja sheria ni nyie, kwa sababu mtu kama kashakwenda kashatoa cheti cha kuzaliwa kashathibitishwa, kashakaa kitako kashapiga picha amebaki kupewa kitambulisho chake mnataka sheria gani tena ifuatwe.

Mtu ameshafanyiwa kila kitu bado kupewa kitambulisho hivi linalokwamisha kupewa ni nini na wakati mwezi wa saba huu zaidi ya mwezi wa saba wengine mimi binafsi nina mtoto wangu binafsi, amekwenda na cheti sio feki anacho nimemchukulia mimi mwenyewe kapiga picha amekwisha mwezi wa nane huu hapewi kitambilisho, kuna tatizo gani, sheria gani mnayotaka ifuatwe.

Leo mnasema watu wote waende Mahakamani, hivi humu Spika ni mmoja sio sote ni maspika humu, hivi watu wote mnaona wanajua sheria. Nyie hivyo mkitizama watu wote wanajua sheria, kuna watu tunasema kila siku hapa kuna watu ambao kuwa wanafanya uhalifu wa kuwabaka watoto watu wanashindwa kutoa ushahidi kwa sababu ya kutojua sheria. Kwani linalofanya asitoe ni nini, si kutojua sheria.

Hivi mnawafanya watu wote ni mashehe humu au mnawafanya watu wote wanajua sheria, leo mnawakandamiza watu kwa makusudi kwa sababu ya mtaji wenu wa kujifaidisha kisiasa. Mnasema watu waende Mahakamani, haya mtu kama huyo aende Mahakamani akafanye nini tena, ameshapiga picha kashakwisha anakwenda kusemaje huko Mahakamani, anakwenda kufanya kitu gani hata apewe.

Leo mnasema akamshitaki Mkurugenzi, Mkurugenzi ndio mwenye vitambulisho vyote amevizuia yeye kwa sababu zisizokuwa na msingi ukifika unaambiwa mashine ni mbovu hupigi picha, una vyeti vyako kamili, basi vyeti vya kuzaliwa vimekuja kuwa feki vyote hivi sasa hakuna kizima maana hakuna kizima vyote ni feki. Jamaa zanguni hivi sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatoa vyeti feki vyote kwa sababu tuna watoto tunaowazaa kwa umri wanachukua vitambulisho ndani ya wilaya zao, wameshafikia umri sasa leo wakifika mnawaambia ni feki, feki hizo zinatoka wapi.

Ni feki kwa faida yenu wakubwa na huu ni mtaji wenu kama ni mtaji hamuwezi kuung'amua twambieni ukweli humu jamaa zangu. Hili suala tumeshasema sana na linatuuma kwa sababu mnawazuia watu haki zao pasina sababu na vitambulisho kila leo mnatoa mnazuia nusu tu sasa hivi mmetugawa madaraja Zanzibar, kuna wananchi wa daraja la kwanza na wananchi wa daraja la pili, huo ndio ukweli mmetugawa matabaka.

Kuna watu wa CCM daraja la kwanza, CUF ni daraja la pili ndivyo mnavyotufanya hata mtu awe Unguja gani akiwa ni CUF huyo ni Daraja la pili jamani mnatupeleka pabaya viongozi wetu. Tunasema humu Barazani ndio mnamorekebishwa sheria, msituone kama tunakuja kupayuka tu humu. Hivi si haki mnayoifanya mnawazuia watu haki zao, masharti mtu kashatimiza yote kuna sababu gani ya kuzuiliwa hivi vitambulisho mnavyovizuia, watu washapiga mnavizuia kwa nini na ni haki zao.

Washapiga picha wana risiti za kuchukulia ndio masharti hayo, ana cheti cha kuzaliwa kwa sababu watu wanasema ukila na kipofu usimshike mkono. Mungewazuia wale ambao hawana vyeti vya kuzaliwa sawa ndio sheria inavyosema hana ushahidi wowote ule sawa. Lakini ushahidi wote huu mtu jamani mnamzuia kashakuja na cheti chake hiki kashapita picha mwezi wa nane huu hamuwapi vitambulisho halafu tukija tukisema humu mnatuona wapumbavu. Jamaa zanguni sivyo mukiambiwa kama tunarudi kwa Mungu mnasema mnasomewa halbadiri, tutasoma hata siamwi wacha halbadiri.

Mhe. Naibu Spika, tutafanya itikafu hasa kama Mwenyezi Mungu atatupokelea tutakwenda misikitini tuweke itikafu ili mwenye haki yake Mwenyezi Mungu yule anayemnyima haki yake ambainishe, leo mnatwambia tunasoma halbadiri tunasema hapa mnatuona wapumbavu mnapiga kofi mnatujejea, mnasema tuende Mahakamani mbona

nyie hamuendi Mahakamani mnawapa watu wenu, mmewapa watu mawilayani mmewapa huko Sheha mnamwambia hivi ata tukiondoka tunakwenda pamoja na sisi tukirudi mnakwenda kuwaambia vyengine.

Jamaa zanguni watu hawajafika umri sasa hivi mnawatatiza ukienda Mawilayani manawatatiza watu wasiofika umri wala hawataki cheti cha kuzaliwa, wanapewa tu. Lakini sisi tukija humu tukisema mnamcheka Asha Abdi kwa kuwa kasema kuna watoto ambao anasema wanawe hawajafika umri, mwanawe si lazima amzae yeye hata wa ndugu yake ni mwanawe, wa jirani yake ni mwanawe.

Jamaa zangu sivyo tunakwenda kubaya mnaturudisha kule kule nyuma tulikorudi, tulikuwa tumetulia mnaturudisha tu, tumekaa kitako humu tumefanya Serikali ya pamoja tuaminiane tusaidiane ndio mwanzo tunakandamizana. Jana wamepigwa watu mapigi pale mnaturudisha kule nyuma tulikotoka. Wamepigwa watu wameumizwa wametolewa macho, wametolewa pua, jamani mnatupeleka.
Mhe. Naibu Spika, mimi nasema tena jamani Waheshimiwa nawasihi tena Mhe. Waziri unayehusika na vitambulisho pamoja na Serikali Mhe. Makamu wa Pili wa Rais pamoja na Serikali yote tunawaomba sana chonde chonde mwenye haki yake apewe. Jamani nawasihi aliyekuwa hana haki asipewe lakini mwenye haki yake apewe.

Leo kama mtu kashapiga picha kila kitu kashakamilisha kuna sababu gani ya msingi asipewe na ni watu wengi hawa zaidi ya watu 30,000. Mie jimboni kwangu zaidi ya watu 200 na wanao vyeti vyao vya kuzaliwa vilivyokuwa kamili zaidi ya 200 na hawa ndio ni wa hapa Jimbo la Mkwajuni, hao jimbo la Mkwajuni hapa Unguja kwa sababu wanaonekana tu hawa labda wanaelekea upande huu tayari hawapewi.

Hawa wa Jimbo la Mkwajuni 40 wanao vitambulisho *photocopy* wanakuja nazo hizi hapa hawa ni arubaini hawa na vyeti vya kuzaliwa hivi hapa 45, hawa hakuna sababu hata moja ya kuzuiliwa. Masharti gani tena mnayoyataka Mheshimiwa hivi hapa, kama unataka njoo uchukue nisijekuwa nasema tu shika mpelekee ushahidi huu hatusemi tu, hatupayuki humu, hatuji kupiga makelele tu humu tunakuja kwa ushahidi halafu mnakanusha basi ukweli hata mkikanusha wananchi wanajua ukweli uko wapi.

Musikanushe bure humu mukaiona hii hoja mnaififiza tu haififii, wananchi wanajua ukweli mtawanyima kwa sababu sasa hivi mna nguvu tu basi, nguvu mnazo lakini inashaallah na sisi tutakaa Mwenyezi Mungu akipenda tutaitikafu misikitini tutaomba dua haki ipatikane Mhe. Naunga mkono hoja *(Makofi)*

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia hoja hii ambayo imeletwa na Mhe. Hamad Masoud Hamad. Kwanza Mhe. Naibu Spika, nasema hoja hii mimi sitoikubali kwa sababu haikufuata sheria ya kuweza kufika katika Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, mhusika aliyeleta hoja hii kwa taarifa mimi ni mgeni katika baraza hili lakini nina taarifa kwamba ameanza katika baraza hili tokea mwaka 1995 yumo katika Baraza hili, nilitaka kumuuliza kwanza ni mara ngapi ameleta sheria hii ndani ya Baraza la Wawakilishi kama alikuwa bado hajaleta kwa nini alete miaka hii baada ya kukaa mara tano katika Serikali. Ni mara yake ya kwanza kuweza kuhakikisha kwamba hivi sasa inahusika kuingia katika Baraza hili haoni hilo ni kosa au uchochezi ambao anauanza katika mwaka huu wa 2015.

Wakati tunajua kwamba wao wameshahakikisha kwamba 2015 uchaguzi usiwe uchaguzi iwe ni balaa, hiyo naona kwamba hakutumia haki yake ambayo alikuwa aitumie tangu miaka ya nyuma ili kulihakikishia Baraza kwamba kuna makosa yanafanyika. Sasa nataka kujua kosa hili ndio kwanza alione leo au ndio kwanza alipate leo.

Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, ninavyoelewa mimi kila mwananchi ana haki ya kupata hiki kipande cha Mzanzibari na kweli wanapata haki zao, lakini haki hii ilikuwa aifuate kwa mujibu wa kila mwananchi anakotoka katika shehiya yake na ndio anakoweza kupata kipande cha Mzanzibari. Sasa hivi utashangaa kwamba kuna vijana wengi wanaomba vitambulisho lakini anakokaa au anakotoka hakuomba kitambulisho kile, anakwenda kuomba shehiya nyengine ambayo sio yake, sasa hapo ametumia njia gani ya kuweza kupata haki yake.

Mheshimiwa Muwakilishi mwenzangu hapa yeye anasema anafuatilia Mkwajuni yeye ni Muwakilishi wa Mkwajuni, alishindwa kutumia haki yake katika Jimbo lake kuhakikisha kwamba wananchi wake anawatendea haki, mimi nawatendea haki wananchi wangu wa Jimbo la Koani. Tumempa Waziri wa Sheria katiba tangu nilipoingia katika Baraza hili 2010, nimempa fomu zangu za kuzaliwa mpaka jana namuuliza ananambia mimi bado sijaweza kukupa na yeye yumo humu sio kwamba namsingizia. Kwamba hii sheria isiwe upande mmoja ni pande zote.

Sijaona mtu kutoka Unguja kwenye kuchukua kipande cha *ID* Pemba, lakini unakuta mtu anatoka Chokocho anakuja kwenye Jimbo la Koani anataka kipande cha *ID* tutampa vipi. Hii haki imewekwa kila kitu na shehiya yake na masheha wamepewa wajibu wao vipi wafanye wampe mtu muhusika sio mtu yeyote tu anakwenda kutaka kipande cha *ID*, anapata.

Sasa nashangaa Muwakilishi mwenzangu hapa *backbencher* mwenzangu anazungumzia Mkwajuni kule hakuna Mbunge na Muwakilishi au yeye ndio anajua sana basi achukue majimbo mawili kwa mpigo. Hii haki kwa kweli tusitumie kwamba sisi tunawajibika katika uchaguzi, sisi tutetee wananchi kama tulivyopangiwa na majimbo yetu. Majimbo tumepangiwa kila jimbo na Muwakilishi wake na Mbunge wake ukafuatilia kwamba wewe ndio mwenye majukumu. Ndio ukaona kwamba mimi nimetumia Jimbo la Koani watu kutoka Uzi, nimehakikisha nimempa Waziri fomu zangu tokea 2010, mpaka leo namaliza muda huu hajanipatia jibu hadi leo.

Sasa haki sio pande moja, haki ni pande zote tuzungumzie watu kutoka Unguja tuzungumzie watu kutoka Pemba sina ushahidi kwamba kuna watu angalau 10, waliotoka katika jimbo la Koani kwenda katika jimbo la Chake Chake kwenda kuomba *ID,* lakini nina uhakika kuna watu zaidi ya 100 wamekuja katika Jimbo la Koani kuomba kipande cha *Zan-ID*. Hilo suala haliwezekani kwa sababu kila mtu kapangiwa sehemu yake. Kwa hivyo namuomba Mhe. Hamad Masoud Hamad hoja hii aliyoileta airudishe tena jimboni kwake akaipange upya ili angoje 2015 baada ya kupiga kura ailete tena katika Baraza la Wawakilishi. Lakini hivi sasa sio wakati wake, na sijui kama atarudi kwa sababu hilo jimbo tunalichukua.

Mhe. Naibu Spika, tujiulize kulikoni hata hivi sasa hili suala linachukuliwa na kila mtu kwamba anataka ahakikishe kwamba anapata *Zan-ID*. Tunaelewa wengi vijana wa leo wanataka vipande sio kwenda nyumbani kwenda kuchukua vipande. Mimi mwenyewe ukiniona kipande changu ninacho humu ndani katika mfuko nimechukua katika jimbo la Koani, lakini sikuchukua katika jimbo la Mjini kwa sababu kule ndio jimbo langu na ndio jimbo nitakalohukumiwa na ndiko nitakapohakikisha haki zangu zote nazipata.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na wengi wamechangia nisitafute sifa katika mazungumzo haya, nizungumze kitu cha uwazi. Mchango wangu ni mdogo kwa leo, kuhakikisha kwamba wapate nafasi wenzangu kwa kuweza kuchangia hoja hii ambayo mimi sitoikubali na wenzangu nawahamasisha kwamba wasiikubali kwa sababu sio wakati wake. Ahsante sana, kwa leo hayo ndiyo maoni yangu kwa wananchi wote Wazanzibari na wananchi wote wa Jimbo la Koani, tunaipinga kwa sababu sio wakati wake. Ahsante sana.

Mhe. Abdalla Moh'd Ali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nashukuru na mimi kunipatia fursa hii ya kuzungumzia hoja hii binafsi iliyoleta hapa na Mjumbe mwenzetu wa Baraza lako tukufu.

Kwanza nampongeza sana mleta hoja hii, kwa sababu kama walivyo Wajumbe wengine ameona kwamba kuna umuhimu sasa katika nchi hii ya kuwatetea wanyonge.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba nikukumbushe tu, ikiwa wengine wanashangaa kwa nini Mjumbe kaleta hoja hii, wajumbe hao hao na wao walileta hoja kama hii mwezi wa Disemba mwaka 2013 ya kuliomba Baraza lako tukufu kutoa azimio dhidi ya vitendo vya kunyanyasa watoto na wanawake. Sasa leo tusishangae kwamba Mjumbe na yeye katumia haki yake ya kimsingi kuleta hoja hii mbele ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Naibu Spika, naomba niseme kwamba tunapokwenda vyuoni kusoma unajua ufahamu Mwenyezi Mungu katujaalia kila mmoja na wake; walimu huwa mara nyingi wanapotusainishia huwekea A, B, C, au 50, 60, 80, 90, hayo ni maumbile hayapingiki, kwa hiyo kila mmoja anaufahamu wake.

Mimi nilivyofahamu kwamba hoja hii haikuja hapa kufuta sheria yoyote iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi. Bali hoja hii imekuja kwa kuomba ridhaa ya wajumbe wako ili wapitishe azimio kuhusu haya yaliyotajwa humu.

Mhe. Naibu Spika, hoja hii imeeleza hivi anasema:

> "Na kwa kuwa kumekuwa na vitendo vya makusudi kwa upande wa watendaji wa serikali wa mamlaka zinazohusika, kuwanyima idadi kubwa ya Wazanzibari wakaazi wenye sifa."

Mhe. Naibu Spika, ndivyo ilivyosema hivi, sio wengine wanaopita njia nyengine ni Wazanzibari wenye sifa, sasa hapa hapajakiukwa katiba.

Mhe. Naibu Spika, kwa maana hiyo yeye katumia mamlaka yake kutuonyesha kwamba kuna Wazanzibari wana sifa hawajapatiwa haki hii. Kwa hiyo analiomba Baraza lako tukufu kwamba sasa tupitishe azimio, hawa ambao wana sifa na sio wengine aliyetoka Mkwajuni, sijui akapata Koani, aliyepata wapi akapata wapi, kama hana sifa asipewe. Sisi tunachokisema hapa waliyo na sifa ndio wapewe na hii hoja ndivyo ilivyokuja, haikuja kwa aina nyengine yoyote. Kwa hiyo kama wana sifa pia tutawesema kwamba na wao hawana haki ya kupata. Wakisema hivyo mimi nawashangaa sana Wajumbe wenzangu.

Mhe. Spika, kwamba Baraza lako tukufu wiki nzima iliyopita hapa tulikuwa tunazungumzia utendaji uliyopo katika serikali yetu, watendaji wetu. Wengi wakasema kwamba kuna mapungufu makubwa, sasa leo anasimama mtendaji hapa anasema kwamba waliokuwa hawajapata waende huko Mahakamani. Sasa ah! Mheshimiwa umesahau kwamba wewe umewaponda hawa, au hawa waliokuwepo huku wao wameshakuwa malaika hawana kosa hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, tunasema Sheria hii hayo ndiyo iliyowapendekeza. Pendekezo jengine yeye amesema kwamba iwatake Masheha wa Shehia zote za Unguja na Pemba kuwapatia Wazanzibari wote wenye sifa, fomu za maombi ya kusajiliwa kama Wazanzibari Wakaazi bila ya ubaguzi na bila ya usumbufu. Hivyo ndivyo alivyoomba Mjumbe mwenye kutoa hoja. Sasa hii pia iwe haitakiwi, wenye sifa.

Mhe. Naibu Spika, tunapotea, tunapotea na tunakokwenda hatukujui, Wajumbe tunakuja hapa kama alivyosema Mhe. Omar Yussuf tusiende kisiasa. Sisi tunawatetea wananchi. Hatuwajui hawa tunaowatetea watakuwa wapi. Wewe unasema mtoto mwenye umri wa miaka 18, humjui atakuwa wapi leo, kuna na kesho. Sasa hoja imekuja kuwatetea hawa na sio wengine, kwamba kuna watu wana sifa. Hoja hii imesema kwamba

> "Na kwa kuwa ahadii hizo zilitolewa na Mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar hazijatekelezwa kwa vitendo hadi sasa huku Wazanzibari wengi wakiendelea kuteseka kwa kunyimwa haki yao hiyo ya msingi kisheria."

Sasa zile ahadi walizokuwa wameziweka Mawaziri hawaja zitekeleza.

Mhe. Naibu Spika, hoja hii imekuja kuwataka hawa Mawaziri ambao waliweka ahadi watekeleze. Atakapokuja Waziri hapa atasema nina orodha kubwa Mkoani 16, sijui jimbo la wapi wako 80. Hebu Mhe. Waziri kama wewe mkweli tupe orodha, twende kisayansi maana yake sio tulete maneno tu hapa huyu hivi, twende kisayansi. Si kuna wajumbe wametoa Hoja kwamba kuna mtu ana sifa, sasa nenda ukathibitishe, kwamba huyu aliyesema Mhe. Subeiti kwamba anasifa, hebu niende nikamuone anasifa kweli au anasema tu.

Mhe. Naibu Spika, sasa hili ndio tunaloliomba kwamba hao waliowajibika kama ni Mawaziri waende kunakohusika, kwa sababu walikuja wakatoa maagizo, lakini hayo maagizo yao hayakutekelezwa hadi sasa. Kwa hiyo tunawaomba yale magizo yao yatekelezwe na maagizo yao kutekelezwa ni kuja sasa tutawapa sisi waliokuwa na sifa. Ikiwa hawana sifa wasiwape lakini waliokuwa na sifa kwa nini wasipewe. Hoja hii ndio imekuja kujenga msingi huo Mhe. Naibu Spika.

Sasa wanatokea Wajumbe wanasema inataka kuvunja Baraza la Kutunga Sheria, kaja tokea 1995. *No*, tunasema kwamba kuna Wazanzibari walio na sifa. Sasa Waziri atwambie kwamba mimi nataka hao waliokuwa na sifa niwafanyie kazi waje wanionyeshe kama wana sifa ili wasajiliwe. Sio kuja hapa tuseme maneno tu huyu hivi huyu vile, mimi nimesajiliwa Koani, yanahusu na nini, tunasema kuna watu wanasifa, sasa, Waziri na aje atwambie kwamba huyu hana huyu anayo, ndio tunachokiomba sisi hapa. Sasa hata aliye na sifa asisajiliwe.

Mhe. Naibu Spika, ukweli ni huwo kwamba kuna watu wana sifa, sasa ku- *prove by evidence* sasa ni Waziri kuja, tumemwambia mimi nina watu 18 *for example*, njoo katika jimbo nikwambie hawa, kama hawana sifa usiwape, lakini kama wana sifa kwa nini usiwape.

Mhe. Naibu Spika, mimi ni Mjukuu wa Muhammed Juma Pindua pale Mkoani wote wanamjua hapa. Je, unanikosesha? Unamwambia mwanangu kwamba yeye siye cheti changu cha kuzaliwa mimi nimeandika na paspoti

yangu ya kusafiria nikiulizwa nani nasema *African* kwa maana ya nini? Hapa ndio petu. Sasa anakuja mtu ananambia miye siye, mjukuu wangu siye, anatokana na baba Mshirazi mama Mtumbatu leo asipewe haki yake.

Mhe. Naibu Spika, wale waliofahamu vibaya wasifahamu hivyo, hoja hii imekuja hivyo. Mawaziri tuliwambia kwamba kuna mapungufu haya na watu wako tayari kuthibitisha kwamba kuna watu wanasifa. Kwa hiyo waliyo na sifa wasajiliwe, hao waliokuwa hawana tena wanaotoka Koani msiwape. Lakini walionazo wapeni ndio sheria ilivyokuja ya Baraza la Wawakilishi ilivyotungwa. Mheshimiwa ngoja nikupe kisa kidogo tu sasa hivi namalizia. Kwa sababu naona uchungu sana kusema kweli.

Mimi mwaka 2000 niliondoka nchi hii mwezi Julai tarehe 1 nikenda Uingereza. Kutoka tarehe 1 Julai mpaka tarehe 15 nilikuwepo Uingereza pale. Wakatokea vijana wakanambia hebu twende *Home Office*. Nikawauliza kuna nini? Pale kuna taratibu za kujisajili. Nikawambia hapana, mimi nimekuja na *visa* yangu *genuine* tarehe 15 narudi nyumbani. Wakanambia twende japo ukaone.

Mhe. Naibu Spika, mimi nikenda, tulipofika pale *Home Office* watu tele, wengine wanaomba sheria ya kukaa pale. Matokeo yake nikamsikia mmoja anauliza *where are you from*, basi alisema *alif, bee, tee, thee, jim, khee*! Sasa yule *Home Officer* akamuuliza *where is he from*, akamwambia *he is from Somalia*. Somalia? *Oh! no problem, you give him*. Alah! kwa sababu kasema *alif, bee, tee, thee,* akapewa sheria, akapewa haki ya ukaazi pale. Hakwenda na cheti cha kuzaliwa, hakwenda na karatasi ya Sheha, *that is the system until now*. Wewe leo umemzaa mtoto hapa hapa, mjukuu wako Sheha anakwenda anamwambia hupewi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nakushukuru.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii binafsi.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa kuanzia naanza kuwapongeza kuanzia Waziri anayehusika na Wizara hii, Mkurugenzi na Watendaji wake wote kwa kuwadhulumu wananchi Wazanzibari haki zao za msingi.

Mhe. Naibu Spika, namshukuru kwa sababu vielelezo vipo kwa nini hawapatiwi haki zao wananchi wa Zanzibar ambao wameshatimiza masharti. Sasa Mhe. Naibu Spika, Waziri tunamtaka kwa hili alifanyie kazi ipasavyo, wale wote ambao tunamletea ushahidi tunao ni huu hapa;

(*Hapa Mhe. Mjumbe anaonesha mifano ya karatasi za ushahidi*)

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri azichukue azifanyie kazi kwa muda wa mwezi mmoja. Asipofanya hivyo hii ni ishara tosha mtu kumnyima haki yake na kumdhulumu, inaweza ikaleta tatizo katika nchi hii. Tusipofanya hivyo na tusipokuwa makini tutakuja kuyapata mambo tusiyoyatarajia Mhe. Naibu Spika.

Jamani tuwe na huruma, leo utamuhangaisha mwananchi wa Kijini, kila siku anaenda Wilayani, mwananchi yule yule wa Shehia ya Kijini anashindwa na pesa ya kupata angalau andazi la asubuhi.

Leo mara sita mtu huyu anahangaishwa aende Wilayani anakwenda na targisi yake. Leo anaambiwa hivi, leo sijui magamba hapana, leo sijui hiki hakuna. Kwa nini jamani tunawahangaisha binaadamu wenzetuuu!

Ikisha serikali hii inasema iko makini kweli kweli, mbovu bwana. Haiko makini, hii serikali haiko makini hata kidogo. Kama iko makini waliotimiza masharti wangepewa haki zao bila ya kusumbuliwa. Umakini uko wapi? Mimi sioni. Umakini ukamuhangaishe mwananchi wa nchi hii anayelipa kodi katika nchi hii unamuhangaisha. Mwananchi unatakiwa umpembejekee kwa sababu anakulipia kodi katika nchi yako.

Sasa hili Mhe. Waziri ulichukulie hatua. Mimi hapa nina targisi hizi za watu wa Kandwi, naomba uzichukuwe hizi, za watu wa Shehia ya Kandwi zisizopungua arubaini na kitu. Naomba hizi mzichukuwe mumkabidhi ili zifanyiwe kazi, sio zikabidhiwe zikawekwe kwenye makabati, hizi zifanyiwe kazi.

Mhe. Naibu Spika, Sheha wa Kandwi hawapatii hata barua wananchi wa shehia yake na sio kama wametoka Pemba wamekuja pale kwa muda au hawajachukua barua Shehia kwengine wakaja pale, wamezaliwa pale pale, Pandu

Dunia, Jecha Dunia wengine Sheha huyo huyo wajukuu zake, lakini anashindwa kuwapa. Kwa nini? Wanapata maagizo.

Mhe. Naibu Spika, kwa ushahidi wa hilo nikakwambia kwamba wanapata maagizo siku ya tarehe 21/12/2014 walikwenda hawa wananchi wa Shehia ya Kandwi katika Wilaya yetu ya Kaskazini pale, baada ya kwenda walinipigia simu Mheshimiwa bona tunasumbuliwa na mimi nikaenda pale nikazungumza nao, wakanambia sijui vyeti vyao feki, wangine wamekuja na vyeti kopi, hawajaja na vyeti vya *original*, alimradi wanawahangaisha wananchi.

Mhe. Naibu Spika, kilichojitokeza kuna Mzee moja pale anaitwa Haji Mcha, huyo mzee ni mtumzima wa makamo. Yeye alikwenda kulalamika kwa Mkuu wa Wilaya wakati huo Bi Riziki yupo. Kwenda kulalamika, Mkuu wa Wilaya alichokifanya alimpigia simu Sheha wa Kandwi. Baada ya kupigiwa simu akaambiwa kwa nini huyu mzee humpi barua akenda kuchukua kitambulisho chake. Sheha alisema haya ni maagizo yenu.

Mhe. Naibu Spika, sasa mtwambie je, kweli ndiyo mna niya ya kuwapa wananchi haki zao hizi au mnawapa maagizo kwa kulinda chama chenu lazima kishinde kwa kulinda hivyo. Jamani huu si utaratibu, kwa kila mwenye haki yake naapewe Mheshimiwa. Kwa kweli wananchi tunawahangaisha, wananchi tunawakatisha tamaa na hilo sio jambo zuri, jambo ambalo wananchi linawarejesha nyuma na itakuja kupelekea huko baadaye hata litokee jambo la serikali, wananchi watakuwa hawaliungi mkono. Hata liwe lina maendeleo na manufaa kwao, kwa sababu mnawahangaisha. Haya hilo moja.

Mhe. Naibu Spika, jengine kuna hawa wengine ambao wamekwenda Gamba kuchukua vitambulisho vyao, baada ya kwenda Gamba na risiti zao, risiti wamenyang'anywa, kwa nini wamenyang'anywa wasipewe hiyo *Zan-ID* yao. Unapopeleka risiti ndio unapewa *Zan-ID* yako. Watu wa nne Mhe. Salum kasema yeye hawataji kwa majina. Mmimi nawataja, hakuna kuficha muda wa kuficha kucha umekwisha Mhe. Naibu Spika. Hapa yupo mmoja anaitwa, Mati Haji, Makame Iddi Pakacha, Pili Juma Kidongo, Ndamo Neman Ali. Shehiya ya Kusini Matemwe ukiwafatilia hawa utawapata Mhe. Waziri.

Tunawataja hawa na tunaposema masuala haya sio kwamba tunasema kwamba sisi tunabuni, tunasema kitu ambacho tuna uhakika nacho, ushahidi upo, vielelezo vyote vipo, tena hii serikali inakuwa na ugumu gani kuwashughulikia hawa wananchi kuwapa haki zao za msingi, ikisha leo wengine wanasema wanaogopa halalbadiri. Miye katika Wilaya yangu nawakusanya hawa wote, nawambia tukaeni pamoja wakati mnanyimwa haki zenu za msingi tuzisome halalbadiri, tuzizome bwana. (*Makofi*)

Baada ya kwisha kuzisoma halbadiri aliyoona Mhe. Subeti Khamis, tukae itikafu kumsukumia Mwenyezi Mungu yeye ndiye atakae tuhukumiya.

Kwa nini tusende kwa Mwenyezi Mungu, na yeye ndiye aliyetuumba sisi tumuabudu na wenye haki zao wapatiwe ipasavyo kwa nini tusipeleke kwa Mwenyezi Mungu. Kwa Mwenyezi Mungu sisi tutapeleka kwa sababu hakuna ubavu wa aina nyengine. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu mambo yote tumeshayafanya hapa watu wameshakwenda kujiandikisha, risiti tunazo hizi makoba kwa makoba, sasa tena hapa kilichobakia twende huko Mahakamani. Mwananchi wangu wa Kijini akaende Mahakamani jamani anaogopa, hata ofisi wanaziogopa, jamani hee! mambo mengine tena taireni jamani, taireni serikali hii. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli, Naona umeshaniwashia kitaa, dakika ngapi bado. (*Kicheko*)

Mhe. Naibu Spika: Dakika tatu.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Tatu?

Mhe. Naibu Spika: Ndiyo.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Haya. Mhe. Naibu Spika, kadhia hii inayowakuta ni wananchi wetu wa nchi hii, kwa hivyo tunaiomba Serikali ilifanyie kazi suala hili kwa umakini zaidi, sio wananchi wangu wa Wilaya ya Kaskazini

wakienda pale wanaambiwa mashine leo mbovu, mashine hivi leo mtu anatafuta kipesa chake anakwenda pale kwa nauli anaambiwa mashine mbovu. Jamani mashine mbovu kila siku basi hii Serikali nayo haiko makini kuwahudumia wananchi wake, kwa nini isitengeneze hizo mashine jamani. Tunaomba mashine kila iliyokuwa mbovu itengenezwe na huu ushahidi tunaokuleteeni muufanyie kazi tena ipasavyo, na mkishaufanyia kazi tupewe taarifa kwamba tayari umeshafanyiwa kazi, la si hivyo Mheshimiwa mnatengeza mambo ambayo hatutayatarajia kutokea.

Dhulma hii wanaofanyiwa wananchi ni dhulma kubwa, Mheshimiwa naona ushaniwashia kitaa, namalizia kwa kusema tena Mheshiwa ninaiomba Serikali, ninawaomba hawa Wakurugenzi wanaohusika na watendaji walifanyie kazi suala hili mara moja iwezekanavyo, wasiwasumbue wananchi. Wananchi wana hali ngumu, maisha magumu, hivi Serikali miaka 51 sasa kazi yake kuhangaisha wananchi tu!

Mhe. Spika, naunga mkono hoja halbadiri tutasoma hata mia, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Farida Amour Mohammed: Ninakushukuru Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuzungumza machache katika ripoti hii. Kwanza nianze kwa kuunga mkono asilimia mia moja. Ninavyofahamu mimi sisi tuliomo ndani ya Baraza la Wawakilishi sote ni watetezi wa wananchi kutoka maeneo tofauti. Wengine wanatetea wananchi kutoka majimboni mwao, wengine ndani ya Mawilaya yao, wengine kutoka Ofisi Kuu ya Rais Ikulu. Lakini nitashangaa sana sisi hapa tukisimama tukaambiwa hapa labda tunatafuta kura.

Mimi nataka niwaambie wawakilishi wenzangu waliomo ndani ya Baraza hili kila mmoja kura anapigiwa kutoka Jimboni mwake na anapigiwa kutoka Wilayani mwaake. Kilichopo hapa tunawatetea wananchi wetu na si ajabu kuwatetea wananchi, hatukuanza leo kwa sababu ya kuleta hoja hii. Mambo mbali mbali yakiwemo kuwatetea wananchi, wafanyakazi, wanaodhalilishwa, watoto, yote tunayaleta humu na humu ndio tunapata michango na mawazo ya kila mtu, baadae Serikali ikachukua maamuzi. Sasa tusituhumiane katika hili.

Mhe. Naibu Spika, kila mwenye haki aliyefikia umri wa miaka 18 ambaye kuwa ametimiza masharti basi ana haki ya *Zan- ID. Zan -ID* hii ni haki ya kila Mzanzibari aliyetimiza masharti. Sasa mimi nataka niseme tunawanyima watu haki zao kwa makusudi na sheria imesema aliyetimiza masharti. Hapa hatujawi kumleta mtu mwenye miaka 14 tukamtetea, aliyekuwa hana vielelezo kamili, kila tunalolizungumza hapa tunalizungumza kwa sababu ya ushahidi. Sasa Mhe. Naibu Spika, mimi nataka niseme kuna mambo matatu.

Kuna mambo yanasababishwa na masheha, sijui kwa amri ya nani, kuna mambo yanasababishwa na Ofisi ya Vitambulisho sijui kwa maslahi ya nani, sasa nianze kwenye masheha.

Mhe. Naibu Spika, nataka kwanza niiombe Serikali watufungulie Ofisi za masheha na sisi ili tuwarahisishie wananchi pahala pa kwenda kudai haki zao. Ninasema hili kwa sababu Ofisi za Masheha zote ziko kwenye majumba yao na ndani ya shehia yangu mimi ya Ole masheha wameweka agizo maalum la kuwa kila Ijumaa ndio watu wende pale kwa kupewa fomu za kuchukulia vitambulisho. Na Ijumaa hiyo moja wakienda watu waliozidi 15 wakati katika wiki nzima kaweka siku moja tu ya Ijumaa, sasa wanapokwenda huanza kuwaambia kwa nini mkaja wengi asije mmoja mmoja.

Hivi Ijumaa moja hiyo halafu watu waliomo ndani ya shehia ni zaidi ya 50 waliotimiza masharti ya umri, wana vyeti vya kuzaliwa *original* na wanakwenda pale anawaambia aje mmoja mmoja. Hivi hili ndio agizo mlilotoa Serikali kwa masheha hawa, hilo masheha wanalifanya na hilo ndilo agizo alilolitoa ndani ya shehia yangu kila Ijumaa ndio wanatoa fomu. Na Ijumaa hiyo unaweza ukenda zaidi ya mara 6 humkuti sheha na hii ni kwa sababu hakuna Ofisi maalum ya sheha. Sheha mnamuweka pale kwa mujibu wa sheria na analipwa kwa ajili ya kuwasaidia wananchi.

Sasa nashangaa sana ikawa Sheha huyu niende nyumbani kwake ukenda uambiwe saa hizi kalala, saa hizi yuko kondeni, saa hizi yuko... na siku ni Ijumaa moja. Ninamuomba Mhe. Waziri anisaidie hili, hivi hawa masheha wamewapa agizo gani la kuwapa watu haki zao kama ni siku maalum au ni kila siku, mtu atakapofikia umri wake.

Mhe. Naibu Spika, kuna watu tayari waliokwisha piga picha na wana risiti, Ofisi za Vitambulisho zote ziko katika maeneo ya mjini na watu wetu wengi wako katika maeneo ya vijijini na hali za wananchi wetu tunazijua tusijione sisi tuliomo humu ndani ya Baraza la Wawakilishi kama tunapata milioni saba (7,000,000/=) kama alivyosema Mhe. Hussein Bhaa mbali na maposho.

Mhe. Naibu Spika, haiwezekani mtu mmoja huyo kila siku apande gari kwa nauli 2000/= ende Wete akirudi akifika aambiwe njoo kesho, njoo keshokutwa, mtondogoo lakini hapewi kitambulisho. Kwa hivyo katika hili ninamuomba Mhe. Waziri atufafanulie hapa kwenye Baraza hili baada ya mtu kwishapigwa picha na kupewa risiti yake anachukua muda gani kupewa kitambulisho chake hiki cha *Zan-ID*. Kwa sababu ya kuwaonea huruma watu wetu, kwa kuwasumbua kila siku kwenda mjini na kurudi kwa kutafuta *Zan-ID* hii wakati mtu tayari keshatimiza masharti.

Jengine Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Waziri anayehusika atufafanulie hapa ndani ya Baraza hili kwa sababu ndani ya Baraza hili tuliomo wengi tunatoka katika sehemu tofauti tofauti. Wengine tulikuwa tunasuka makuti, wengine walikuwa wanauza maandazi, wengine walikuwa wakulima, wengine wavuvi, wengine wafugaji, wengine wauza dodo, wengine ndio ma-*doctors* na wengine ni wanasheria, sisi wengine si wanasheria.

Sasa hapa kila anayesimama anasema sheria, sheria, sheria, sasa ninamuomba Mhe. Waziri anayehusika atwambie hasa ni sheria ipi tunayotakiwa tuitumie ili tukawaelimishe hao wananchi wetu huko ndani ya maeneo wapate sheria hiyo ili wende wakapate haki yao hii ya msingi. Kwa sababu ninavyofahamu mimi taratibu tunazozifuata sisi tuliokuwa si wasomi, sisi tuliokuwa tunatoka huko nyuma, tukipika uji, tukiuza maandazi, tulivyowahamasisha anatakiwa mtu awe na cheti cha kuzaliwa *original* na vyeti hivi hapa vinatoka ndani ya shehia yangu, weshakwenda kwa masheha zaidi ya mara 50 lakini kwa bahati mbaya sana sheha anawakimbia; hataki kuwapa haki yao msingi. La kwanza ni hili ninalolifahamu mimi niliyekuwa si msomi.

La pili Mhe. Naibu Spika, ni risiti, hatua ya pili kuna watu hawa wana risiti hizi za muda mrefu mpaka leo hii kila siku wanahangaishwa, wanasumbuliwa, wanapelekwa na kurudishwa na kupoteza nauli mtu aliyekuwa hali yake, chakula chake cha siku moja kinamshinda. Sasa sijui sheria ipi inayotakiwa Mhe. Waziri anayehusika atwambie ni sheria ipi au ni taratibu zipi mnazotaka zifuatwe, ili hawa watu wetu wapate haki zao za msingi na sisi kukaa hapa tukawadaia watu haki zao za msingi si vibaya. Sasa nyinyi hapa hili dogo la kwenda kwa Sheha na kwenda kwenye Ofisi ya Vitambulisho hawatekelezewi haki zao, leo kila anayesimama anasema aliyekuwa hakuridhika ende mahkamani, mahkama ipi, mahkama ni zenu wenyewe, taasisi zote ni zenu wenyewe. Hivi kweli mtu anayetoka Micheweni, mtu anayetoka Tumbe kweli atakwenda mahkamani hata atizamwe, si mtu anakwenda kudharauliwa bure na kupoteza muda wake.

Mhe. Naibu Spika, ninaiomba sana Serikali iwaonee huruma raia wake kwa kuwapa haki zao hizi za msingi, nyinyi msitegemee kama hiki kitambulisho ni kwa ajili ya kupiga kura tu, kwa sababu kitambulisho hiki tumekipeleka kwenye siasa. Jamani sisi CUF ambao Pemba ni wengi na hapa Unguja tuna asilimia zaidi ya 75, sasa mimi ninataka niwaambie hivyo vitambulisho tulivyonavyo vya kupigia kura sisi vishatutosha, lakini hawa watu wana haki zao nyengine ndani ya nchi hii.

Mhe. Spika, ndani ya nchi hii vijana wetu tumewasomesha katika mazingira magumu, hawana ajira, hawana lolote. Sasa mtu hata akiamua kutoka hapa kutafuta pahali pengine pakutafuta ajira anadaiwa kitambulisho, hana mnakizuia. Kweli mnawatendea haki wananchi wetu hawa. Kwa hivyo ninaoiomba Serikali kitambulisho hiki si kwa sababu ya kupigia kura tu, hiki kitambulisho kina mambo mengi hata mimi binafsi kwa ushahidi siku moja nimesafiri na mtoto wa miaka 14 bandarini, hapo Unguja, hajafikia hata umri wa kuchukua kitambulisho naingia naye pale nikaambiwa huyu mtoto lete kitambulisho. Nikawaambia huyu mtoto hajafikia umri hana kitambulisho, basi kama hana kitambulisho asisafiri. Hivi kweli waliofikia miaka 40 na 50 hawapewi vitambulisho akapewe kitambulisho mtoto wa miaka 14.

Sasa mimi Mhe. Naibu Spika, katika hili ninaiomba sana Serikali ilichukulie hatua hili wawape watu haki zao bila ya ubaguzi wa aina yoyote.

Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru na ninaiunga mkono hoja hii asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru kwa dhati kwa kunipa fursa hii lakini zaidi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na uhai nikaweza kusimama hapa.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninamshukuru Mhe. Hamad Masoud kwa kuleta hoja hii na wengi wataniuliza kwa nini unamshukuru, ninamshukuru kwa sababu leo wananchi wetu watafahamu sheria hii ya vitambulisho vya mzanzibari, kwa sababu watu wengi walikuwa wanapotoshwa na wengi walikuwa hawajui haki zao za msingi.

Mhe. Naibu Spika, suala ambalo tunalijadili linawezekana ni suala la kikatiba na Katiba nayo imetambua uwepo wa sheria. Mheshimiwa mimi ninashangaa hata baadhi ya wenzetu hapa wanaposimama, sisi wengine pamoja na ugeni wetu lakini tunajua kwamba sheria zipo na kama viongozi sisi ndio tunapaswa tuzijue sheria, ili tuwaelekeze hao wananchi namna ya kuzifata sheria.

Sasa mwakilishi unasimama hapa unamtaka waziri akueleze sheria wakati wewe mwenyewe ndio mtunga sheria, wewe unatakiwa uwaeleze wananchi wako kutunga sheria. Mheshimiwa sheria ni namba 7 ya mwaka 2005, usipate tabu iko wazi na imeeleza kila kitu namna ya haki ya mwananchi katika kupata haki ya kitambulisho cha mzanzibari.

Mhe. Naibu Spika, tutapiga kelele sana na ninafikiri aliyeleta hoja hii kama ingekuwa makini ninamuelewa zaidi ninafikiri angetafuta namna ya kuwashauri waheshimiwa na kuishauri Serikali kutuletea sheria hii kuifanyia mabadiliko. Kwa sababu hii sheria inaonekana ina mapungufu na ina mapungufu katika maeneo mbali mbali na ndio maana watu wengi hapa waheshimiwa wenzangu wanakuwa wanapata tabu sana. Maana yake mtu anakuonesha vyeti hivi, mtu katimia miaka 18, sijui tayari ana haki ya msingi lakini pamoja na miaka 18 kuna suala la kukaa katika eneo.

Inawezekana umetimia miaka 18 Unguja au umezaliwa Unguja una miaka 3 ukaondoka ukenda ukaishi Mascut, Mascut umekaa miaka 40. Leo una miaka 40 unajua huu mwaka wa uchaguzi unakuja unakwenda kwa sheha upewe barua wende ukachukue vitambulisho. Hata kama una miaka 50 sheria bado inakukataa kwa sababu unatakiwa ukae miezi 3 mfululizo katika eneo. Na masheha nao pia wamepewa *role* katika sheria zao lazima wawe na *registration* za ukaazi wa eneo lao.

Sasa wewe si mkaazi wa shehiyani mwake hata kama umefika ukaazi muda unaostahiki hujafika, barua kutoka kwa sheha unakotoka huna. Sasa hata ufike miaka 100 bwana lakini bado sheria inakupinga kupewa barua na sheha kwenda kutafuta *Zan-ID* kwa sheha yule urudi unakotoka. Kama umetokea Pemba, kama umetokea Mascut.

Mhe. Naibu Spika, na wenzetu hawa lazima tukubali hawa wenzetu wamekaa kama kunguru maana yake kunguru unapofika usiku ndipo wanapolala sasa na wao ndivyo walivyo, ndani ya mwaka mmoja mtu huyu au ndani ya mwezi mmoja anaishi maeneo si chini ya 7. Leo yuko Pemba, kesho yuko Arusha, keshokutwa sijui yuko Mwanza sasa inakuwa kuna ugumu wa kupata hata ile haki yake ya msingi kwa sababu hapajui hasa pale anapokaa.

Sasa hilo ndio tatizo, sasa suala la kwamba wewe una miaka 18, hilo ni sehemu moja lakini sehemu nayo pia ya pili kuwa unakaa hapa Zanzibar au umekuja Zanzibar mwaka huu kwa sababu tayari uchaguzi, kweli utakuwa na haya mambo. Hilo la kwanza.

Jengine Mhe. Naibu Spika, watu wametuonesha *documents* hapa kwamba aa mavyeti, marisiti. Juzi tulipata semina na wengine wakaipinga kwa nguvu zote kwamba isifanyike namna ya wizi wa IT ulivyotandawaa duniani. Tuleteeni vyeti gunia zima lakini bado Serikali ina kazi ya kujiridhisha, hivyo vyeti vina uhalali.

Mhe. Naibu Spika, sisi wengine tulisafiri zamani sana kabla hatujawa viongozi na wakati tunasafiri paspoti zetu zilikuwa zinagongwa viza zile za muhuri wa kibao, ukenda ubalozini unaambiwa njoo kesho, unagongewa kibao unasafiri. Lakini ikafikia pahala *visa* zile zikawa zinatengenezwa Darajani, kumezagaa utazikuta Darajani unagongewa muhuri Dubai, ukenda Darajani unagongewa muhuri wa India, mabalozi wakashtuka, watu wanaingia huku, idadi ya wanaoingia wengi kwa mujibu wa takwimu za tiketi za ndege, lakini takwimu za ubalozini ndogo. Wenzetu kwa sababu ya utaalamu wao wameondosha *design* ile ya *visa* za kugongewa kibao wakenda na *visa* tulizonazo sasa hivi za *electronic* ambazo zina uhakika.

Sasa hili suala Mhe. Naibu Spika, la *forgery* limekuwa kubwa sana mimi ninafikiri nataka na Serikali ije itwambie hivyo katika kazi zao hawajagundua vyeti feki na kwa idadi gani. Hata hayo marisiti yaliyotolewa hapa watwambie mimi leo ninashangaa kila mwakilishi kutoka Pemba kutoka CUF ana marisiti, ana mavyeti wanapata wapi.

Mhe. mimi nina ushahidi na ninalitaka Jeshi la Polisi lije linihoji kuna mwakilishi wa CUF humu ndani na anatumia gari ya *Noah* kupita katika baadhi ya majimbo kuwatafuta wananchi kuwaorodhesha wapate kadi za mzanzibari, wakati sifa za maeneo hawana. Jeshi la Polisi ninalitaka lije linihoji huyo mtu ninaye na nitamtaja na wakati wowote

niko tayari kuifanya kazi hiyo Mheshimiwa. Ninazungumza with *evidence* mwakilishi wa Chama cha Upinzani yumo ndani ya Baraza, nalitaka Jeshi la Polisi lije linihoji na ushahidi ninao.

Mhe. Naibu Spika, suala la *forgery* sio Zanzibar tu Tanzania nzima. Mimi ninalishukuru sana Jeshi la Polisi la Tanzania namna walivyogundua *forgery* katika vyeti vya kuzaliwa pamoja na vyeti vya shule. Sasa leo watu wanashangaa risiti keshapewa, wewe umpe risiti umpe mpaka kitambulisho lakini kama tukikugundua hakikufuata utaratibu ana haki pia ya kunyan'ganywa. Waangalie depu letu la Polisi na tunasikia kila siku kwamba depu hili watu 40 wamekamatwa vyeti feki, wamerejeshwa.

Mtu keshafika kuanza depu, *interview* zote keshamaliza anatoka Moshi miezi mitatu depu tayari lakini baada ya utafiti wa kina kwa muda mrefu sasa suala la kuchelewa Serikali imepata mashaka kuna *duplicate* katika masuala haya, kwa hivyo Serikali lazima i-*relay* ifanye utafiti wa hivi vitu vina usahihi. Watu sasa hivi hakuna hata kimoja kisichoibiwa. Juzi hapa tumesikia mawio miezi miwili iliyopita hapa kuna mkaazi kutoka Amani fresh hapa amekamatwa na vyeti bandia vya kuzaliwa, kesi imeenda Madema. Sasa haya mambo yamezagaa, haya mambo yamekuwa makubwa sasa lazima Serikali ijenge hofu.

Mhe. Naibu Spika, mimi ningewashukuru sana waheshimiwa waliokuja na mavyeti hapa kwamba vyeti vyao wana imani wana uhakika na ni vya kweli wangepeleka huko kwenye Wilaya vinakotolewa hivyo vitambulisho vya mzanzibari, wasikuletee wewe Mhe. Spika, wakikuletea wewe sijui ufanye kazi gani. Wavipeleke huko na watu wapeleke huko sheria imetamka wazi kama hukuridhika nenda katoe malalamiko kwa Mkurugenzi, kama hukuridhika kwa Mkurugenzi nenda kwa Waziri. Leo Mheshimiwa amewakimbia hapa, ninachotaka kusema, mimi namuheshimu sana Mhe. Abdalla anam-*shout* Da Mgeni Mwenyekiti, kwamba alileta hoja binafsi ya watoto. Watoto hawana uwezo wa ku-*defend*, mtoto hana uwezo wa kufika Mahakamani lazima atetewe. Vitambulisho vya Mzanzibari anapewa mtu ambaye keshakuwa mtu mzima, ana miaka 18 ana uwezo wa kusimama popote na kudai haki yake, na ndio maana hiyo sheria tukaitengeneza hivyo, na ndio maana tukasema kama tunahisi sheria ina matatizo basi tuifanyie marekebisho ili hawa watu wapate utetezi.

Haiwezekani kwamba tumeunda sheria na sheria imeelekeza lakini baada ya kutengeneza sheria tuje hapa waheshimiwa tuje tusimame tuivunje sheria, tumtake sheha akatoe barua hata kama mtu hana haki. Sheha atafuata utaratibu unaomwelekeza, hatofuata maelekezo ya mheshimiwa kwa shindikizo.

Mhe. Naibu Spika, wamesema sana wenzetu hapa…

Mhe. Naibu Spika: Bado dakika tano.

Mhe. Ali Salum Haji: Namalizia dakika tano mheshimiwa, tunahisi masuala ya kisiasa CCM wana mambo yao, CCM ina mtaji mkubwa wa kushinda bwana. Na ndio maana hatuna wasi wasi mkitaka tutashinda, hamtaki tutashinda kwa sababu tuna mtaji mkubwa. Tuna mtaji mkubwa na sera zetu zinakubalika kwa wananchi. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, wanasema aah wengi waliwarudisha hapa watu wa Pemba hawapewi vitambulisho, mimi nataka niwaulize halafu watanijibu, watanijibu hapa kwa hoja zangu nikeshakaa au watanijibu nje kwa sababu wengi ni rafiki zangu na Mwalim Abubakar hapa ni mtu wangu hapa.

Mhe. Naibu Spika, huko Pemba tulidhani hivyo kama tungekuwa hatutoi vitambulisho vya Mzanzibari tukawapa CUF wangeshindaje kura au wale wanaopigia kura wakawachagua wao sio CUF. Tunatoa kwa CUF, kwa CCM na ndio maana wana idadi kubwa huko Pemba wanatushinda na sisi tumeridhika, tunakubali. Mimi nina imani na bado nakubali hivyo hivyo naishauri serikali hili sikatai mwenye haki yake apewe, lakini wenzetu wamekuwa wajanja katika masuala ya *duplicate*.

Mhe. Naibu Spika, siungi mkono kabisa hoja hii, siungi mkono mimi nina imani na wawakilishi wa CCM wote wataunga mkono tusiunge mkono na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwahani hatuungi mkono. Tunataka sheria ifate mkondo wake, mwenye haki yake apewe na nina imani wanapewa, lakini lazima tusimamie nidhamu na sheria. Lazima tusimamie utaratibu tusije hapa tukataka kuvunja utaratibu, kwa sababu sisi tunatetea wanachi, wananchi tunawatetea kwa haki hatuwatetei kwa dhulma. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa Jihadi vipi tena? Mheshimiwa endelea muda unakwenda.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi hii kuchangia hoja hii.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Hamad Masoud Hamad kwa kutuletea hoja hii katika Baraza hili la Wawakilishi kuhusiana na kutaka serikali kuchukua hatua za kuwatimizia Wazanzibari wote waliotimiza sifa za kisheria kuwapatia haki yao vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niseme hili ni Baraza la Kutunga Sheria, na Baraza la Kutunga Sheria wananchi wote wanatusikiliza sisi tunachokitunga, lakini niwaombe tu wawakilishi wenzangu tunatunga sheria tusichukue jazba, kwa sababu tukichukua jazba wananchi hawatotuelewa. Kwa hiyo, nawaombeni wenzangu kila mmoja ana haki ya kuchangia na kila mmoja ana haki ya kutoa maoni yake, lakini tutambue hiki ni chombo cha kutunga sheria. Sasa tukisema kama tunachukua jazba itakuwa wananchi wetu hawatotuelewa.

Mhe. Naibu Spika, pili niwapongeze wale waliosema kwamba hawaungi mkono hoja hii, hii ni haki yao. Halafu niwapongeze vile vile wale wanaowashawishi wenzao kwamba wasiunge mkono hoja hii, lakini ningesema kwamba wasiwashawishi kwa sababu watu wote humu wana akili zao timamu hawana haja ya kuwashawishi. Sababu ya kusema hivyo kwamba niwaunge mkono wale waliokuwa hawataki kuunga mkono hoja hii, ni kwa sababu Mhe. Naibu Spika watu hawa tayari wao wanavyo vitambulisho na wazee wao, na watoto wao, na wajukuu zao na ndio maana wakasema kwamba hatuungi mkono hoja hii. Kwa hiyo nasema nawapongeza sana.

Mhe. Naibu Spika, jengine niseme kwamba tusihadaike jamani, tusihadaliwe na ulimwengu, tusihadaliwe na vyeo, tusihadaliwe na uzima. Hii ni haki ya kila mtu na serikali ndio ambayo inayotoa haki ya kila mtu lakini sasa leo iweje kwamba tuseme hawaungi mkono hawa kwa sababu ya kwamba wao tayari wanavipata vitambulisho hivyo.

Mhe. Naibu Spika, pia nataka niseme kwamba sheria ni msumeno, sheria ni msumeno inakereza kwenda mbele na kurudi nyuma na Waswahili husema kwamba "mambo ni kangaja huenda yakaja". Lakini tunasema 2015 tusije tukalaumiana wala tusioneane haya, hakuna cha kuficha na hii yote kwamba wanasema hawaungi mkono wenzetu ni kwa sababu wanajua 2015 ni hakika chama kinaingia Ikulu, CUF. Hii ni hakika hakuna siri, hakuna aibu, hakuna cha kuficha, sasa hili lote ni kwamba wote hawaungi mkono, wafanye fujo wanavyotaka. Lakini tunasema na sisi tuko tayari lakini hatulipizi kisasi. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, pia nisome katika kifungu cha 3 kinachosema kwamba "kwa kuwa Baraza la Wawakilishi limetunga sheria Nam. 7 ya mwaka 2005 ambayo imeanzisha utaratibu wa usajili wa Wazanzibari Wakaazi na kuwapatia vitambulisho vya Uzanzibari Mkaazi *Zan-ID* kwa kila Mzanzibari aliyetimiza sifa za kisheria". Sasa hapa niulize hii sheria iliyotungwa hapa tuseme ina maana ni kazi bure, kwa sababu sheria imetungwa kila mtu ana haki ya kupata haki yake aliyekwishatimia umri wa miaka 18. Leo hii sheria tunaikiuka inakuwa tunakuja hapa kufanya kazi ya bure, kwamba sheria tunatunga na hatimae inakiukwa, leo kwa nini mtu keshatimia umri wa miaka 18 asipate haki yake. Hii itakuwa ni sheria gani ambayo kuwa hatuifuati na kwamba tumeitunga sisi hapa wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, naomba sheria zifuatwe lakini Waswahili husema kwamba "tumbili akimaliza miti anakuja mwilini" na sisi hivi sasa tunasema kwamba hatuji tena kwa waziri, tunamuomba Mhe. Rais mwenyewe aliingilie kati suala hili watu wapewe haki zao. Leo Rais mzima anasikia hali kama hii hawezi kuliingilia suala kama hili na hawa ni watu wake waliomo katika nchi yake.

Kwa kweli jamani tunafika wapi hili tuliangalie ni hatari kubwa sana, tena kubwa sana tusiringie madaraka, tusiringie uhai, tusiringie pumzi zina mwisho, pumzi zina mwisho, iko siku utakuja kutaka yule mwenzako na yeye akufanyie kama vile lakini tunasema hatulipizi kisasi na yafanywe yote yanayofanywa, lakini katu tunasema hatulipizi kisasi, hata tuingie madarakani leo sisi hatulipizi kisasi na aliye na haki yake atapata haki yake atapata haki yake, na aliyekuwa hana haki hapati haki yake. Hili naomba lieleweke.

Mhe. Naibu Spika, pia niseme kwamba watu wengi humu wanamlaumu sheha, sheha yeye hana matatizo lakini matatizo yote ya sheha yanatokana na juu kwa viongozi wake, hawezi akawakiuka viongozi wake kwa hiyo tusiwalaumu masheha, tuwalaumu viongozi wa masheha ndio wanaofanya hivi.

Leo kwa nini Mhe. Naibu Spika watoto wetu wateswe tena si watoto tu mpaka watu wazima ambao tayari wana miaka 50 hawana vitambulisho, jamani hawa pia tuseme hawajafikia kupiga kura hapa. Ushahidi tunao hebu waziri twendeni Pemba tufuatane mguu kwa mguu mkawaangalie watu ambao watu wazima miaka 60 na wajuu zao hawana vitambulisho hawapewi kwa nini. Jamani Mzanzibari anazaliwa hapa asipewe haki yake apewe mtu ambaye anatoka Bara, kwa siku mbili tayari anapewa kitambulisho. Jamani dhulma hii tuangalie watoto wetu, tuangalie hatma yetu, tusiangalie hapa tu tuone na pale, wala tusiangalie sisi tuangalie na watoto wetu, na wao wana haki ya kupiga kura, na wao wana haki na nchi yao.

Mhe. Naibu Spika, naomba hili lieleweke sana na namuomba Mhe. Waziri hili alichukue, Makamu wa Pili upo unasikia hili suala tumeshachoka, tumeshachoka kwa sana tu kwa nini leo mtu anazaliwa hapa na ni mkaazi wa hapa na tangu miaka enzi na enzi asipewe haki yake. Jamani basi tuwatafutieni pahala watu hawa tuwaweke kama hapa sio pao, tuwatafutieni pahala watu hawa tuwatenge kwa sababu ikiwa wao hawana haki ya kupiga kura na leo mtu ikiwa hana kitambulisho kusafiri hasafiri, leo mtu akiwa hana kitambulisho hata ile kula yake hatimae ataikosa. Jamani tunaelekea wapi, hii ni serikali nzima ambayo inasikia yote hayo. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru ahsante.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi nikaweza kuchangia.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia jioni hii na mimi nikapata nafasi ya kuchangia hoja binafsi ya Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Hamad Masoud Hamad kuhusiana na kuitaka serikali kuchukua hatua za kuwatimizia Wazanzibari wote waliotimiza sifa za kisheria haki yao ya kuwapatia vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mkurugenzi wa Vitambulisho, niwapongeze Waheshimiwa Masheha kwa kazi nzuri wanayoifanya, nawambia waendeleze kufuata sheria kama ilivyokuwa wazi.

Mhe. Naibu Spika, mimi niwakumbushe wenzangu Wajumbe wa Baraza hili kama walivyokuwa wamesema sheria hii imepitishwa humu ndani kwenye Baraza hili tukufu. Ni kweli lakini naona kidogo katika hotuba zao wanazochangia hapa huwa wanasahau.

Mhe. Naibu Spika, juzi tu ilikuja hoja ya vitambulisho kupitia kwa Mhe. Haji Omar Kheir, alitoa funzo jengine jipya hapa kuwafahamisha sheria hii ya vitambulisho, akawaelekeza kila kitu, lakini naona bado Waheshimiwa Wawakilishi kuna wengine vichwa vyao vizito. Kwa sababu ni juzi tu katika Baraza hili hili Mhe. Haji aliwafahamisha akawaambia kwamba mwenye malalamiko basi akate rufaa, lakini leo nashangaa kila anayesimama Mwakilishi hapa analeta vyeti vyake hapa, analeta mbele ya Naibu Spika, sasa Naibu Spika avifanye nini.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu Mhe. Waziri kasema kazidi kuwafahamisha, kazidi kuwaelekeza asiyefahamu sheria iko wazi, sasa tunalalamika nini jamani. Halafu malalamiko hayo yanakuja wakati huu karibu tunakwenda kwenye uchaguzi, kwa sababu kitambulisho hiki hakihusiani na uchaguzi tu kina mambo tele mbona huko nyuma hakijaletwa. Tangu kilipopitishwa humu kwenye Baraza haijaletwa hoja binafsi. Kwa sababu kuna waheshimiwa humu tayari wanaogopa kusema kweli hasa wanaogopa, wanaogopa kuhusu vitambulisho ndio maana wakajidai kuleta hoja hapa, ili tuone kuna watu hawafati sheria. Lakini mimi naiomba serikali ifate sheria kama ilivyokuwa wazi, masheha waendelee na kazi yao kama kawaida mtu aliyekuwa hajafikia muda wa kukaa katika eneo asipewe barua ya kwenda kuchukua vitambulisho.

Mhe. Naibu Spika, kuna kipindi humu humu Barazani Mhe. Mwinyihaji Makame alituambia kuna vitambulisho tele alitoa data kila sehemu vilipo vitambulisho, lakini mpaka muda huu vitambulisho vipo haoni kama hiyo serikali imeingia hasara, hivyo vitambulisho vilivyokuwa wamekwenda kujiandikisha kina nani. Wajiulize vitambulisho hivi kajiandikisha nani mbona hawaendi kuvichukua wanaogopa, waende wakachukue. Hawaendi kuchukua kwa sababu wanajua wakienda sehemu nyengine watajuulikana.

Sasa kama wao wanaweza wakachukue hivyo vitambulisho vilivyokuwepo halafu ndio aanze kulalamiko, sio walalamike vitambulisho vyengine vipo serikali inaipa hasara vitambulisho viko kibao. Mnalalamika ovyo humu hatuandikishwi, Mhe. Mwinyihaji akachukua hatua watu wakaandikishwa hapa haya vitambulisho tayari kachukueni, hamna wenyewe hawajuulikani wamekwenda wapi? Wenyewe wamekwenda wapi, mnapenda kuleta lawama humu Barazani kwani humu Barazani ndio jukwaa la siasa, tusubiriane nje huko tukaelezane, humu sheria ifanye kazi yake. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa vile watu wengi wameshasema naamini waheshimiwa waliokuwa hawajafahamu leo hii watakuwa wamefahamu, wasilalamike tu wafahamu sheria iliyokuwepo wazi tena wafate. Mimi naiomba serikali ifanye kazi zake isipelekeshwe na watu waliokuwa wanataka kutupelekesha, sheria iko wazi imepitishwa humu ifatwe. Baada ya kusema maneno hayo siungi mkono hoja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa tusikilizane tumebaki na dakika 10 wachangiaji wengi nampa Mhe. Salma Mohammed Ali amalizie muda uliokuwepo.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuichangia hoja hii binafsi ya Mjumbe Mhe. Hamad Masoud Hamad, mwakilishi makini.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kuanza mchango wangu naomba niwape pole wale wenzetu waliofikwa na matatizo jana walipotoka katika mkutano, na pia niwape pole wale wazazi wa kijana ambaye ametangulia mbele ya haki kwa sababu kila mmoja na mauti Mwenyezi Mungu aliyompangia, lakini vile vile nasema mimi sina uwezo wa kumpeleka mtu kwa Mwenyezi Mungu. Lakini vile vile hata kama mtu ana minyororo nimeizuia sina uwezo wa kumzuia asifike kwa Mwenyezi Mungu, lakini nawaomba wazazi hawa wawe na ustahamilivu kwa hakika najua wamepata maumivu mazito kwa sababu na mimi ni mzazi na najua uchungu wa uzazi; mwanao kuondoka ukarudishiwa ni maiti, kwa kweli inasikitisha sana.

Kama tulivyoambiwa yeyote yule aliyefanya jambo jema hata kama ni punje ya mchanga basi Mwenyezi Mungu atamlipa kwa wema wake, na yeyote yule aliyefanya jambo baya hata kama ni punje ya mchanga Mwenyezi Mungu atamlipa ubaya wake. Naomba wazazi wa mtoto huyu wawe na subra, hakika Mwenyezi Mungu atamlipa yeyote aliyesababisha mauti ya kijana huyu.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba niende kwenye hoja na kwa kweli mimi sitozungumza sana kwa sababu mazungumzo mengi yameshaelezwa na vielelezo vimeoneshwa, lakini naomba niseme kwa kweli tatizo hili la vitambulisho vya Uzanzibari ni kubwa. Ni kubwa na tatizo hili linasababishwa na serikali yenyewe kuwanyima haki wananchi wake ambao wana haki ya kupata vitambulisho hivyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli mimi nashangaa sana serikali kupitia taasisi zake baada ya kuwatetea wananchi wao wakapata haki zao, wao ndio wanaozuia kupata haki zile. Sheria Nam. 7 ya mwaka 2005, kifungu cha 14, kifungu kidogo cha (1a) kinasema "ni kosa la jinai kwa kila Mzanzibari Mkaazi aliyetimiza masharti kuwa hana kitambulisho hiki" na adhabu hapa zimeelezwa.

Mhe. Naibu Spika, ni jambo la kusikitisha na naomba niendelee kwanza kusema mwezi mmoja nyuma nilikuwepo *Islamic Bank* pale walikuja wenzetu Watanganyika kufungua *account* nikiwa nimekaa kitako pale nasubiri huduma. Watu hawa walitakiwa watoe kitambulisho cha Uzanzibari Mkaazi, walijibu kama hawana na wakasema kama sisi hatujapata kwa sababu tumekuja juzi tu, lakini tumeambiwa baada ya wiki moja tutavipata vitambulisho. Mhe. Naibu Spika, narudia kusema kwamba kwa kweli naishangaa sana serikali kuwanyima haki wananchi wake na ikawapa haki wale waliokuwa hawana haki.

Mhe. Naibu Spika, kuna viongozi hapa, viongozi wetu wa serikali husimama hapa mbele wakatwambia kama wananchi wafuate sheria, nashangaa sana Baba mlezi kumkataza mtoto wake asilewe, unamwambia mtoto wako asilewe wakati wewe unaanguka na chupa njiani.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli linasikitisha, mimi nilitegemea viongozi wetu wawambie wananchi wafate sheria lakini wao wangelifata mwanzo sheria. Sheria inasema kila mtu aliye na haki apewe kitambulisho, na aliyetimiza masharti ikiwa hana kitambulisho basi adhabu inaonekana. Sasa ikiwa hawa hawana kitambulisho kwa nini hamuwapi adhabu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, inaonesha serikali hawafuati sheria hata moja kwa sababu ama wangeliwapa vitambulisho wakati wameshatimiza sheria au wangeliwahukumu kwa kuwa hawakutafuta vitambulisho na tayari wameshatimiza umri.

Mhe. Naibu Spika, ni jambo la kushangaza leo hapa kuna watu wanasema eti mtu anatoka Pemba anakuja Jimbo la Unguja anataka apewe *Zan-ID.* Mimi nashangaa sana kuwasema Wapemba wanaokuja Unguja na wakataka *Zan-ID*

lakini nipo *Islamic Bank* pale watu kutoka Tanganyika wanasema tumeambiwa baada ya wiki moja tutapata *Zan-ID*. Hivyo kweli katika visiwa hivi ni bora Mpemba ana tatizo kuchukua kitambulisho Unguja lakini Mtanganyika wa wiki moja hana tatizo kuchukua kitambulisho?

Mhe. Naibu Spika, naomba sana kila aliye na haki ya kupata kitambulisho awe ni Mmakonde, ni Mnyamwezi, ni Mpemba ilimradi ikiwa ameshatimiza sheria basi apewe kitambulisho.

Mhe. Naibu Spika, lakini tunaosema masheha ni haki tuwaseme, lakini naamini ni maagizo kutoka juu. Katika Jimbo la Wawi kuna sheha mmoja maarufu sheha huyo. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwanza nimshukuru Mhe. Salma umepata na wewe muda kidogo wa kukohoa, tunakushukuru. Niwashukuru Wajumbe wote kwa pamoja bado ajenda yetu tumekusudia tuimalize kesho na tayari wachangiaji jumla walikuwa ni 30 sasa wamebakia kama wachangiaji sita na mawaziri watano. Kwa hiyo, tunatanguliza wachangiaji watatu kesho tukijaaliwa waje mapema waanze wao mmoja ni Rufai Said Rufai, Mhe. Panya Ali Abdalla na baadae Mhe. Machano Othman Said wengine tutakuja endeleza na mawaziri waliokuwa tayari wameshaniletea majina wa kwanza ni Mhe. Abubakar Khamis Bakary, Mhe. Abdilahi Jihadi Hassan, Mhe. Juma Duni Haji, Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban na Mhe. Mohammed Aboud Mohammed.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, nilileta mapema au jina langu hukuliona Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika: Nasema bado wawakilishi sita nimetanguliza watatu wa mwanzo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Umeanza kuingia kwa mawaziri.

Mhe. Naibu Spika: Wewe umo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Haya.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe baada ya maelezo hayo naomba sasa niahirishe kikao chetu hadi kesho siku ya Jumanne tarehe 31/03/2015 saa 3:00 asubuhi.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliakhirisha mpaka kesho tarehe 31/03/2015 saa 3:00 asubuhi)